# NIDHAMU YA UISLAMU

Taqiuddin An-Nabahani

Hizb ut Tahrir

**<u>Chapa ya Uhariri wa 1440H / 2019M</u>**

1. NJIA YA IMANI.

2. AL-QADHAA WA AL-QADAR.

3. UONGOZI WA KI-FIKRA KATIKA UISLAMU.

4. NAMNA YA KUBEBA ULINGANIZI WA KIISLAMU.

5. HADHARA YA KIISLAMU.

6. NIDHAMU YA KIISLAMU.

7. HUKMU YA SHARI'AH.

8. AINA ZA HUKMU ZA KISHARI'AH.

9. SUNNA.

10. KUIGIZA VITENDO VYA MTUME (SAW).

11. KUTABANNI HUKMU ZA KISHARI'AH.

12. KATIBA NA KANUNI.

13. AKHLAQI KATIKA UISLAMU.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيم

## 2: NJIA YA IMANI

Mwanadamu huendelea kwa fikra alizonazo juu ya uhai, ulimwengu na binadamu na mahusiano yake yote na (yaliyoko) kabla ya maisha ya duniani na (yaliyoko) baada yake. Basi hapana budi ila kubadilisha kijumla na kimsingi fikra zilizobebwa na mwanadamu. Na mahala pake kuwekwa fikra nyengine itakayo muendeleza mbele, kwa sababu fikra ndiyo inayozalisha fahamu juu ya vitu, na kumakinisha fahamu hizi. Mwanadamu hupeleka mambo yake duniani kwa mujibu wa fahamu alizo nazo juu ya mambo hayo. Fahamu za mwanadamu kwa ampendae huathiri mahusiano yake na yeye, kinyume na mahusiano yake na mtu anaemchukia kwa sababu ya chuki alizozibeba juu yake. Na pia ni tofauti na mahusiano yake na mtu asiyemjua, asiye na ufahamu wowote juu yake. Basi mwenendo wa mwanadamu umefungamana na fahamu zake. Tukitaka kubadilisha mwenendo duni wa mwanadamu na kuufanya kuwa mwenendo wa kimaendeleo, basi hapana budi kwanza kubadilisha ufahamu wake.

إِنَّ اللَّهَ لاَ يُغَيِّرُ مَا بِقَوْمٍ حَتَّى يُغَيِّرُوا مَا بِأَنفُسِهِمْ (الرعد: 11

"*Hakika Mwenyezi Mungu habadili waliyonayo watu mpaka wabadili yaliyomo katika nafsi zao*" [TMQ 13:11]

Njia pekee ya kubadilisha ufahamu ni kwa kuwekwa fikra juu ya uhai wa duniani ili upatikane ufahamu sahihi kupitia kwake. Fikra juu ya maisha ya duniani haitosimama msimamo utakao zaa natija ila baada ya kupatikana fikra juu ya ulimwengu, uhai na binadamu na kilicho tangulia maisha ya duniani na baada yake, na mahusiano yake na kilicho kabla yake na kilichoko baada yake. Hii ni kwa kuwekwa fikra jumla (*fikra kulliyya*) juu ya kilichoko nyuma ya ulimwengu, binadamu na uhai. Kwani hii ndio fikra kitegemeo (*qa'ida fikriyya*) ambayo juu yake hujengwa fikra zote kuhusu maisha. Kuwekwa fikra jumla juu ya vitu hivi ndio tatuo la tatizo kubwa kwa binadamu. Na pindi litakapotatuka tatizo hilo hutatuka matatizo yote yaliyobakia, kwani matatizo hayo ni sehemu yake au ni matawi yake. Lakini tatuo hili halileti mwamko sahihi ila ikiwa ni tatuo sahihi linalo afikiana na umbile la mwanadamu na kukinaisha akili yake, basi hujaza moyo wake utulivu.

Wala haiwezekani kufikia tatuo sahihi ila kwa fikra angavu iliyo kamilika (*fikra mustaniir*) juu ya ulimwengu, binadamu na uhai. Kwa hivyo ni juu ya wenye kutaka mwamko na kusonga mbele katika njia ya maendeleo kwanza watatue tatizo hili, utatuzi ulio sahihi kupitia fikra angavu iliyo kamilika. Na tatuo hili ndio aqida, na pia ni fikra kitegemeo ambayo juu yake hujengwa fikra zote za matawi juu ya mienendo katika uhai na nidhamu za maisha.

Uislamu umelilenga tatizo hilo kubwa na kulitatua kwa mwanadamu kwa tatuo linalo afikiana na umbile la mwanadamu na kukinaisha akili yake na kuujaza moyo wake utulivu. Na ukalazimisha kwa anayetaka kuingia ndani yake (ndani ya Uislamu) kutegemea kukiri tatuo hili, kukiri kunakotokana na akili. Kwa hivyo Uislamu umejengwa juu ya msingi mmoja nao ni aqida. Ambayo ni kuwa nyuma ya ulimwengu, uhai na binadamu kuna muumba aliyeviumba vyote hivyo, na kuumba kila kitu, naye ni Mwenyezi Mungu. Na kwamba muumba huyu aliumba kila kitu ambacho kabla ya kuumba kwake havikuwepo, na pia akaumba maumbile (*wajaba al-wujud*). Na kuwa Yeye si kiumbe, na lau angekuwa kiumbe basi asingekuwa muumba. Na sifa yake kama muumba hulazimisha kwambe Yeye si kiumbe, na hulazimisha kwamba Yeye ndiye aliyeumba maisha haya, kwa sababu vitu vyote humtegemea Yeye kuwepo wala Yeye hategemei chochote.

Ama kuhusu vitu vilivyoumbwa hapana budi ila kuwepo muumba, hii ni kwa sababu vitu vinavyotambuliwa na akili ni binadamu, uhai na ulimwengu. Vitu hivi vina kikomo na ni dhaifu, pungufu na humhitaji mwengine. Binadamu ana kikomo kwa sababu hukuwa katika kila kitu kwa kiwango ambacho hakivuki mipaka maalum, hivyo yeye ni mwenye kikomo. Uhai nao una kikomo kwa sababu hudhihirika kibinafsi tu na hushuhudiwa kihisia kwa kumalizika kwa mtu binafsi, hivyo uhai una kikomo. Ulimwengu pia una kikomo, kwa sababu ulimwengu ni mjumuiko wa sayari (nyota, jua, sayari zenyewe, mwezi na vyenginevyo), na sayari hizo zina kikomo, na mjumuiko wa vitu vyenye vikomo ni kuwa vina kikomo kiwazi na kiakili. Kwa hivyo binadamu, uhai na ulimwengu bila shaka yoyote vina kikomo.

Na pindi tunapo kiangalia kilicho na kikomo tutakikuta kuwa si cha kudumu milele, na lau kingelikuwa cha kudumu milele kisingekuwa na kikomo. Basi hakuna budi kwa kila chenye kuwa na kikomo kuwa ni kiumbe kilicho umbwa na mwengine. Na huyu mwengine ni muumba wa binadamu, uhai na ulimwengu. Na yeye ima ni kiumbe aliyeumbwa na mwengine au amejiumba mwenyewe au ni wa kudumu milele aliyeumba uhai huu. Ama kuwa yeye ni kiumbe aliyeumbwa na mwengine, hilo ni batili kwa sababu angekuwa na kikomo. Ama kuhusu kujiumba mwenyewe hilo pia ni batili kwa sababu haiwezekani kuwa ni kiumbe na muumba wa nafsi yake kwa wakati huo huo mmoja. Basi hapana budi kuwa yeye ni muumba anayedumu milele aliyeumba uhai huu naye ni Mwenyezi Mungu.

Kila mwenye akili hufahamu mujarad wa kuwepo vitu anavyovihisi ni lazima vitu hivi vina muumba aliyeviumba kwa kuwa vyote vinadhihirisha kuwa vina upungufu, havijitoshelezi na vinamuhitajia mwengine. Basi kwa hakika hivyo ni viumbe. Kwa hivyo hutosha kutizama kitu chochote katika ulimwengu, uhai na binadamu ili kutoa dalili kwacho kuwepo kwa muumba muendeshaji. Tutakapo tizama nyota yoyote miongoni mwa nyota zilizoko ulimwenguni, au kutafakari dhihirisho lolote miongoni mwa madhihirisho ya uhai, au kuzingatia kiungo chochote cha mwanadamu, hutujulisha kwa dalili iliyowazi ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo tutakuta kuwa Al-Qur'an Al-Kariim huupeleka mtazamo wetu kwa vitu, na humlingania mwanadamu aviangalie na aangalie vilivyovizunguka na vilivyoshikamana navyo ili avitumie kujenga hoja ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu. Na pindi anapovitizama vitu jinsi vinavyo muhitaji mwengine, hufahamu kutokana navyo fahamu ya kukatikiwa kuwepo Mwenyezi Mungu, muumba anayeendesha viumbe. Zimekuja ma-mia ya Ayah kwa maana hiyo. Amesema Mwenyezi Mungu katika Surat Al-Imran:

**إِنَّ فِي خَلْقِ السَّمَاوَاتِ وَالأَرْضِ وَاخْتِلاَفِ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ لآيَاتٍ لأُولِي الأَلْبَابِ (آل عمران: 190)**

"*Katika kuumbwa mbingu na ardhi na mfuatano wa usiku na mchana ziko dalili (za kuonyesha kuwepo Mwenyezi Mungu mmoja) kwa wenye akili*" [TMQ 3:190]

Na anasema Mwenyezi Mungu katika Surat Ar-Rum:

**وَمِنْ آيَاتِهِ خَلْقُ السَّمَاوَاتِ وَالأَرْضِ وَاخْتِلاَفُ أَلْسِنَتِكُمْ وَأَلْوَانِكُمْ (الروم: 22)**

"*Na katika dalili zake ni kuumba mbingu na ardhi na kutofautiana lugha zenu na rangi zenu*" [TMQ 30:22]

Na amesema Mwenyezi Mungu katika Surat Al-Ghashiya:

**أَفَلاَ يَنْظُرُونَ إِلَى الإِبِلِ كَيْفَ خُلِقَتْ - وَإِلَى السَّمَاءِ كَيْفَ رُفِعَت - وَإِلَى الْجِبَالِ كَيْفَ نُصِبَتْ - وَإِلَى الأَرْضِ كَيْفَ سُطِحَتْ (الغاشية:20-17)**

"*Je: Hawatizami ngamia jinsi walivyoumbwa. Na mbingu jinsi zilivyoinuliwa.Na milima jinsi ilivyo thibitishwa. Na ardhi jinsi ilivyo tandazwa*" [TMQ 88:17-20]

Na amesema Mwenyezi Mungu katika Surat At-Tariq:

**فَلْيَنظُرْ الإِنسَانُ مِمَّ خُلِقَ - خُلِقَ مِنْ مَاءٍ دَافِقٍ - يَخْرُجُ مِنْ بَيْنِ الصُّلْبِ وَالتَّرَائِبِ (الطارق: 7-5)**

"*Hebu naajitizame mwanadamu ameumbwa kwa kitu gani. Ameumbwa kwa maji yatokayo kwa kuchupa. Yatokayo katikati ya mifupa ya mgongo na kifua (mbavu)*" [TMQ 86:5-7].

Amesema Mwenyezi Mungu katika Surat Al-Baqarah:

**إِنَّ فِي خَلْقِ السَّمَاوَاتِ وَالأَرْضِ وَاخْتِلاَفِ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ وَالْفُلْكِ الَّتِي تَجْرِي فِي الْبَحْرِ بِمَا يَنفَعُ النَّاسَ وَمَا أَنزَلَ اللهُ مِنْ السَّمَاءِ مِنْ مَاءٍ فَأَحْيَا بِهِ الأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا وَبَثَّ فِيهَا مِنْ كُلِّ دَابَّةٍ وَتَصْرِيفِ الرِّيَاحِ وَالسَّحَابِ الْمُسَخَّرِ بَيْنَ السَّمَاءِ وَالأَرْضِ لآيَاتٍ لِقَوْمٍ يَعْقِلُونَ (البقرة: 164)**

"*Hakika katika kuumbwa kwa mbingu na ardhi na kutofautiana usiku na mchana na vyombo ambavyo hupita katika bahari kwa viwafaavyo watu, na maji aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu kutoka mawinguni na kwayo akahuisha ardhi baada ya kufa kwake, na akaeneza humo kila aina ya wanyama, na mabadiliko ya pepo na mawingu yanayoamrishwa kupita baina ya mbingu na ardhi, zimo dalili kwa watu wenye akili*" [TMQ 2:164]

Na aya nyenginezo zenye kumlingania mwanadamu kutizama mtazamo wa undani katika vitu na vilivyo vizunguka na vilivyo fungamana navyo. Na kuvitumia kama dalili ya kuwepo muumba mwenye kuviendesha, ili iwe imani yake juu ya Mwenyezi Mungu imani thabiti iliojengeka kiakili na kwa dalili.

Ndio, imani juu ya muumba anayeendesha ni suala la kimaumbile kwa kila mwanadamu, isipokuwa imani hii ya kimaumbile huja kupitia njia ya hisia. Njia hii ikiwachwa peke yake haidhamini mwisho mwema wala msimamo wa kudumu. Hisia mara nyingi humfanya mtu aamini vitu visivyo na uhakika wowote, lakini hisia humdanganya kuziamini kama sifa za lazima na akatumbukia katika ukafiri na upotevu. Ibada ya masanamu, uzushi, na visa vya urongo (*turhat*) zote ni natija ya makosa ya kihisia. Kwa sababu hiyo Uislamu haukuwacha njia ya imani kuwa ni hisia pekee, ili Mwenyezi Mungu asipewe sifa zinazogongana na Uungu wake au kushirikishwa na vitu au kumfanya aweza kujiunganisha na vitu vya ki-mada au kuwaza uwezekano wa kujikurubisha kwake kwa kuabudu vitu vya ki-mada, kukampelekea kwenye ukafiri au ushirikina au katika hawaa na uzushi, (mambo haya) ambayo yanapingwa na imani ya kweli. Kwa sababu hii Uislamu umelazimisha kutumiwa akili pamoja na hisia, na ukamuwajibisha Muislamu kutumia akili yake pale anapomuamini Mwenyezi Mungu. Na ukakataza kuigiza (*taqliid*) katika aqida, basi kwa hivyo Uislamu ukaifanya akili kuwa ni muamuzi wa imani kwa Mwenyezi Mungu. Amesema Mwenyezi Mungu:

**إِنَّ فِي خَلْقِ السَّمَاوَاتِ وَالأَرْضِ وَاخْتِلاَفِ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ لآيَاتٍ لِأُولِي الأَلْبَابِ(آل عمران: 190)**

"*Kwa hakika katika kuumbwa mbingu na ardhi, na tofauti ya usiku na mchana, ziko dalili kwa wenye akili*" [TMQ 3:190]

Kwa hivyo imekuwa ni wajibu wa kila Muislamu kufanya imani yake iwe imetokana na mazingatio, uchunguzi na kutazama, na iamue akili uamuzi wa kukata katika imani juu ya Mwenyezi Mungu. Na mwito wa kuutazama ulimwengu ili kutambua mwenendo wake na kujenga imani kwa muumba wake amekaririwa na Qur'ani ma-mia ya mara katika sura tofauti. Yote (miito hiyo) inalenga kwenye nguvu za akili za mwanadamu azingatie na atafakari ili imani yake itokane na akili na dalili. Na humtahadharisha kuchukuwa kutoka yale aliyoyakuta nayo wazee wake bila kufikiri wala kuzingatia juu yake na kuamini kidhati kwa kufikia haki. Hii ndio imani inayolinganiwa na Uislamu, wala si ile imani inayoitwa 'imani ya wakongwe.' Bali ni imani angavu iliyokamilika yenye

kuyakinisha kwa aliyetazama na kutazama kisha akatafakari na kutafakari kisha akafika kwenye yakini juu ya Mwenyezi Mungu aliyetukuka uweza wake, baada ya kutumia njia ya kutazama na kutafakari.

Pamoja na uwajibu wa mwanadamu kutumia akili ili kufikia imani juu ya Mwenyezi Mungu, lakini haimkiniki kwa mwanadamu kudiriki vilivyoko juu ya hisia zake na juu ya akili yake. Hii ni kwa sababu akili ya mwanadamu ina kikomo na nguvu zake pia zina kikomo; vyovyote itakavyokua na kuendelea, kuna kikomo ambacho haitakivuka. Kwa hivyo kudiriki (kufahamu) kwake kuna kikomo kwa hivyo hapana budi iwe na kasoro isiweze kudiriki dhati ya Mwenyezi Mungu na isiweze kujua uhakika wake, kwa sababu Mwenyezi Mungu yuko juu ya ulimwengu, binadamu na uhai. Akili ya mwanadamu haidiriki uhakika (wa mambo) yaliyo nyuma ya ulimwengu, binadamu, na uhai, kwa hivyo hushindwa kudiriki dhati ya Mwenyezi Mungu. Wala haisemwi: Vipi kumuamini Mwenyezi Mungu kiakili pamoja na kuwa akili yake inashindwa kudiriki dhati ya Mwenyezi Mungu? Kwa sababu imani ni kuamini kuwepo kwa Mwenyezi Mungu na kuwepo kwake hufahamika kwa kuwepo viumbe vyake, navyo ni ulimwengu, binadamu na uhai. Na viumbe hivi huingia ndani ya mipaka inayodirikiwa na akili, ikavitambua; na kuvitambua ni kutambua muumba wake naye ni Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo kuamini kuwepo kwa Mwenyezi Mungu ni kupitia akili na ni ndani ya mipaka ya akili, tofauti na kudiriki dhati ya Mwenyezi Mungu, jambo ambalo ni muhali, kwa sababu dhati yake iko nyuma ya ulimwengu, binadamu na uhai, kwa hivyo iko nyuma ya akili. Na akili haiwezi kutambua uhakika wa kilichoko nyuma ya utambuzi wake kwa sababu ya kasoro zake katika kudiriki huku. Kasoro hiyo yenyewe ni wajibu iwe katika mambo yanayoitia nguvu imani na sio sababu ya kutia wasiwasi na shaka. Basi kwa kuwa imani yetu kwa Mwenyezi Mungu hutokana na akili, huwa utambuzi wetu wa kuwepo kwa Mwenyezi Mungu ni utambuzi kamili, na kwa kuwa hisia zetu juu ya kuwepo Mwenyezi Mungu zimefungamana na akili huwa hisia zetu juu ya kuwepo Mwenyezi Mungu ni hisia za yakini. Yote haya hutufanya tuwe na utambuzi uliokamilika na hisia za yakini kwa sifa zote za Uungu. Na kazi ya haya ni kutukinaisha kuwa sisi hatuwezi kudiriki hakika ya dhati ya Mwenyezi Mungu pamoja na uthabiti kamili wa imani yetu kwake. Ni wajibu kwetu sisi kusalimu amri kwa kila anacho tupasha habari kwacho hata kama akili zetu hazidiriki au kufikia kukidiriki. Hayo ni kwa sababu ya kushindwa kwa akili ya kibinadamu kimaumbile kufikia kudiriki kilicho juu yake kwa vipimo vyake vya kulinganisha, (vipimo) vyenye kikomo. Kwa sababu kudiriki huku kunahitaji vipimo visivyo vya kulinganisha au vya kikomo, na uwezo huu haumilikiwi na binadamu na wala hatoweza kuumiliki.

Ama kuthibitisha haja ya kuwepo wajumbe, nako ni kwamba imethibitika kuwa binadamu ni kiumbe cha Mwenyezi Mungu na kuwa hisia ya kidini ni katika maumbile ya binadamu kwa sababu ni ghariza (hisia) miongoni mwa ghariza zake. Basi ni katika maumbile yake kumtukuza muumba wake, na kutukuza huko ni ibada. Nayo ni mahusiano baina ya mwanadamu na muumba wake. Na mahusiano hayo yakiachwa bila nidhamu, humfanya mwanadamu achanganyikiwe na kumuabudu asiyekuwa muumba. Basi hapana budi ila kuyapangia nidhamu sahihi mahusiano haya. Na nidhamu hii haipaswi kutoka kwa mwanadamu kwa sababu hawezi kudiriki uhakika wa muumba ili imstahikie kupanga nidhamu baina yake Mwenyezi Mungu na yeye, basi hakuna budi ila nidhamu hii iwe ni kutoka kwa Muumba. Na kwa sababu hakuna budi ila Muumba amfikishie mwanadamu nidhamu hii, ndipo hakuna budi kuwepo wajumbe watakao wafikishia watu dini ya Mwenyezi Mungu.

Na dalili nyengine juu ya haja ya watu kwa wajumbe, ni kwamba mwanadamu ana haja ya kushibisha *ghariza* (hisia za kimaumbile) na mahitaji yake ya kiviungo. Na kushibishwa huku kukitekelezwa bila nidhamu huleta ushibishwaji wa kimakosa na

kombo, na husababisha dhiki kwa mwanadamu. Basi hapana budi ila kuwepo nidhamu maalumu itakayompangia mwanadamu ghariza zake na mahitaji yake ya kiviungo. Na nidhamu hii haitoki kwa mwanadamu kwa sababu fahamu yake ya upangaji wa ghariza za mwanadamu na haja zake za kiviungo hubeba tofauti, ikhtilafu, mgongano na huathiriwa na mazingira anapoishi. Basi akiachiwa yeye hilo, huwa nidhamu imebeba tofauti, ikhtilafu na mgongano unaosababisha dhiki kwa mwanadamu. Basi hakuna budi ila nidhamu hii itoke kwa Mwenyezi Mungu.

Ama kuthibitisha kuwa Qur'ani yatoka kwa Mwenyezi Mungu, nayo Qur'ani ni kitabu cha kiarabu alichokuja nacho Muhammad (saw). Nacho ima chatoka kwa waarabu au kutoka kwa Muhammad au kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Na wala haimkiniki kutoka kwa asiyekuwa mmoja miongoni mwa hawa watatu kwa sababu ni cha kiarabu kilugha na kimbinu.

Ama kuwa chatoka kwa waarabu, hili ni batili kwa sababu Qur'ani iliwalingania walete mfano wake.

**قُلْ فَأْتُوا بِعَشْرِ سُوَرٍ مِثْلِهِ (هود:13)**

"*Sema: Leteni sura kumi mfano wake*" [TMQ 11:13] na

**قُلْ فَأْتُوا بِسُورَةٍ مِثْلِهِ (يونس: 38)**

"*Sema: Leteni sura moja mfano wake*" [TMQ 10:38]

Walijaribu kuleta mithali yake lakini wakashindwa, kwa hivyo si katika maneno yao kwa kushindwa kwao kuleta mfano wake pamoja na kupewa changamoto na majaribio yao kuleta mfano wake. Na ama kuwa chatoka kwa Muhammad hilo pia ni batili kwa sababu Muhammad ni mwarabu miongoni mwa waarabu na jinsi utakavyo kuwa uhodari wake, yeye ni miongoni mwa wanadamu na ni mmoja wao katika mujtama wake na umma wake. Na maadamu waarabu walishindwa kuleta mfano wake basi huwa sawa kwa Muhammad aliye muarabu kushindwa kuleta mfano wake kwa hivyo hakitokani na yeye. Zaidi ya hili ni kuwa Muhammad (saw) ana hadithi sahihi na nyengine zilizopokelewa na wapokezi wengi (*tawatur*) ambazo ni muhali ila kuzisadikisha. Na inapo fananishwa hadithi na aya yoyote haupatikani mlingano baina yao katika mtindo, na alikuwa akisoma Aya iliyomshukia na akitamka hadithi katika wakati huo huo mmoja na baina yake kulikuwa na tofauti katika mbinu. Maneno ya mtu jinsi atakavyo yatafautisha hushabihiana katika mtindo kwa sababu ni sehemu yake. Na kwa kukosekana kushabihiana baina ya hadithi na Aya basi haiwi Qur'ani kata kata ni maneno ya Muhammad kwa sababu ya tofauti iliyowazi inayodhihirika baina yake na maneno ya Muhammad. Pia waarabu ambao ni wajuzi kushinda watu wengine kwa mitindo ya lugha ya kiarabu, lakini hakuna kati yao aliyedai kuwa Qur'ani ni maneno ya Muhammad au hushabihiana na maneno yake. Walichodai ni kwamba yeye anaileta kutoka kwa kijana wa kinasara aliyeitwa (Jabr), na kwa hili Mwenyezi Mungu aliwarudi kwa kauli yake:

**وَلَقَدْ نَعْلَمُ أَنَّهُمْ يَقُولُونَ إِنَّمَا يُعَلِّمُهُ بَشَرٌ لِسَانُ الَّذِي يُلْحِدُونَ إِلَيْهِ أَعْجَمِيٌّ وَهَذَا لِسَانٌ عَرَبِيٌّ مُبِينٌ (النحل:103)**

"*Na tunajua kwamba wao wanasema: Yuko mtu anayemfundisha. Lugha ya yule wanaye mwelekeza kipotofu ni ya kigeni, na hii ni lugha ya kiarabu yenye ubainifu!*" [TMQ 16:103]

Na kwa sababu ya kuthibitika kuwa Qur'an si maneno ya waarabu wala si maneno ya Muhammad, basi huwa ni maneno ya Mwenyezi Mungu kwa yakini, na ni muujiza kwa yule aliyeileta. Na kwa kuwa Muhammad ndio aliyekuja nayo, nayo ni maneno ya Mwenyezi Mungu na Sheria zake, wala haji na Sheria ya Mwenyezi Mungu isipokuwa Mitume au Wajumbe, basi kwa yakini Muhammad ni Mtume na Mjumbe kwa dalili ya

kiakili. Hii ni dalili ya kiakili juu ya imani kwa Mwenyezi Mungu na ujumbe wa Muhammad na kuwa Qur'ani ni maneno ya Mwenyezi Mungu.

Na kwa haya huwa imani juu ya Mwenyezi Mungu ni yenye kupatikana kwa njia ya kiakili na hapana budi kwamba imani hiyo iwe kwa njia ya ki-akili. Na kwa hivyo huwa ni nguzo inayosimama juu yake imani juu ya mambo yote yasiyoonekana (*ghayb*), na yote anayotueleza nayo Mwenyezi Mungu, kwa kuwa tumekwisha muamini Yeye. Na Yeye amesifika kwa sifa za Uungu twawajibika kuamini yote anayotueleza sawa sawa yawe yanadirikiwa na akili au kuwa juu ya akili zetu, kwa sababu Mwenyezi Mungu ndiye aliyetupasha habari nayo. Na kufika hapa ni wajibu kuamini Siku ya kufufuliwa na kukusanywa, Pepo, Moto, Hisabu, Adhabu, Malaika, Majini, Mashetani na mengineo yaliyokuja nayo Al-Qur'an Al-Kariim au hadithi zilizokatikiwa (*qat'iyy*). Na imani hii ijapokuwa imetokana na njia ya kunukuliwa na kusikilizwa lakini katika msingi wake ni imani ya kiakili kwa sababu msingi umethubutu kiakili. Na kwa hivyo hakuna budi ila kuwa itikadi ya Muislamu kutegemea akili au yale yaliyothubutu msingi wake kwa njia ya kiakili. Basi Muislamu huwajibika kuitakidi yaliyothubutu kwa njia ya akili au kwa njia ya kusikiliza iliyoyakini na kukatikiwa juu yake, yaani yaliyothubutu katika Al-Qur'an Al-Kariim na hadithi za kukatikiwa yaani *mutawatir*. Na kisichothubutu kutoka njia mbili hizi: Akili na maelezo wazi (*nass*) ya Kitabu na Sunna ya kukatikiwa, ni haramu kwake kuitakidi kwa sababu itikadi hazichukuliwi ila kwa yakini.

Kwa hayo ni wajibu kuamini kilicho kabla ya maisha ya duniani naye ni Mwenyezi Mungu, na yaliyoko baada yake nayo ni Siku ya Qiyama. Na kwa kuwa maamrisho ya Mwenyezi Mungu ndio fungamano la kilicho kabla ya maisha na maisha (ya duniani) na ziada ya kuwa fungamano la kuumbwa, na kuhisabiwa kwa vitendo vya mwanadamu katika maisha ni fungamano la yale ya baada ya maisha na maisha (ya duniani) na ziada ya kuwa fungamano la kufufuliwa na kukusanywa. Kwa hakika hapana budi ila kwamba maisha haya kufungamana na yaliyoko kabla na baada yake, na kuwa hali za mwanadamu ndani yake zimefungika na fungamano hilo. Kwa hivyo mwanadamu ni wajibu kupeleka maisha yake kulingana na nidhamu za Mwenyezi Mungu na kuitakidi kuwa Yeye atamhisabu Siku ya Qiyama juu ya vitendo vyake katika maisha ya dunia.

Na kwa haya hupatikana fikra ya ndani iliyokamilika kwa kilichoko nyuma ya ulimwengu, uhai na binadamu na pia hupatikana fikra ya ndani iliyokamilika kwa kilichoko kabla ya maisha na baada yake, na kuwa maisha haya yana mahusiano na kilicho kabla yake na kilicho baada yake. Na kwa haya huwa tatizo kubwa limetatuliwa lote na itikadi ya Kiislamu.

Na mwanadamu anapomaliza katika tatuo hili huweza kuhama kwenda kwenye fikra juu ya uhai wa duniani, na kwenda pia kwenye kupatikana fahamu sahihi zinazozaa natija. Na tatuo hilo lenyewe ni msingi unaosimama juu yake mfumo ambao huchukuliwa kuwa ni njia ya maendeleo, na pia ni msingi unaosimama juu yake hadhara ya mfumo huu. Na ni msingi unaotokana kwayo nidhamu zake, na ni msingi unaosimama juu yake serikali yake. Basi msingi unaosimama juu yake Uislamu—fikra na njia (*twariiqa*)—ni Aqida ya Kiislamu.

**يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا آمِنُوا بِاللهِ وَرَسُولِهِ وَالْكِتَابِ الَّذِي نَزَّلَ عَلَى رَسُولِهِ وَالْكِتَابِ الَّذِي أَنزَلَ مِنْ قَبْلُ وَمَنْ يَكْفُرْ بِاللهِ وَمَلاَئِكَتِهِ وَكُتُبِهِ وَرُسُلِهِ وَالْيَوْمِ الآخِرِ فَقَدْ ضَلَّ ضَلاَلاً بَعِيدًا (النساء: 136)**

"*Enyi mlioamini, mwaminini Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake na kitabu ambacho kimeteremka kwa Mjumbe wake na Kitabu ambacho kimetangulia kuteremshwa. Yeyote anayemkufuru Mwenyezi Mungu na Malaika wake na Vitabu vyake na Wajumbe wake na Siku ya Mwisho basi amepotea upotofu wa mbali!*" [TMQ 4:136]

Ama baada ya kuthibitika haya na kuyaamini kuwa ni jambo la lazima, basi imempasa kila Muislamu kuamini Sheria ya Kiislamu kikamilifu kwa sababu imekuja katika Al-Qur'an Al-Kariim na Mjumbe (saw) amekuja nayo au atakuwa ni kafiri. Kwa hivyo kuikanusha Sheria kwa jumla, au ufafanuzi wake uliokatikiwa, ni ukafiri sawa sawa ziwe ni ahkamu zenye kuambatana na ibada au maingiliano (*mu'amalat*) au nidhamu ya kuadhibu waasi au vyakula. Kukanusha Aya.

**{ وَأَقِيمُوا الصَّلاَةَ } (البقرة: 43)**

"*Simamisheni swala*" [TMQ 2:43] ni kama kukanusha Aya

**{ وَأَحَلَّ اللهُ الْبَيْعَ وَحَرَّمَ الرِّبَا } (البقرة: 275)**

"*Allah amehalalisha biashara na kuharamisha riba*" [TMQ 2:275] ni sawa kama kukanusha Aya

**{ وَالسَّارِقُ وَالسَّارِقَةُ فَاقْطَعُوا أَيْدِيَهُمَا }(المائدة: 38)**

"*Mwizi, mume au mke, wakateni mikono yao*" [TMQ 5:38] na ni kama kukanusha Aya

**{ حُرِّمَتْ عَلَيْكُمْ الْمَيْتَةُ وَالدَّمُ وَلَحْمُ الْخِنزِيرِ وَمَا أُهِلَّ لِغَيْرِ اللهِ بِهِ }**

"*Imeharamishwa kwenu nyamafu na damu na nyama ya ngurue na kilichochinjwa si kwa ajili ya Mwenyezi Mungu*" [TMQ 5:3].

Wala imani juu ya Sheria haitegemei akili bali hapana budi ila kusalimu amri kikamilifu kwa kila alichokileta Mwenyezi Mungu:

**{ فَلاَ وَرَبِّكَ لاَ يُؤْمِنُونَ حَتَّى يُحَكِّمُوكَ فِيمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لاَ يَجِدُوا فِي أَنفُسِهِمْ حَرَجًا مِمَّا قَضَيْتَ وَيُسَلِّمُوا تَسْلِيمًا } (النساء: 65)**

"*La, naapa kwa Mola wako, hawana imani mpaka wahukumu kukupitia wewe kwa kila husuma baina yao, kisha wasione uzito katika nafsi zao kwa yale uliyohukumu bali wasalimu amri kikamilifu!*" [TMQ 4:65].

## 2: AL-QADHAA WA AL-QADAR

Asema Mwenyezi Mungu katika Surat Al-'Imran:

**{ وَمَا كَانَ لِنَفْسٍ أَنْ تَمُوتَ إِلاَّ بِإِذْنِ اللهِ كِتَابًا مُؤَجَّلاً } (آل عمران: 145)**

"*Na haiwezi nafsi kufa ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu kama ilivyo andikwa ajali yake*" [TMQ 3:145].

Na amesema katika Sura Al-'Araf:

**{ وَلِكُلِّ أُمَّةٍ أَجَلٌ فَإِذَا جَاءَ أَجَلُهُمْ لاَ يَسْتَأْخِرُونَ سَاعَةً وَلاَ يَسْتَقْدِمُونَ} (الأعراف: 34)**

"*Na kila Umma una muda (ajal) wao.Unapofika muda wao basi hawataakhirishwa hata saa moja wala hawatatangulizwa*" [TMQ 7:34].

Na amesema katika Surat Al-Hadiid:

**{ مَا أَصَابَ مِنْ مُصِيبَةٍ فِي الأَرْضِ وَلاَ فِي أَنْفُسِكُمْ إِلاَّ فِي كِتَابٍ مِنْ قَبْلِ أَنْ نَبْرَأَهَا إِنَّ ذَلِكَ عَلَى اللهِ يَسِيرٌ } (الحديد:22)**

"*Hautokei msiba katika ardhi wala katika nafsi zenu ila uko katika Kitabu kabla hatujauumba; Hakika hayo ni mepesi kwa Mwenyezi Mungu*" [TMQ 57:22].

Na amesema katika Surat At-Tawbah:

**{ قُلْ لَنْ يُصِيبَنَا إِلاَّ مَا كَتَبَ اللهُ لَنَا هُوَ مَوْلاَنَا وَعَلَى اللهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُونَ } (التوبة: 51)**

"*Sema: Hakitotusibu sisi ila kile alichotuandikia Mwenyezi Mungu. Yeye ni Mola wetu. Na juu ya waumini wamtegemee* Mwenyezi Mungu" [TMQ 9:51].

Na amesema katika Surat Saba:

**{ لاَ يَعْزُبُ عَنْهُ مِثْقَالُ ذَرَّةٍ فِي السَّمَاوَاتِ وَلاَ فِي الأَرْضِ وَلاَ أَصْغَرُ مِنْ ذَلِكَ وَلاَ أَكْبَرُ إِلاَّ فِي كِتَابٍ مُبِينٍ } (سبأ: 3)**

"*Hakuna kilicho fichika kwake katika mbingu wala katika ardhi hata chenye uzito wa chembe tu, wala kidogo kushinda hicho wala kikubwa ila kiko katika kitabu chenye kubainisha*" [TMQ 34:3].

Na amesema katika Surat Al-An'am:

**{ وَهُوَ الَّذِي يَتَوَفَّاكُمْ بِاللَّيْلِ وَيَعْلَمُ مَا جَرَحْتُمْ بِالنَّهَارِ ثُمَّ يَبْعَثُكُمْ فِيهِ لِيُقْضَى أَجَلٌ مُسَمًّى ثُمَّ إِلَيْهِ مَرْجِعُكُمْ ثُمَّ يُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ }(الأنعام: 60)**

"*Naye ndiye anayewafisheni usiku na anajua mlicho fanya mchana. Kisha Yeye huwafufua humo (mchana) ili utekelezwe muda uliotajwa. Kisha kwake Yeye ndiyo marejeo yenu, naye tena atawaambieni mliyo kuwa mkiyafanya*" [TMQ 6:60].

Na amesema katika Surat An-Nisaa:

**{ وَإِنْ تُصِبْهُمْ حسنة يقولوا هذه من عند الله وإن تصبهم سَيِّئَةٌ يَقُولُوا هَذِهِ مِنْ عِنْدِكَ قُلْ كُلٌّ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ فَمَالِ هَؤُلاَءِ الْقَوْمِ لاَ يَكَادُونَ يَفْقَهُونَ حَدِيثًا } (النساء: 78)**

"*Na likiwafikia jambo zuri wanasema: Hili limetoka kwa Mwenyezi Mungu. Na likiwafikia jambo baya wanasema: Hili limetoka kwako wewe. Sema: Yote yanatokana na Mwenyezi Mungu. Basi wana nini watu hawa hata hawakaribii kufahamu maneno?*" [TMQ 4:78]

Aya hizi na aya nyenginezo zinazo fanana nazo hutumiwa na wengi kama ushahidi katika mas-ala ya *al-qadhaa wa al-qadar*, ushahidi ambao unabeba ufahamu ya kuwa mwanadamu hulazimishwa kutenda anayoyatenda, na hivi vitendo anavyovitenda huwa amelazimishwa na matakwa (*irada*) ya Mwenyezi Mungu na mapendeleo yake (*mashiiatih*), na Mwenyezi Mungu ndiye aliyemuumba mwanadamu na akaumba vitendo vyake. Nao wanajaribu kutilia nguvu msemo wao kwa msemo wa Mwenyezi Mungu:

**{ وَاللهُ خَلَقَكُمْ وَمَا تَعْمَلُونَ } (الصافات: 96)**

"*Na Allah amewaumba nyinyi na mnayoyatenda*" [TMQ 37:96]

Kama vile wanavyoshuhudisha kwa hadithi nyengine kama msemo wake (saw): *"**Roho mtakatifu amenitia wahyi kuwa haiwezi kufa nafsi mpaka imalizike rizki yake na ajali yake na qadar yake iliyo qadiriwa juu yake**."*

Mas-ala ya *al-qadhaa wa al-qadar* yamechukuwa dori muhimu katika madhehebu ya Kiislamu. Ahl as-Sunna wakawa na rai inayofupishwa kwamba mwanadamu ana uchumaji (*kasb*) wa khiyari katika kutenda vitendo yake na atahisabiwa juu ya huo uchumaji (*kasb*) wa khiyari. Na ufupi wa rai ya Mu'utazila ni kwamba mwanadamu ndiye anayeviumba vitendo vyake vyote kwa nafsi yake, basi atahisabiwa juu yake kwa sababu yeye ndiye aliyeviumba. Na ufupi wa rai ya Jibriyya ni kwamba Mwenyezi Mungu ndiye aliyemuumba mwanadamu na ameumba vitendo vyake, kwa hivyo huwa mja amelazimishwa kwa vitendo vyake wala hana khiyari, basi huwa kama unyoya angani unaopeperushwa na upepo unakopenda kuvuma.

Mchunguzi makini wa mas-ala ya *al-qadhaa wa al-qadar* hufikia kwamba, umakini wa uchunguzi wake huwajibisha kujuwa msingi unaojengewa juu ya uchunguzi. Na msingi huu si vitendo vya mja kuwa yeye ndiye aliyeviumba au Mwenyezi Mungu. Na sio elimu ya Mwenyezi Mungu kujuwa kwamba mja atatenda kitendo kadha na elimu yake izunguke (kitendo) hichi, na si matakwa (*irada*) ya Mwenyezi Mungu kuwa matakwa yake yameambatana na kitendo cha mja basi hakuna budi ila kutokea kwa sababu ya matakwa haya. Wala sio kuwa vitendo vya mja vimeandikwa katika *Al-lawh al-mahfudh* basi hakuna budi ila avitende kulingana na yaliyoandikwa.

Ndio, havijawa kabisa vitu hivi kuwa msingi wa uchunguzi kwa sababu havina mahusiano yoyote na maudhui hii kwa upande wa thawabu na adhabu. Bali mahusiano yake huwa kwa upande wa uumbaji, elimu iliyozunguka kila kitu, matakwa yanayohusiana na yote yanachowezekana na *Al-lawh al-mahfudh* kuzunguka kila kitu. Na mahusiano haya ni maudhui nyengine tofauti na maudhui ya kutoa thawabu au adhabu kwa vitendo, yaani: Je mwanadamu ni mwenye kulazimishwa kutenda kitendo cha kheri au shari, ama ana khiyari juu yake? Na je ana khiyari kutenda kitendo au kukiwacha au hana khiyari?

Na mchunguzi makini katika vitendo huona kwamba mwanadamu anaishi ndani ya mizunguko miwili, mmoja ana utawala juu yake ambao ni mzunguko unaotokea ndani ya mipaka ya vitendo (*tasrifat*) vyake na ndani ya mpaka huu hupatikana vitendo vyake anavyo vitenda kwa khiyari yake pekee. Na wapili una mtawala yeye na ndio mzunguko ambao yeye yuko ndani ya mipaka yake, na hupatikana ndani ya mzunguko huu vitendo ambavyo hana muingiliano wowote juu yake sawa ikiwa vyamtokea kutoka kwake au juu yake.
Kwa hivyo vitendo ambavyo hutokea katika mzunguko unao mtawala yeye, hana muingiliano wowote juu yake wala hana lolote juu ya matukio yake. Navyo ni vifungu viwili: Kifungu kinacho lazimishwa na nidhamu ya maumbile, na kifungu ambacho hutokea ndani yake vitendo ambavyo haviko ndani ya uweza wake na ambavyo hana nguvu ya kuvipinga lakini havilazimishwi na nidhamu ya maumbile. Ama vinavyolazimishwa na nidhamu za maumbile, yeye husalimu amri kwake na kwa hivyo hupelekwa kwa mujibu wake kilazima kwa sababu hupelekwa pamoja na ulimwengu na uhai kulingana na nidhamu mahsusi isiyobadilika. Kwa hivyo hutokea vitendo ndani ya mzunguko huu bila ya matakwa yake, na yeye ndani yake hupelekwa wala hakhiyarishwi. Amekuja katika dunia hii bila matakwa yake na ataondoka bila matakwa yake, wala hawezi kukirusha kiwiliwili chake kipekee na kupaa angani. Wala hawezi kwa hali ya maumbile yake kutembea juu ya maji wala hawezi kujiumbia nafsi yake rangi ya macho yake wala sura ya kichwa chake wala ukubwa wa mwili wake. Hakika yule aliyeumba yote haya peke yake ni Mwenyezi Mungu pasina mja aliyeumbwa kuwa na athari yoyote wala mahusiano yoyote katika haya. Kwa sababu Mwenyezi Mungu ndiye aliyeumba nidhamu ya maumbile na akaijaalia kuwa ni yenye kupangilia maumbile, na akafanya maumbile ni yenye kuenda kwa mujibu wake wala hayawezi kuenda kinyume chake.

Ama vitendo ambavyo haviko ndani ya uweza wake na ambavyo hana uweza wa kujikinga navyo na wala havilazimishwi na nidhamu ya maumbile, navyo ni vitendo vinavyotokana na mwanadamu au juu yake kinguvu, wala hamiliki kabisa uwezo wa kujikinga navyo. Kama mtu kuanguka kutoka juu ya ukuta na kumwangukia mtu mwengine na kumuuwa, au kama mtu anapofyetua risasi akimlenga ndege ikamsibu mtu asiyemjua na kumuuwa. Au kama ajali ya gari moshi au gari au kuanguka kwa ndege kwa sababu ya hitilafu iliyotokea isiyoweza kuepukika na kwa kuanguka kwake isababishe kufa kwa abiria, na yenye kufanana na haya. Hivi vitendo vinavyotokana na mwanadamu au juu yake hata kama si katika yale yaliyolazimishwa na nidhamu ya maumbile lakini hutokea kutoka kwa mwanadamu au juu yake bila matakwa yake na yeye hana uwezo ndani yake basi huingia katika mzunguko unao mtawala mwanadamu. Vitendo hivi vyote vinavyotokea katika mzunguko ambao humtawala mwanadamu ndivyo vinavyoitwa "*qadhaa*" kwa sababu Mwenyezi Mungu peke yake ndiye aliye yaamulia. Kwa hivyo hatohisabiwa mja kwa vitendo hivi hata kama vitakuwa na manufaa au madhara au mapenzi au uchukivu kwa mujibu wa mwanadamu, yaani vitakavyo kuwa na kheri au shari kwa mujibu wa anavyo vifasiri mwanadamu hata kama Mwenyezi Mungu peke yake ndiye anayejua shari na kheri katika vitendo hivi. Hii ni kwa sababu

mwandamu hana athari yoyote ndani yake wala havijui wala hajui jinsi vinavyotokea, wala hamiliki kabisa uwezo wa kujikinga navyo wala kuvivuta (vitokee). Na ni juu ya mwanadamu kuamini "*al-qadhaa*" hii na kuwa inatoka kwa Mwenyezi Mungu.

Ama *al-qadar* nayo ni kuwa vitendo vinavyo patikana sawa sawa viwe katika mzunguko unao mtawala mwanadamu au mzunguko anao utawala yeye vinatukia katika vitu na juu ya vitu katika vitu (mada) vya ulimwengu, mwanadamu na uhai. Mwenyezi Mungu ameviumba vitu hivi na sifa maalumu, akaumba moto na sifa ya kuchoma na katika kuni sifa ya kuungua na katika kisu sifa ya kukata; na akazifanya sifa za lazima kwa mujibu wa nidhamu ya maumbile isiyobadilika. Na ikidhihirika kwamba imebadilika huwa Mwenyezi Mungu ndiye aliye vipokonya sifa hizo na jambo hilo huwa kinyume na ada. Haya hupatikana kwa Mitume na huwa ni miujiza kwao wao. Kama Mwenyezi Mungu alivyoumba vitu na sifa zake hivyo hivyo ameumba ndani ya mwanadamu ghariza na mahitaji ya kiviungo na akajaalia humo sifa maalumu kama sifa katika vitu. Akaumba katika ghariza ya kuendeleza kizazi matamanio ya kijinsiya na katika mahitaji ya kiviungo akaweka sifa ya njaa, kiu na mifano yake. Akazifanya sifa hizi kuwa ni lazima kwa mujibu wa mwenendo wa maumbile. Sifa hizi maalumu ambazo Mwenyezi Mungu amezitia katika vitu na katika ghariza na katika mahitaji ya kiviungo katika mwanadamu huitwa *al-qadar,* kwa sababu ni Mwenyezi Mungu peke yake aliyeviumba vitu, ghariza na mahitaji ya kiviungo na akavikadiria sifa zake maalum. Nazo hazitoki kwa mwanadamu wala mja hana usemi wowote ndani yake wala hana athari yoyote juu yake. Ni juu ya mwanadamu kuamini kuwa yule aliyevikadiria vitu kuwa na sifa maalum ni Mwenyezi Mungu. Kuna uwezekano katika sifa hizi kwa mwanadamu kutenda vitendo kwa kupitia sifa hizi kwa mujibu wa maamrisho ya Mwenyezi Mungu na huwa kheri, au aende kinyume na maamrisho ya Mwenyezi Mungu na huwa shari, sawa sawa katika utumiaji wa vitu na sifa zake ama kuitikia ghariza na mahitaji ya kiviungo huwa kheri vikiambatana na maamrisho na makatazo ya Mwenyezi Mungu na shari ikiwa ni kinyume na maamrisho na makatazo ya Mwenyezi Mungu.

Na kufikia hapa vitendo vinavyotokea katika mzunguko ambao humtawala mwandamu kutoka kwa Mwenyezi Mungu imma ni kheri au shari, na sifa zinazopatikana katika vitu na ghariza na mahitaji ya kiviungo hutoka kwa Mwenyezi Mungu sawa sawa natija yake ikiwa ni kheri au shari. Na kufikia hapa ni lazima kwa Muislamu kuamini *al-qadha*a, kheri yake na shari yake ni kutoka kwa Mwenyezi Mungu yaani ni aitakidi kuwa vitendo nje ya mzunguko wake ni kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Na pia aamini *al-qadar*, kheri yake na shari yake ni kutoka kwa Mwenyezi Mungu yaani aitakidi kuwa sifa katika vitu zilizomo katika maumbile yao zatoka kwa Mwenyezi Mungu. Sawa sawa ikiwa natija inayopatikana kutoka kwake ni kheri au ni shari, na mwanadamu kiumbe hana athari yoyote juu yake. *Ajal* (kifo) ya mwandamu na riziki yake na nafsi yake vyote ni kutoka kwa Mwenyezi Mungu, kama hisia ya kijinsiya na hisia ya kumiliki zinavyopatikana katika ghariza mbili za kuendeleza kizazi na kuhifadhi maisha, na njaa na kiu zinavyopatikana katika mahitaji ya kiviungo vyote ni kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Haya ni kuhusu vitendo vinavyotokea katika mzunguko unaomtawala mwanadamu na katika sifa za vitu vyote.

Ama mzunguko anao utawala mwanadamu nao ni mzunguko anaokwenda ndani yake kwa khiyari kwa nidhamu anayoichagua sawa sawa ni Sheria ya Mwenyezi Mungu au nyengineyo. Na mzunguko huu ndio unaotokea ndani yake vitendo vinavyotokana na mwanadamu au juu yake kwa mapendeleo yake. Yeye hutembea, hula, hunywa na husafiri wakati wowote apendao na hujizuia na hayo wakati wowote apendao. Huchoma kwa moto na hukata kwa kisu kama apendavyo, naye hushibisha njaa ya kijinsia au njaa ya kumiliki au njaa ya matumbo kama apendavyo; hutenda kwa khiyari na hujizuia

kutenda kwa khiyari. Kwa hivyo ataulizwa juu ya vitendo anavyovitenda ndani ya mzunguko huu.

Hata kama sifa maalum ya vitu na ghariza na mahitaji ya kiviungo ambavyo amevikadiria Mwenyezi Mungu na akavifanya vya lazima ndivyo ambavyo vina athari katika natija ya vitendo, lakini sifa hizo zenyewe hazitendi, bali mwanadamu huvitumia pindi anapofanya kazi navyo. Hisia ya kijinsiya inayopatikana katika ghariza ya kuendeleza kizazi ina uwezekano wa kheri au shari. Njaa inayotokamana na mahitaji ya kiviungo ina uwezekano wa kheri au shari, lakini yule anayetenda kheri au shari ni mwanadamu na sio ghariza au mahitaji ya kiviungo. Hii ni kwa sababu Mwenyezi Mungu amemuumba mwanadamu na akili inayotambua na akaijaalia katika umbile la akili hiyo ni kutambua kupambanua na akamjulisha mwanadamu njia ya kheri au shari:

**{ وَهَدَيْنَاهُ النَّجْدَيْنِ } (البلد: 10)**

"*Na tukamuongoza katika njia mbili*" [TMQ 90:10].

Na akaijaalia kujua uovu na uchaji mungu:

**{ فَأَلْهَمَهَا فُجُورَهَا وَتَقْوَاهَا } (الشمس: 8)**

"*Na akaifahamisha uovu wake na uchaji mungu wake*" [TMQ 91:8].

Na mwanadamu pindi anapoitikia mwito wa ghariza zake na mahitaji yake ya kiviungo kwa mujibu wa maamrisho na makatazo ya Mwenyezi Mungu huwa amekwisha tenda kheri na amefuata njia ya uchajimungu. Na pindi anapoitikia mwito wa ghariza na mahitaji ya kiviungo kinyume na maamrisho na makatazo ya Mwenyezi Mungu huwa amekwisha tenda shari na kufuata njia ya uovu. Na huwa katika yote hayo yanayotokana naye ni kheri au shari na yanayotokea juu yake ni kheri au shari, na akawa yeye anaitikia njaa kwa mujibu wa amri za Mwenyezi Mungu na makatazo yake huwa anafanya kheri na akiziitikia njaa hizo kinyume na amri za Mwenyezi Mungu na makatazo yake huwa anafanya shari. Juu ya msingi huu huhisabiwa juu ya vitendo hivi vinavyotokea katika mzunguko anao utawala yeye na hupewa thawabu au huadhibiwa juu yake kwa sababu yeye amevitenda kwa khiyari bila ya kutenzwa nguvu ya aina yoyote juu yake. Pamoja na kuwa ghariza na mahitaji ya kiviungo ni sifa maalum kutoka kwa Mwenyezi Mungu, na uwezekano wao wa shari na kheri hutoka kwa Mwenyezi Mungu, lakini Mwenyezi Mungu hakuzilazimisha sifa hizi zitekelezwe kwa njia maalum sawa sawa inayomridhisha Mwenyezi Mungu au kumuudhi yaani sawa sawa shari au kheri. Kama ilivyo sifa ya kuchoma haikulazimishwa kuchoma kwa njia ya lazima, sawa sawa kuchoma kwa njia inayomridhisha Mwenyezi Mungu au kumuudhi, yaani kwa kheri au shari. Na zimejaaliwa sifa hizi zinapo tekelezwa na mtendaji kwa njia inayo takikana kufikia (kheri au shari). Na Mwenyezi Mungu pindi alipomuumba mwanadamu na akamuumba na ghariza na mahitaji hayo na akamuumba na akili inayo tambua na akampa khiyari ya kutenda au kutotenda wala hakumlazimisha kutenda au kutotenda. Wala hakuzijaalia sifa za vitu na mahitaji ya kiviungo ni vyenye kumlazimisha kutenda au kutotenda. Kwa hivyo mwanadamu ni mwenye kukhiyarishwa kuja kutenda au kutotenda akitumia akili inayotambua aliyotunukiwa na Mwenyezi Mungu na akaifanya kituo cha kukalifishwa na Sheria. Kwa haya akamjaalia thawabu kwa kitendo cha kheri kwa sababu akili yake imechagua kutenda kwa mujibu wa maamrisho ya Mwenyezi Mungu na kuepukana na makatazo yake, na akajaalia adhabu kwa kitendo cha shari kwa sababu akili yake imechagua kinyume na maamrisho ya Mwenyezi Mungu, na akatenda yale aliyokatazwa nayo katika kuitikia ghariza na mahitaji yake ya kiviungo kinyume na njia aliyoiamrisha Mwenyezi Mungu. Na malipo yake kwa vitendo hivi ni haki na uadilifu kwa sababu yeye ni mwenye kukhiyarishwa katika utendaji na si mwenye kutenzwa nguvu, wala hakuna mahusiano na mas'ala ya *al-qadhaa wa al-qadar* ndani

yake. Bali mas'ala ni kutenda kwa nafsi yake kwa kitendo alichokichagua, na kwa haya ni mwenye kuulizwa kwa aliyoyachuma:

**{ كُلُّ نَفْسٍ بِمَا كَسَبَتْ رَهِينَةٌ } (المدثر: 38)**

"*Kila nafsi iko katika rehani kwa iliyoyachuma*" [TMQ 74:38].

Ama kuhusu elimu ya Mwenyezi Mungu, hakika haimtenzi nguvu mja kutenda kitendo, kwa sababu Mwenyezi Mungu anajua yeye atatenda kitendo kwa khiyari. Wala haiwi kutenda kwake kitendo kumejengewa juu ya elimu, bali elimu hiyo imemtangulia (*azaliyy*) kwamba yeye atatenda kitendo. Na haiwi kuandikwa katika *Al-lawh al-mahfudh* ila ni msemo (*ta'abir*) kwamba elimu ya Mwenyezi Mungu imezunguka kila kitu.

Ama matakwa ya Mwenyezi Mungu hayo pia hayamtenzi nguvu mja juu ya kitendo, bali hutokana na kuwa hakitokei chochote katika ufalme wake ila anachokitaka, yaani hatenzwi nguvu pindi linapotokea jambo lolote ulimwenguni. Anapotenda mja kitendo Mwenyezi Mungu hamzuilii wala hamlazimishi bali humuacha atende kwa khiyari yake, na huwa kitendo chake hicho ni kwa matakwa ya Mwenyezi Mungu wala hatenzwi nguvu juu yake. Na huwa ni kitendo cha mja kwa nafsi yake kwa khiyari yake, basi matakwa (ya Mwenyezi Mungu) hayakumtenza nguvu katika amali yake.

Haya ndio mas'ala ya *al-qadhaa wa al-qadar*, na humfanya mwanadamu kutenda kheri na kuepukana na shari pindi anapojua kuwa Mwenyezi Mungu anamuangalia na atamhisabu na kuwa yeye amemkhiyarisha katika kutenda na kuwacha, na ikiwa yeye hatatumia vizuri khiyari yake katika vitendo itakuwa ole wake na adhabu kali juu yake. Kwa hivyo tutamkuta muumini mkweli anayefahamu uhakika wa *al-qadhaa wa al-qadar*, anayejua uhakika wa tunu aliyoneemeshwa na Mwenyezi Mungu katika akili na khiyari, tutamkuta anamchunga sana Mwenyezi Mungu na kumwogopa Mwenyezi Mungu sana. Atatenda kwa mujibu wa maamrisho ya Kiungu na kujiepusha na makatazo kwa kuhofia adhabu ya Mwenyezi Mungu na kwa tamaa ya Pepo yake na kwa kupenda kuchuma kilicho kikubwa kushinda hayo nacho ni radhi za Mwenyezi Mungu.

### 3. UONGOZI WA KI-FIKRA KATIKA UISLAMU

Huzuka baina ya watu fungamano la kizalendo kila fikra inapozorota. Hilo huwa ni kwa sababu ya kuishi kwao katika nchi moja na kufungika kwao na nchi hiyo. Huathiriwa na ghariza ya kuhifadhi maisha na huwasukuma kuitetea nchi wanamoishi ndani yake na ardhi wanaoishi juu yake, na hapa huja fungamano la kizalendo na ni dhaifu zaidi kinguvu miongoni mwa mafungamano na ni duni zaidi. Hupatikana katika wanyama, ndege kama linavyopatikana katika wanadamu, na daima huchukua dhihirisho la ki-huruma. Hujilazimisha katika hali ya uadui wa kigeni kwa nchi kwa kuivamia au kuitawala juu yake, wala halijitokezi katika hali ya usalama wa nchi kutokana na uadui. Na atakapo fukuzwa (adui) au kutolewa nchini huisha kazi yake, kwa hivyo huwa ni fungamano duni.

Na pindi fikra inapokuwa finyu huzuka baina ya watu fungamano la kikabila, nalo ni fungamano la kifamilia lakini kwa sura pana. Hilo ni kwa kuwa mwanadamu ana ghariza ya kuhifadhi maisha basi hupatikana ndani yake mapenzi ya ubwana. Na hupatikana katika mwanadamu aliyezorota fikra ya kibinafsi, na kila inapozidi fahamu yake hupanuka mapenzi yake ya ukubwa. Basi hutaka ubwana wa famila yake na wa karibu yake kisha hupanuka kwa kupanuka upeo na fahamu na hutaka ubwana juu ya kaumu (kabila) yake katika nchi yake mwanzoni. Kisha unapohakikishwa ubwana juu ya kaumu (kabila) yake katika nchi yake hutaka ubwana wao juu ya wengine. Kwa hivyo huzuka kwa upande huu husuma za ndani baina ya watu wa jamii juu ya ubwana, kisha unapo makinika ubwana katika jamii kwa mmoja wao kwa ushindi wake juu ya wengine

huhama husuma kuwa baina ya jamii hiyo na jamii nyengine juu ya ubwana. Mpaka unapomakinika ubwana juu ya kabila kwa jamii au kwa kikundi cha watu kutoka jamii tafauti, kisha huzuka husuma baina ya kabila hili na makabila mengine juu ya ubwana na kupanda cheo katika kila nyanja ya maisha. Kwa hivyo hutekwa na ukabila (*asabiyya*) watu wenye fungamano hili, na hutekwa na matamanio (*hawaa*) na kusaidiana wao kwa wao. Kwa hivyo huwa fungamano si la kibinadamu na litabaki kuwa ni sababu ya husuma za ndani ikiwa halitokuzwa na husuma za nje.

Kwa hivyo fungamano la kizalendo ni fungamano potofu kwa sababu tatu:

Kwanza—kwa sababu ni fungamano duni lisilofaa kuwa fungamano baina ya mwanadamu mmoja kwa mwengine pindi wanaposhika njia ya mwamko. Pili—kwa sababu ni fungamano la kihuruma linalotokana na ghariza ya kuhifadhi maisha, na fungamano la kihuruma lina uwezekano wa kubadilika kwa hivyo halifai kufanywa ni fungamano la kudumu baina ya wanadamu. Tatu—kwa sababu ni fungamano la muda mfupi hupatikana katika hali ya kujitetea ama katika hali ya utulivu—nayo ni hali asili ya mwanadamu—halipatikani kwa hivyo halifai kuwa ni fungamano baina ya wanadamu.

Na hivyo hivyo fungamano la kikabila ni fungamano potofu kwa sababu tatu: **Kwanza—** kwa sababu ni fungamano la kikabila wala halifai kumfunga mwanadamu mmoja kwa mwengine pindi wanaposhika njia ya mwamko. **Pili—**kwa sababu ni fungamano la kihisia linalotokana na ghariza ya kuhifadhi maisha inayoleta mapenzi ya ubwana. **Tatu—**kwa sababu ni fungamano lisilokuwa la kibinadamu kwani husababisha husuma baina ya watu juu ya ubwana. Kwa hivyo halifai kuwa ni fungamano baina ya wanadamu.

Na miongoni mwa mafungamano fisidifu yanayoyadhaniwa  ni sahihi na baadhi ya watu ni fungamano la kimaslahi na fungamano la kiroho lisilokuwa na nidhamu yoyote inayotokana nalo. Ama fungamano la ki-maslahi nalo ni fungamano la muda mfupi lisilofaa kuwafunga watu, kwa sababu hutokea mashindano ya kupata maslahi makuu, basi hupotea katika hali ya kupimwa maslahi makubwa zaidi. Na kwamba humalizika pindi maslahi yanapotofautika, na hugawanya watu, na kwa sababu humalizika pindi maslahi haya yanapotimia (yanapopatikana). Kwa hivyo ni fungamano la hatari kwa watu wake.

Ama fungamano la kiroho bila nidhamu inayotokana nalo, hilo hudhirika katika hali ya kidini wala halidhihiriki katika mambo ya kimaisha. Kwa hivyo ni fungamano la kivipande lisilokuwa la kivitendo na wala halifai kuwa ni fungamano baina ya watu juu katika mambo yao maishani. Na hapa hudhirika kuwa aqida ya Kikristo haikufaa kuwa ni fungamano baina ya watu wa bara la Ulaya pamoja na kuwa wote ni wakristo kwa sababu ni fungamano la kiroho bila ya nidhamu yoyote.

Kwa hivyo mafungamano yote yaliyotangulia hayafai kumfunga mwandamu mmoja na mwengine maishani wanaposhika njia ya maendeleo. Na fungamano sahihi la kuwafunga wanadamu maishani ni fungamano la kiaqida ya kiakili inayotokana nayo nidhamu, nalo ni fungamano la kimfumo.

Mfumo ni aqida ya kiakili inayozaa nidhamu. Ama aqida, hii ni fikra jumla (*fikra kuliyya*) juu ya ulimwengu, binadamu na uhai, na lile la kabla ya maisha ya duniani na la baada yake, na mahusiano yake na lile la kabla yake maisha ya duniani na baada yake maisha ya duniani. Ama nidhamu inayotokana na aqida hii, hayo ni masuluhisho ya matatizo ya mwanadamu, na ufafanuzi wa vipi kutekeleza masuluhisho haya, kuhifadhi aqida na

kubeba mfumo. Na kuwa ufafanuzi wa namna ya kutekeleza masuluhisho na kuhifadhi na kubeba da'wah ni njia (*twariqa*), na yasiyokuwa hayo nayo ni aqida na suluhisho, haya ni fikra. Na hapo mfumo huwa ni fikra na twariqa.

Mfumo hauna budi ila kuanza katika akili ya mtu ima kwa *wahyi* kutoka kwa Mwenyezi Mungu na kuamrisha aufikishe, au ni uhodari unaotokana na mtu. Ama mfumo unaoanza katika akili ya mtu kupitia wahyi wa Mwenyezi Mungu kwake huo ndio mfumo sahihi kwa sababu ni kutoka kwa muumba wa ulimwengu, binadamu na uhai naye ni Mwenyezi Mungu; basi ni mfumo usio na shaka. Ama mfumo unaoanza na akili ya mtu unaotokana na uhodari wake, huu ni mfumo batili kwa sababu umeanza na akili ilio na kikomo inayoshindwa kuzingira na kujua maumbile, na kwa kuwa fahamu ya mwanadamu katika kupanga nidhamu huathiriwa na tofauti, ikhtilafu, kugongana na kuathiriwa na mazingira anayoishi ndani yake yanayo sababisha nidhamu ya kugongana inayomfikisha mwanadamu katika dhiki. Kwa hivyo mfumo unaoanzwa katika akili ya mtu ni batili katika aqida yake na nidhamu yake inayotokana nayo.

Na juu ya haya huwa msingi wa mfumo ni fikra jumla (*fikra kuliyya*) juu ya ulimwengu, mwanadamu na uhai, na huwa twarika ambayo inayojaalia mfumo uhai na utendaji katika nyanja za maisha ni jambo la lazima kwa fikra hiyo ili upatikane mfumo. Ama kuwa fikra jumla ni msingi hilo ni kwa sababu ndiyo aqida na ni fikra kitegemeo (*qa'ida fikriyya*), na pia ni fikra kiongozi (*qiyada fikriyya*). Juu ya msingi wake huelekea mwanadamu mwenye fikra na mtazamo wake maishani, na juu yake hujengwa fikra zote na hutokana kwake kila suluhisho la matatizo yote maishani. Ama kuwa twarika ni jambo la lazima, hili ni kuwa nidhamu inayotokana na aqida isipohusisha ufafanuzi wa jinsi ya utekelezaji wa suluhisho, na ufafanuzi wa jinsi ya kuhifadhi aqida, na ufafanuzi wa jinsi ya kulingania da'wah, huwa fikra ya kifalsafa na ndoto na nadharia inayobaki kusajiliwa katika vitabu bila kuwa na athari yoyote katika maisha ya dunia. Kwa hivyo hapana budi kuwepo aqida, na hapana budi kuwepo suluhisho la matatizo, na hapana budi kuwepo twarika ili uwe mfumo. Mujarad wa kuwepo fikra na twarika katika aqida inayotokana kwake nidhamu haimaanishi kuwa mfumo huo ni sahihi, bali humaanisha tu kuwa ni mfumo, wala haimaanishi jambo lolote jengine. Jambo ambalo hujulisha usahihi au ubatili wa mfumo ni aqida ya mfumo kwa jinsi ya kuwa ni sahihi au batili. Hii ni kwa sababu aqida hiyo ni fikra kitegemeo ambayo juu yake hujengwa fikra zote, na ambayo huuelekeza kila mtazamo, na hutokana kwake kila suluhisho na kila twarika. Ikiwa hiyo fikra kitegemeo ni sahihi, basi mfumo huwa ni sahihi na ikiwa ni batili huwa mfumo ni batili kutokea msingi wake.

Fikra kitegemeo itakapo afikiana na maumbile ya mwandamu na kujengwa juu ya akili basi huwa kitegemeo (aqida) sahihi, na pindi inapo khitalifiana na maumbile ya mwanadamu au kutojengwa juu ya akili basi huwa fikra kitegemeo batili. Maana ya kuafikiana fikra kitegemeo na maumbile ya mwanadamu ni kukiri kwake kuwa maumbile ya mwanadamu ni ya udhaifu na kumhitajia muumba anayeendesha ulimwengu, au kwa maana nyengine ni kuafiki ghariza ya kuabudu. Na maana ya kuwa imejengeka juu ya akili ni kutojengwa juu ya mada au suluhisho la kati na kati.

Tunapouangalia ulimwengu wote leo hatupati ndani yake ila mifumo mitatu: nayo ni ubepari (urasilmali), ujamaa unaotokana kwake ukomunisti na mfumo wa tatu ni Uislamu. Mifumo miwili ya mwanzo hubebwa kila mmoja na serikali moja au serikali nyingi. Na mfumo wa tatu haubebwi na serikali bali hubebwa tu na watu binafsi katika umma, lakini hupatikana kiulimwengu katika dunia.

Ama ubepari umesimama juu ya msingi wa kutenganisha dini na maisha. Fikra hiyo ndio aqida yake na ni fikra kiongozi (*qiyada fikriyya*) yake na fikra kitegemeo (*qa'ida fikriyya*) yake. Na juu ya fikra kitegemeo hiyo huwa mwanadamu ndiye anayejiwekea nidhamu maishani. Na huwa hapana budi kumhifadhia mwanadamu uhuru wake, nao ni uhuru wa kuitakidi, uhuru wa rai, uhuru wa kumiliki na uhuru wa kibinafsi. Na natija ya uhuru wa kumiliki ni nidhamu ya kiuchumi ya kibepari. Urasilimali ndio uliojitokeza mbele katika mfumo huu na ndio uliojitokeza mbele kutoka kwenye itikadi ya mfumo huu. Kwa hivyo mfumo huu umeitwa mfumo wa urasilmali (ubepari) katika mlango wa kuita kitu kwa jina la lile linalojitokeza mbele zaidi kwake.

Ama demokrasia iliyochukuliwa kutoka mfumo huu, hutoka katika upande wa kuwa mwanadamu ndiye anayejiwekea nidhamu. Kwa hivyo umma huwa ni chimbuko la utawala, ndio unaoweka nidhamu, na ndio unaomuajiri mtawala kuwatawala, na humpokonya utawala wakati wowote wautakao. Na humuwekea nidhamu yoyote waitakayo kwa sababu utawala ni mkataba wa ajira baina ya watu na mtawala kwa kuwatawala kwa nidhamu aliyowekewa na watu awatawale kwayo.

Hata kama demokrasia imetokana na mfumo huo lakini si muhimu kuliko nidhamu yake ya kiuchumi  kwa dalili ya kuwa nidhamu ya ubepari katika magharibi ndio inayomuathiri mtawala na humfanya ni mnyenyekevu kwa matajiri wenye rasilimali mpaka huwa warasilmali hawa ndio watawala wa kiuhakika katika biladi ambayo imeamini mfumo wa ubepari. Na juu ya yote hayo, demokrasia sio makhsusi kwa mfumo huu kwani wakomunisti pia huidai demokrasia na husema kuwa wanaupa umma utawala. Basi ni sawa zaidi mfumo huu kuitwa kuwa ni mfumo wa ubepari.

Chanzo cha kuzuka mfumo huu ni kuwa makaisari na wafalme wa Ulaya na Urusi walichukuwa dini kama mbinu ya kuwatumia watu, kuwadhulumu na kunyonya damu zao na mapato yao na wakawafanya watu wa dini kuwa ni chombo kwa hayo. Pakazuka mpambano mkali baina ya wanafalsafa na wajuzi (*mufakkiruun*) waliosimama miongoni mwao waliokanusha dini kabisa na miongoni mwao walioitambua dini lakini wakatangaza kwamba itenganishwe na maisha. Mpaka ikamakinika rai kwa wengi wa wanafalsafa na wajuzi juu ya fikra moja, nayo ni kutenganisha dini na maisha, na natija yake ya kutarajiwa ni kutenganisha dini na serikali. Na ikamakinika rai ya kutochambua dini katika upande wa kuikanusha au kuikiri, uchambuzi ukafungwa juu ya uwajibu wa kutenganisha dini na maisha. Na huchukuliwa fikra hiyo kuwa ni suluhisho la kati na kati baina ya watu wa dini ambao wanataka kila kitu kiwanyenyekee kwa jina la dini, na baina ya wanafalsafa na wajuzi ambao wanaikanushi dini na utawala wa watu wa dini. Basi (fikra hiyo) haikuikanusha dini na wala haikuipa nafasi kuingia katika maisha, bali iliitenganisha dini na maisha na ikawa aqida wanayoiamini wamagharibi wote ni kutenganisha dini na maisha. Na ikawa aqida hiyo ndiyo fikra kitegemeo ambayo juu yake zimejengwa fikra zote. Na huelekeza kwa msingi wake mwelekeo wa kifikra wa mwanadamu na mtazamo wake maishani. Na juu ya msingi wake hutatuliwa matatizo yote maishani, na ndio fikra kiongozi inayobebwa na wamagharibi na wanayoilingania kwayo ulimwenguni kote.

Aqida ya kutenganisha dini na maisha ni kukiri kwa undani ya kuwa kuna kitu kinachoitwa dini, yaani yupo muumba aliyeumba ulimwengu, mwanadamu na uhai na kuna siku ya kufufuliwa, kwa sababu hii ndio asili ya dini kwa jinsi ilivyo dini. Na kukiri huko ni kupeana fikra juu ya ulimwengu, mwanadamu na uhai na kilichoko kabla ya maisha na baada yake, kwa sababu haikukanusha kuwepo kwa dini, bali pindi ilipoweka fikra ya kuitenga ilikiri kiundani kuwepo kwake. Na huwa imethibitisha kuwepo kwa dini na ikaweka fikra ya kuwa maisha haya hayana mahusiano na yaliyoko kabla na baada

yake pindi iliposema kutengwa dini na maisha, na kuwa dini ni fungamano baina ya mtu na muumba wake tu. Na kwa haya huwa aqida ya “kutenganisha dini na maisha” kwa maana yake kamilifu ni fikra jumla juu ya ulimwengu, mwanadamu na uhai. Kutoka hapa huwa mfumo wa ubepari kwa sura yake tuliyoibainisha ni mfumo kama mifumo mengine.

Ama ujamaa na kutokana nao ukomunisti huuona ulimwengu, mwanadamu na uhai kuwa ni mada tu, na kuwa mada ni asili ya kila kitu na kwa kubadilika kwake ndio huwa vitu. Wala hakuna nyuma ya mada hiyo kitu chochote kata kata, na mada ni ya milele (azaliyyah) na ya tangu (*qadiim*) wala hakuna aliyeileta, yaani mada ndiyo iliyoanzisha maisha. Kwa hivyo wanakanusha fikra ya kuwa vitu ni viumbe vilivyoumbwa na muumba, yaani hukanusha upande wa kiroho katika vitu na wanachukulia kukiri kuwepo kwake ni hatari kwa maisha. Kwa hivyo wanachukulia dini ni kilevya (*afyuun*) kinachowalevya watu na kuwazuia kufanya kazi. Hapana kitu chochote kwao ila mada, hata fikra ni taathira ya mada juu ya ubongo, basi mada ndio asili ya fikra na asili ya kila kitu na kwa kubadilika kwake kimada ndio hupatikana vitu. Kwa ufahamu huu wanakanusha kuwepo muumba na huchukulia kuwa mada ni ya milele na pia hukanusha kilichoko kabla ya uhai na baada yake wala hawatambui ila uhai tu.

Pamoja na tofauti baina ya mifumo hii miwili katika mtazamo wa kimsingi kwa mwanadamu, ulimwengu na uhai, wao huwafikiana ya kuwa mifano mikuu kwa mwanadamu ni katika viwango vikuu anavyovipanga mwanadamu mwenyewe, na furaha na mafanikio (*sa’ada*) ni kuchukua fungu kubwa zaidi la starehe za kiwiliwili kwa sababu kwa mtazamo wao ndio njia ya kufikia mafanikio bali yenyewe ndio mafanikio. Wamekubaliana pia kumpa mwanadamu uhuru wa kibinafsi kwa kujipeleka apendavyo na kwa upande anaotaka maadamu huona yapo mafanikio katika kujipeleka hivi. Kwa hayo huwa miondoko ya kibinafsi au uhuru wa kibinafsi ni miongoni mwa yale yanayotukuzwa na mifumo hii miwili.

Na mifumo miwili hii hutofautiana katika mtazamo juu ya mtu binafsi na mujtamaa. Ubepari ni mfumo wa kibinafsi na huona kwamba mujtamaa ni mkusanyiko wa watu binafsi wala hauutizami mujtamaa ila kwa mtazamo wa kudharau. Huhusisha mtazamo wake kwa mtu binafsi, na kwa hayo ni wajibu kuhifadhiwa uhuru wa mtu binafsi. Kwa hayo huwa uhuru wa itikadi ni katika baadhi ya unayotukuza na pia uhuru wa kiuchumi hutukuzwa. Wala haufungwi (uhuru huu) kwa mujibu wa falsafa yake bali hufungwa tu kupitia serikali ili kuhifadhi uhuru, na serikali hutekeleza kufungwa huku kwa nguvu ya jeshi na ukali wa kanuni. Lakini serikali ni njia wala si lengo, basi ubwana wa mwisho ni kwa watu binafsi wala si kwa serikali. Kwa hivyo mfumo wa kibepari hufanya fikra yake kiongozi kuwa kutenganisha dini na maisha, na kwa mujibu wake huhukumu kwa nidhamu zake na huzilingania na hujaribu kuzitekeleza kila mahali.

Ama ujamaa na kutokana nao ukomunisti, huu ni mfumo unao ona kwamba mujtamaa ni mjumuiko jumla unaokusanya wanadamu na mahusiano yao na mazingira, na haya mahusiano yamefungwa na ni ya kilazima nayo hunyenyekea unyenyekevu wa kilazima na kama mashine. Huu mjumuiko wote ni kitu kimoja; mazingira, binadamu na mahusiano yote ni kitu kimoja wala si viungo vinavyogawanyika. Huona kwamba mazingira ni sehemu ya shakhsiya ya mwanadamu nayo ni sehemu inayobebwa na dhati yake. Kwa hivyo habadaliki mwanadamu kitabia ila kwa kufungika na upande huu wa shakhsiyya yake nayo ni mazingira, na fungamano lake na mazingira ni kama fungamano la kitu na nafsi yake. Kwa hivyo huchukulia mujtamaa ni mkusanyiko mmoja, hubadilika wote kwa pamoja pindi linapobadilika moja wapo, na huzunguka mtu binafsi kwa kufuata mkusanyiko kama linavyozunguka jino katika gurudumu. Kwa hivyo kwao wao hana mtu binafsi uhuru wa itikadi wala uhuru wa kiuchumi. Itikadi imefungwa kwa

yale yaitakayo serikali na uchumi umefungika kwa yale yaitakayo serikali; kwa haya huwa serikali ni miongoni mwa yale yanayotukuzwa na mfumo. Na kutokana na falsafa hii ya mada imebuniwa nidhamu ya kimaisha. Na ikaifanya nidhamu ya kiuchumi ndio msingi wa kwanza na ndio dhihirisho la kijumla la nidhamu zote. Kwa hivyo mfumo wa ujamaa, na ukomunisti unaotokana nao umebeba fikra kiongozi, nayo ni mada na mabadaliko ya kimada. Na juu ya msingi huu huhukumu (hutawala) kwa nidhamu zake, na huulingania na hujaribu kuutekeleza kila mahali.

Ama Uislamu umebainisha kuwa nyuma ya ulimwengu, uhai na mwanadamu kuna muumba aliyeviumba naye ni Mwenyezi Mungu. Kwa hivyyo umekuwa msingi wake ni aqida ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu na imekuwa aqida hiyo ndio inayohusisha upande wa kiroho. Nayo ni kuwa mwanadamu, uhai na ulimwengu wameumbwa na muumba. Na kwa hapa huwa fungamano la ulimwengu kwa sifa yake kama kiumbe, na Mwenyezi Mungu muumba, ndio upande wa kiroho katika ulimwengu. Na fungamano la uhai uliyoumbwa na Mwenyezi Mungu muumba ni upande wa kiroho katika uhai. Na fungamano la mwanadamu kiumbe, na Mwenyezi Mungu muumba, ni upande wa kiroho katika mwanadamu. Na kufikia hapa huwa roho ni kutambua (*idraak*) kwa mwanadamu fungamano lake na Mwenyezi Mungu.

Imani juu ya Mwenyezi Mungu yawajibishwa kuunganishwa na imani kwa Utume wa Muhammad na ujumbe wake na kuwa Qur'ani ni maneno ya Mwenyezi Mungu na hupasa kuamini yote aliyokuja nayo. Na kwa haya aqida ya Kiislamu ina msimamo wa kuwa yupo kabla ya uhai anayelazimika kuaminiwa naye ni Mwenyezi Mungu na imelazimisha kuamini yaliyo baada ya uhai nayo ni Siku ya Qiyama. Na kuwa mwanadamu katika maisha ya dunia amefungwa na maamrisho na makatazo ya Mwenyezi Mungu, na hili ndilo fungamano la maisha na yaliyo kabla yake. Na amefungwa kwa kuhisabiwa juu ya kufuata kwake maamrisho na kuepukana na makatazo hayo, na hili ndio fungamano la maisha na yale ya baada yake. Kwa hivyo ni lazima kwa Muislamu kutambua fungamano lake na Mwenyezi Mungu pindi anapotenda kitendo. Hupeleka vitendo vyake kwa mujibu wa maamrisho ya Mwenyezi Mungu na makatazo yake na hiyo ndio maana ya kuunganisha mada na roho. Na lengo la kupeleka mambo kwa mujibu wa maamrisho ya Mwenyezi Mungu na makatazo yake ni radhi za Mwenyezi Mungu. Na shabaha inayokusudiwa katika kutenda matendo hayo ni thamani itakayopatikana kwa matendo hayo.

Kwa hivyo hayakuwa malengo makuu ya kulinda mujtamaa ni yenye kupangwa na mwanadamu bali ni maamrisho ya Mwenyezi Mungu na makatazo yake. Nayo ni thabiti yasiyobadilika wala kugeuka. Kuhifadhi jinsi ya mwanadamu, akili, heshima ya mwanadamu, nafsi ya mwanadamu, mali ya mtu binafsi, dini, usalama na serikali ni malengo makuu thabiti ya kulinda mujtamaa. Hayafikiwi na mabadiliko wala mageuzi, na zikawekwa adhabu kali ili kuyahifadhi. Zikawekwa hududi na adhabu ili kuhifadhi malengo haya thabiti. Kwa hivyo huchukuliwa kuhifadhi malengo hayo ni jambo la lazima kwa sababu ni maamrisho na makatazo kutoka kwa Mwenyezi Mungu na si kwa sababu ya kuhakikisha thamani ya ki-mada. Hivi ndivyo anavyo simama Muislamu na kusimama serikali kwa vitendo vyake vyote kwa mujibu wa maamrisho ya Mwenyezi Mungu na makatazo yake, kwa sababu hayo ndio yanayo mpangia mwanadamu mambo yake yote. Kutenda vitendo kwa mujibu wa maamrisho ya Mwenyezi Mungu na makatazo yake ndiyo yanayoleta utulivu kwa Muislamu. Na hapa huwa kupata furaha na mafanikio (*sa'ada*) si kushibisha kiwiliwili na kukipa starehe yake bali ni (furaha na mafaniko) katika kumridhisha Mwenyezi Mungu.

Ama mahitaji ya kiviungo na ghariza vimekwisha pangwa na Uislamu kwa nidhamu inayo dhamini kushibisha njaa zote, iwe njaa ya tumbo au njaa ya kijinsia au njaa ya kiroho au yasiyokuwa hayo. Lakini sio kushibisha baadhi kwa hisabu ya vyengine na wala si kwa kunyima baadhi na kuachia mikono vyengine, wala si kuwacha yote huru, bali kuyahusisha yote kwa pamoja na kuyashibisha yote kwa nidhamu ya kina fafanuzi inayomfikisha mwanadamu katika furaha na utulivu. Na humzuia mwanadamu kushuka hadhi ya kufikia daraja ya kinyama kwa sababu ya ukosefu wa utaratibu wa kighariza.

Na kudhamini mpango huu, Uislamu una uangalia mujtamaa kwa kipimo cha kijumla bila kuugawanya, na unamuangalia mtu binafsi kwa sifa yake ya sehemu ya jamii bila kumtenganisha nayo. Lakini hali ya kuwa yeye ni sehemu ya jamii haimaanishi usehemu wake ni kama jino katika gurudumu, bali humaanisha ni sehemu ya jamii kama ulivyo mkono ni sehemu ya kiwiliwili. Kwa hivyo Uislamu humuangalia mtu binafsi kwa sifa yake kama sehemu katika jamii, sio mpweke aliyetenganishwa nayo kwa namna ambayo unapeleka uangalizi huo katika kuhifadhi jamii. Na ikaiangalia wakati huo huo jamii si kwa sifa yake ya kijumla bila vipande bali kwa sifa yake ya mjumuiko inayojumuisha vipande, nao ni watu binafsi, kwa njia inayopelekea uangalizi huo kuhifadhi watu binafsi kama vipande vyake. Mtume (saw) asema*:* "***Mfano wa yule anayechunga mipaka ya Mwenyezi Mungu na yule anayetumbukia ndani yake ni kama watu waliopanda jahazi wakawa baadhi yao juu yake na baadhi yao chini yake. Wakawa wale walio chini yake wakiwa na kiu ya maji hupita kwa walio juu yao. Wakasema: Lau kama sisi tutatoboa tundu katika sehemu yetu tusiwaudhi wale walio juu yetu. Wakiwaacha (kutenda) wanayotaka wataangamia wote pamoja na wakiwazuia wataokoka na kuokoka wote pamoja****.*"

Na mtazamo huu kwa jamii na mtu binafsi ndio unaofanya mujtamaa uwe na ufahamu maalum kwa sababu watu hawa binafsi ndio sehemu ya jamii hivyo hawana budi kuwa na fikra itakayo waunganisha watakayoishi kwa mujibu wake, na kuwa na hisia moja inayo waathiri na itakayo wasukuma kwa mujibu wake. Na kuwa na nidhamu moja itakayo tatua matatizo yao yote maishani. Na kufikia hapa huwa mujtamaa umeundwa na watu, fikra, hisia na nidhamu. Na huwa mwanadamu amefungwa maishani na fikra hizo, hisia na nidhamu. Kwa hiyvo huwa Muislamu maishani amefungwa katika kila kitu na Uislamu na hana uhuru wowote. Na aqida kwa Muislamu imefungwa kwa mipaka ya Kiislamu na wala haikuwachwa wazi. Kwa hivyo huhisabiwa kuritadi kwake kuwa ni kosa kubwa linalostahiki kwa aliyeritadi kuuliwa ikiwa hatorudia imani yake. Na upande wa kibinafsi amefungika kwa nidhamu ya Kiislamu, kwa hivyo huwa zinaa ni kosa analoadhibiwa kwa kosa hilo bila huruma pamoja na kutekelezwa hadharani.

**{ وَلْيَشْهَدْ عَذَابَهُمَا طَائِفَةٌ مِنْ الْمُؤْمِنِينَ } (النور: 2)**

"*Na lishuhudie adhabu yao kundi la Waislamu*" [TMQ 24:2].

Na huwa kunywa tembo ni kosa la kuadhibiwa kwa kosa hilo. Na kuwadhuru wengine ni kosa linalo khitalifiana kwa kutofautiana madhara, kama kumsingizia mtu amezini, au kuuwa au yanayo fanana nayo. Na upande wa kiuchumi umefungwa na Sheria na kwa sababu zilizofanywa kuwa ni mubah kwa mtu binafsi kuzitumia ili kumiliki. Na kwa uhakika wa umilikaji wa mtu binafsi ni kuwa mteremshaji Sheria (Mwenyezi Mungu) ametoa idhini kunufaika nayo. Na kwa kukiuka vifungo (mambo) hivi huwa ni makosa yanayo khitalifiana kwa kutafautiana aina ya ukiukaji unaotokana kama wizi au kupora au yanayofanana nayo. Na kwa haya hakuna budi kuwa na serikali ambayo itahifadhi jamii hiyo na mtu binafsi huyu, na kutekeleza nidhamu juu ya mujtamaa. Na huwa hapana budi kwa mfumo kuathiri wafuasi ili hifadhi hiyo iwe ya kimaumbile inayotoka kwa watu wenyewe. Kwa hivyo mfumo ndio unaofunga na kuhifadhi na serikali ndio inayotekeleza. Na kwa haya ubwana huwa kwa Sheria na sio kwa serikali au kwa

Umma, hata kama utawala huwa ni wa Umma na dhihirisho lake ni katika serikali. Na kufikia hapa huwa twarika ya kutekeleza nidhamu ni serikali, hata kama tegemeo ni juu ya uchajimungu wa mtu binafsi muumini kusimamisha hukumu za Kiislamu. Basi hakuna budi ila kuwepo Sheria itakayo tekelezwa na serikali, na muelekeo kwa mtu binafsi muumini atekeleze Uislamu kwa msukumo wa uchaji mungu. Na kufikia hapa huwa Uislamu ni aqida na nidhamu, na huwa mfumo wa Kiislamu ni fikra na twarika kutokana na jinsi ya fikra hii. Na nidhamu hutokana na aqida yake, na imekuwa hadhara yake ina muundo wa kipekee maishani. Na imekuwa twarika yake katika kubeba da'wah hutekelezwa na serikali na hubebwa fikra kiongozi kwa ulimwengu, na ndio msingi wa kufahamu nidhamu ya Uislamu na kuifanyia kazi. Na utendaji wake huwa katika jamii ambayo huhukumiwa na nidhamu ya Kiislamu katika kueneza ulinganizi wa Uislamu, kwa sababu utekelezaji wa nidhamu ya Kiislamu juu ya wasiokuwa Waislamu miongoni mwa watu huchukuliwa ni njia ya kivitendo ya da'wah. Na bila shaka umekuwa na athari kubwa zaidi utabikishaji huu kuunda ulimwengu huu mpana wa Kiislamu.

Kwa ufupi mifumo inayopatikana katika ulimwengu ni mitatu nayo ni ubepari (urasilmali), ujamaa na kutokana nao ukomunisti, na mfumo wa tatu ni Uislamu. Na kila mmoja wapo katika mifumo hii ina aqida inayotokana kwayo nidhamu zake, na ina kipimo cha vitendo vya mwanadamu maishani, na mtazamo maalum kwa mujtamaa na njia ya kutekeleza nidhamu.

Ama kwa upande wa aqida, mfumo wa kikomunisti huona kuwa mada ni asili ya vitu na kuwa vitu vyote hutokana na mabadiliko ya mada. Na mfumo wa ubepari huona kuwa ni lazima kutenganisha dini na maisha, na natija yake ni kutengwa dini na serikali. Wabepari hawataki kuchambua je kuna muumba au la, lakini uchambuzi wao ni juu ya kuwa muumba hana mahusiano na maisha, sawa akikukubaliwa kuwepo kwake au akikanushwa. Kwa hivyo hufanana kwao anayekiri kuwepo muumba na anaye mkanusha katika aqida yao, nayo ni kutenganisha dini na maisha.

Ama Uislamu huona kuwa Mwenyezi Mungu ndiye muumba aliyeumba maumbile yote na kuwa yeye ndiye aliyetuma Mitume na wajumbe na dini yake kwa binadamu, na kuwa yeye ndiye atakayemhisabu mwanadamu kwa vitendo vyake siku ya qiyama. Kwa hivyo aqida yake ni imani juu ya Mwenyezi Mungu, Malaika wake, Vitabu vyake, Mitume wake, Siku ya Mwisho na *al-qadhaa* na *al-qadar* kheri yake na shari yake kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Ama kwa upande wa jinsi nidhamu inavyotokana na aqida, mfumo wa ukomunisti huona kuwa nidhamu huchukuliwa kutokana na chombo cha uzalishaji kwa sababu mujtama wa kishamba (feudalism) kwa mfano, shoka kwake ni chombo cha uzalishaji, na kutokana na chombo hichi hupatikana nidhamu ya (feudalism). Na unapobadilika mujtama ukawa ni ubepari ikawa mashine ni chombo cha uzalishaji; kwa hivyo huchukuliwa nidhamu ya kibepari kutokana nayo. Nidhamu yake huchukuliwa kutokana na mabadiliko ya kimada. Ama mfumo wa kibepari huona kuwa pindi mwanadamu anapotenganisha dini na maisha huwa hakuna budi kwake ila ajiwekee nidhamu kwa nafsi yake juu ya maisha yenyewe. Akawa ni mwenye kuchukua nidhamu zake anazojitungia mwenyewe kutokana na mazingira yake. Ama Uislamu huona kuwa Mwenyezi Mungu ndiye aliyempangia mwanadamu nidhamu maishani ili ajipeleke kwa mujibu wake, na akamtuma bwana Muhammad (saw) kwa nidhamu hii na akaibalighisha. Basi ni wajibu kuishi kwa mujibu wake. Na kwa hivyo husoma tatizo na kisha kuchukua tatuo lake kutoka Kitabu na Sunna.

Ama kwa upande wa vipimo vya vitendo maishani, mfumo wa ukomunisti huona kuwa mada yaani nidhamu ya kimada ndiyo kipimo maishani; na kwa kubadilika kwake hubadilika kipimo. Na mfumo wa kibepari huona kuwa kipimo cha vitendo maishani ni manufaa, na jinsi yalivyo manufaa ndipo vitendo hupimwa na hutendwa juu ya msingi huu. Na Uislamu huona kuwa kipimo cha vitendo maishani ni halali na haramu, yaani maamrisho ya Mwenyezi Mungu na makatazo yake. Halali hutendwa na haramu huepukwa. Wala hayo hayabadiliki wala hayageuki, wala hayapimwi kwa manufaa bali hupimwa kwa Sharia tu basi.

Ama kwa upande wa mtazamo juu ya mujtamaa, mfumo wa kikomunisti huona kuwa mujtamaa ni mkusanyiko wa kijumla unaojumuisha ardhi, vyombo vya uzalishaji, maumbile na mwanadamu vyote huchukuliwa kama kitu kimoja nacho ni mada. Na pindi yanapobadilika maumbile hubadilika pamoja nayo yote yaliyomo, na pia mwanadamu hubadilika na hubadilika mujtamaa wote. Kwa hivyo huwa mujtamaa ni wenye kunyenyekea mabadiliko ya kimada na ni juu ya mwanadamu kuleta migongano ili kuharakisha mbadiliko huu. Na pindi unapobadilika mujtama hubadilika mtu binafsi kwa kubadilika kwake, na huzunguka pamoja nao kama linavyozunguka jino katika gurudumu.

Ama mfumo wa kibepari huona kuwa mujtamaa ni mkusanyiko wa watu binafsi na pindi yanavyo pangika mambo ya mtu binafsi basi hupangika mambo ya mujtamaa. Kwa hivyo hakuna budi ila kumtazama mtu binafsi pekee. Na serikali humfanyia kazi mtu binafsi na kwa hivyo umekuwa mfumo huu ni mfumo wa kibinafsi. Ama Uislamu huona kuwa msingi unaosimama juu yake mujtamaa ni aqida na inayoyabeba katika fikra na hisia, na nidhamu zinazotokana nayo (hiyo aqida). Pindi zinapotawala fikra za Kiislamu na hisia za Kiislamu, na kutabikishwa nidhamu za Kiislamu juu ya watu hupatikana mujtamaa wa Kiislamu. Kwa hivyo mujtamaa umekusanya watu, fikra, hisia na nidhamu. Mwanadamu peke yake pamoja na mwanadamu mwengine huwa ni kundi la watu tu, lakini haupatikani mujtamaa ila kwa fikra zinazobebwa na wanadamu, na hisia zao, na nidhamu zinazo tekelezwa juu yao. Kwa sababu kinacholeta mafungamano baina ya mwanadamu na mwanadamu mwengine ni maslahi, na maslahi pindi yanapounganika na fikra juu yake, na inapounganika hisia juu yake huunganika ridhaa na ghadhabu. Na inapo ungana nidhamu ambayo itakayo tatua basi hupatikana mahusiano baina ya mwanadamu mmoja na mwanadamu mwengine. Lakini zitakapo ikhitalifiana fikra juu ya maslahi au kukhitalifiana hisia juu yake hakutakuwa na muungano katika ridhaa wala ghadhabu, au ikitofautika nidhamu itakayo tatua baina ya mwanadamu mmoja na mwanadamu mwengine, hakutopatikana mahusiano hali itakayo fanya kusipatikane mujtamaa. Kwa hivyo huwa mujtama umejumuisha wanadamu, fikra, hisia na nidhamu kwa sababu (mambo haya) ndiyo yanayoleta mahusiano na kuufanya mujtama kuwa ni mujtama maalumu.

Kwa hivyo lau kama watu wote ni Waislamu na wangekuwa fikra walizozibeba ni za kibepari za kidemokrasia, na hisia wanazozibeba ni za kiroho za kikasisi au kizalendo na nidhamu inayo tekelezwa juu yao ni ya kibepari za kidemokrasia huwa mujtamaa ni mujtamaa usiokuwa wa Kiislamu hata kama wengi wa watu wake ni Waislamu.

Ama kuhusu upande wa utekelezaji wa nidhamu, mfumo wa kikomunisiti huona kuwa ni serikali peke yake inayo tekeleza nidhamu kwa nguvu za kijeshi na ukali wa kanuni, na husimamia mambo ya mtu binafsi na mambo ya jamii, na ndiyo inayobadilisha nidhamu. Na urasilmali huona kuwa serikali ndio inayo simamia uhuru, na pindi anapokiuka mmoja juu ya uhuru wa mwengine huzuia ukiukaji huu, kwa sababu imewekwa kudhamini uhuru, na asipokiuka mmoja juu ya uhuru wa mwengine hata kama

amemtumia na akachukuwa haki zake lakini kwa kuridhika kwake, wakati huo huwa hakuna ukiukaji wa uhuru na serikali haingilii. Kwa hivyo serikali ipo ili kudhamini uhuru.

Ama Uislamu huona kuwa nidhamu ina takelezwa na mtu binafsi muumini kwa msukumo wa uchajimungu, na hutekelezwa na serikali kwa kuhisi jamii uadilifu wake. Na kwa ushirikiano wa umma pamoja na mtawala kuamrisha mema na kukataza uovu, na kwa nguvu za serikali. Na husimamia serikali mambo ya jamii wala haimsimamii mtu binafsi mambo yake ila anaposhindwa nayo, na wala haibadiliki nidhamu katu. Na serikali ina uwezo wa kutabanni hukmu za kisheria yakiwa mengi matunda ya ijtihadi ndani yake.

Na fikra kiongozi ya mfumo wa Uislamu huafikiana na umbile la mwanadamu, pamoja na kina chake ni sahali na nyepesi (kuifahamu, na kuiamini). Haraka anapofungua mwanadamu akili yake na moyo wake ni haraka kuikubali na kuifahamu, na kuzama katika ufahamu kwa umakini na uhodari kwa sababu kuwa na hisia ya kuabudu ni katika umbile la mwanadamu, na kila mwanadamu kwa maumbile yake ni mwenye kutaka kuabudu. Wala haiwezi nguvu yoyote kung'oa kutoka kwake umbile hili, kwa sababu inahusiana naye. Mwanadamu kwa umbile lake hujihisi kuwa yeye ni mpungufu na kuwa kuna nguvu iliyokamilika kumshinda yeye, na kwamba nguvu hiyo yastahiki kutukuzwa. Na sifa ya dini ni kumhitaji muumba anayeendesha, inayotokana na udhaifu wa kiasili katika maumbile ya mwanadamu. Nayo ni ghariza thabiti ilio na athari maalumu nayo ni kutukuza, kwa hivyo wamekuwa wanadamu kupitia karne zote wakiabudu kitu. Wakaabudu wanadamu, nyota, mawe, wanyama, moto na mengineyo. Ulipokuja Uislamu na aqida yake, ulikuja kuwatoa watu kutoka ibada ya kuwaabudu viumbe kufikia ibada ya Mwenyezi Mungu aliyeumba kila kitu. Na ulipodhihiri mfumo wa kimada unaokanusha kuwepo kwa Mwenyezi Mungu na kukanusha roho, haukuweza kuimaliza hiyo hisia ya dini ya kimaumbile, bali ukahamisha sura ya mwanadamu juu ya nguvu kubwa kumshinda yeye na kuhamisha kutukuza nguvu hiyo, ukahamisha yote hayo kuwa na sura ya kwamba nguvu hiyo iko katika mfumo na kwa wanaoubeba. Ukafanya kutukuzwa ni kwa haya mawili tu kana kwamba ikamrudisha nyuma na kuhamisha kutukuza watu kutoka kumuabudu Mwenyezi Mungu kufika kuabudu waja wa Mwenyezi Mungu, na kutoka kutukuza aya za Mwenyezi Mungu kufikia kutukuza maneno ya viumbe, basi ukawa ni wenye kurudi nyuma katika haya. Wala hauwezi kumaliza umbile la hisia ya dini, lakini ukaibadilisha kwa kuchanganyikiwa mbadiliko ya kurudisha nyuma. Kwa hivyo umekhitalifiana uongozi wake wa kifikra na umbile la mwanadamu na umekuwa uongozi kombo; na kufikia hapa umekuwa uongozi wa kifikra wa kikomunisti ni wenye kuzorota katika upande wa kimaumbile. Lakini wakadanganya kwa kuahidi kujaza matumbo, wakashawishi walio na njaa, walio na khofu na walio kata tamaa. Na wakashikana nao wale waliozorota walio duni maishani, wenye hila mbaya maishani na waliolemaa kiakili mpaka wakaambiwa ndio walio na akili pindi wanapozungumza kwa mtazamo wa mabadiliko ya kimada ulio dhihirisha ufisadi zaidi na uliokanushwa kwa ushahidi wa kihisia na kiakili pamoja. Na unatumia mbinu ya ki-nguvu ili kuwalazimisha watu na mfumo wao; na kufikia hapa twaona kuwa ukandamizaji na unyanyasaji na mapinduzi, uchafuzi, uharibifu na balaa ni miongoni mwa mbinu muhimu kwake.

Na hivyo hivyo uongozi wa kifikra wa kibepari umekhalifu umbile la mwanadamu ambalo ni umbile la kuabudu, kwa sababu umbile la kuabudu kama linavyojitokeza katika kutukuza, hujitokeza katika kupeleka mwanadamu mambo yake maishani kwa kudhihirika ikhtilafu na migongano pindi anapotekeleza mambo hayo. Na hii ni dalili ya kushindwa kwake (huo uongozi wa kifikra), kwa hivyo hakuna budi ila kufanya dini ndio inayompangia mwanamdamu vitendo vyake maishani. Kutenganisha dini na maisha ni kinyume na umbile la mwanadamu. Na hii haimaanishi kuwepo dini maishani ni kufanya

vitendo vyote maishani ni ibadati, bali maana ya kuwepo dini maishani ni kuifanya nidhamu alioiamrisha kwayo Mwenyezi Mungu ndio inayotatua matatizo ya mwanadamu maishani. Nidhamu hiyo hutokana na aqida inayokiri yaliyomo katika maumbile ya mwanadamu, na kuiweka mbali na kuchukuwa nidhamu inayotokana na aqida isiyowafikiana na ghariza ya kuabudu inayokhalifu maumbile ya mwanadamu. Kwa hivyo uongozi wa kifikra wa kibepari umezorota katika upande wa kimaumbile kwa sababu ni uongozi wa ki-makosa kwa kutenganisha dini na maisha; na kwa kuiweka kwake dini mbali na maisha na kuifanya ni jambo la kibinafsi, na kwa kutenganisha nidhamu ambayo Mwenyezi Mungu ameiamrisha kutatua matatizo ya mwanadamu.

Na uongozi wa kifikra wa Kiislamu ndio uongozi ulio sawa kwa sababu umefanya akili kuwa ni msingi wa imani juu ya kuwepo Mwenyezi Mungu kwani unaupeleka mtazamo kwa yaliyomo ulimwenguni, mwanadamu na uhai jambo linalobeba kuamini imani ya kukatikiwa (*jazm*) ya kuwepo Mwenyezi Mungu aliyeumba viumbe hivi. Na humuainishia mwanaadamu anachokitafuta kimaumbile kwa mkamilifu aliyekamilika asiyepatikana kwa mwanadamu, ulimwengu na uhai, na (uongozi wa kifikra) huongoa akili yake kwake (Mwenyezi Mungu) hivyo humtambua na kumuamini.

Ama uongozi wa kifikra wa kikomunisti, umejengeka juu ya mada na sio akili hata kama imefikiwa na akili, kwa sababu ukomunisti husema kuwa mada ilikuwepo kabla ya fikra na ukaifanya ndio asili ya vitu navyo ni vya kimada. Ama uongozi wa kifikra wa kirasilmali umejengwa juu ya suluhisho la kati na kati ambalo umelifikia baada ya mapambano ya kumwaga damu yaliyoendelea kwa karne kadhaa baina ya watu wa kanisa na watu wa falsafa ambayo natija yake ni kutenganishwa dini na serikali.
Kwa hivyo uongozi wa kifikra hizi mbili za ukomunisti na urasilmali umepotea kwa sababu umegongana na maumbile na haukujengwa juu ya akili.

Kwa hivyo uongozi wa Kiislamu ndio uongozi wa kifikra pekee ulio sahihi, na usiokuwa huo ni uongozi wa kifikra ulio fisidika kwa sababu uongozi wa kifikra wa Kiislamu umejengwa juu ya akili, wakati ambapo uongozi mwengine wa kifikra haukujengwa juu ya akili. Na pia kwa sababu uongozi wake wa kifikra huwafikiana na umbile la mwanadamu basi anauitikia, wakati ambao uongozi mwengine wa kifikra hukhalifu maumbile ya mwanadamu. Na hilo ni kuwa fikra kiongozi ya kikomunisti imejengwa juu ya mada na sio akili, kwa sababu husema kuwa mada hutangulia fikra yaani hutangulia akili. Kwa hivyo mada pindi inapomulikwa juu ya ubongo hupatikana kwa sababu yake fikra. Hufikiri juu ya mada iliomulikwa juu yake. Ama kabla ya kumulikwa mada juu ya ubongo haipatikaniki fikra, kwa hivyo kila kitu kimejengwa juu ya mada. Na asili ya aqida ya kikomunisti yaani uongozi wa kifikra wa kikomunisti ni mada na sio akili.

Na hilo ni kosa kwa pande mbili. Kwanza, haupatikani umulikaji baina ya mada na ubongo. Ubongo haumuliki juu ya mada, wala mada haimuliki juu ya ubongo, kwa sababu umulikaji huhitaji kuwepo uwezekano wa umulikaji juu ya kitu kitakacho mulikwa kama kioo. Hakika yake huhitaji uwezekano wa umulikaji juu yake. Na hili halipatikani, si katika ubongo wala si katika hali ya mada. Kwa hivyo haupatikani umulikaji baina ya mada na ubongo kabisa, kwa sababu mada haimuliki juu ya ubongo na wala hainukuliwi kwake, bali hunukuliwa kwa kuhisiwa kufikia katika ubongo kwa njia ya hisia. Na kunukuliwa mada na hisia kufikia ubongo sio umulikaji wa mada juu ya ubongo wala umulikaji wa ubongo juu ya mada bali ni kuhisiwa kwa mada tu. Wala hakuna tofauti baina ya jicho na kisicho kuwa jicho miongoni mwa hisia, hupatikana hisia katika kugusa, kunusa, kuonja na kusikia kama inavyo patikana katika kuona. Basi kinachopatikana kutokana na vitu sio umulikaji juu ya ubongo bali ni hisia juu ya vitu. Mwanadamu huhisi vitu kupitia hisia zake tano wala havimuliki vitu juu ya ubongo wake.

Pili, haipatikani fikra kutokana na hisia peke yake, bali kinachopatikana ni hisia pekee yaani kuhisi juu ya hali (waqia) na hisia juu ya hisia izidi hisia mara milioni, jinsi itakavyo ongezeka sampuli ya hisia, itafikia tu hisia wala si fikra kabisa. Bali hakuna budi ila kuwepo elimu iliyotangulia kabla kwa mwanadamu ili afasiri kuipitia hali anayoihisi mpaka apate fikra. Tukimchukua mwanadamu wa leo, mwanadamu yeyote, na tumpe kitabu kilicho andikwa kwa lugha ya '*Siriyaniyya*' (lugha ya kale ya Bilad Ash-Sham) na akawa hamiliki elimu itakayo muunganisha na lugha hiyo, na tujaalie hisia zake zitulie juu ya kitabu kwa kukiona na kukigusa, kisha tuzikariri hisia hizi mara milioni moja, hatokuwa na uwezo wa kujua hata neno moja. Mpaka apewe elimu juu ya lugha ya '*Siriyaniyya*' na kinachohusika na '*siriyaniyya*', basi wakati huo huanza kufikiria juu yake na kuitambua. Hivyo hivyo tukimchukua mtoto mchanga ambaye ana hisia lakini hana elimu yoyote, kisha tumuwekee mbele yake kipande cha dhahabu na kipande cha shaba na jiwe, na tujaalie kwamba hisia zake zote zishiriki kuhisi vitu hivi, hatokuwa na uwezo wa kuvifahamu hata kama tutamkaririsha hisia juu yake na sampuli zake. Lakini tukimpa elimu juu yake kisha avihisi, basi atatumia elimu na kuvitambua. Mtoto huyu huyu lau atakuwa kiumri na kufikia miaka ishirini na asipate elimu yoyote atabakia kama siku ya kwanza akihisi vitu tu wala havitambui vyovyote litakavyokuwa bongo lake. Kwa sababu kinachomfanya mtu kutambua sio bongo, bali ni elimu iliyotangulia (*alma'aluumaat assaabiqah*) pamoja na bongo na hali anayoihisi. Hii ni kwa upande wa utambuzi wa kiakili. Ama katika upande wa utambuzi wa kihisia hiyo ni natija ya ghariza na mahitaji ya kiviungo. Kinacho patikana katika wanyama hupatikana katika wanadamu. Hujulikana kwa kukariri kupeana tufaa na jiwe, kuwa tufaa huliwa na jiwe haliliwi, kama anavyojua punda kuwa ngano huliwa na mchanga hauliwi. Upambanuzi huu sio fikra wala sio utambuzi bali hutokana na ghariza na mahitaji ya kiviungo. Nayo hupatikana katika wanyama kama inavyopatikana katika wanadamu. Kwa hivyo haimkiniki kupatikana fikra ila baada ya kupatikana elimu iliyo tangulia (*previous information*) pamoja na kunukuliwa hisia ya hali ilivyo (*reality*) kupitia viungo vya hisia kufikia ubongo.

Kwa hayo akili au fikra au utambuzi ni kunukuu hisia juu ya hali ilivyo kupitia viungo vya kuhisi kufikia ubongo na kuwepo elimu iliyo tangulia inayo fasiri hali ilivyo. Kwa hivyo fikra kiongozi ya kikomunisti ni ya kimakosa na fisifidifu kwa sababu haikujengwa juu ya akili, kama ilivyo fisidika kwake maana ya akili na fikra.

Na hivyo hivyo uongozi wa kifikra wa kibepari uliojengwa juu ya suluhisho la kati na kati baina ya watu wa kanisa na wajuzi (*mufakirina*). Baada ya mpambano mkali ulioendelea kwa karne kadhaa baina ya watu wa dini na *mufakirina*, suluhisho walilofikia ni suluhisho la kati na kati nalo ni kutenganisha dini na maisha, yaani linalokiri kindani kuwepo dini pamoja na kuitenganisha kwake na maisha. Kwa hivyo uongozi wake wa kifikra haukujengwa juu ya akili bali ni suluhisho la maridhiano au la kati na kati. Kwa hivyo tutakuta kwamba suluhiso la kati na kati ni asili ya fikra yao. Nao hukurubisha baina ya haki na batili kwa suluhisho la kati na kati, na baina ya imani na ukafiri kwa suluhisho la kati na kati, na baina ya nuru na giza kwa suluhisho la kati na kati. Pamoja na kuwa suluhisho la kati na kati ni suluhisho lisilo kuwepo, kwa sababu mas'ala ima ni haki au batili, ima ni imani au ukafiri, na imma ni nuru au giza. Lakini suluhisho la kati na kati walio lijengea juu yake aqida yao na fikra yao kiongozi limewaweka mbali na haki, imani na nuru. Kwa hivyo fikra yao kiongozi ni fisidifu kwa sababu haikujengwa juu ya akili.

Ama fikra kiongozi ya Kiislamu, hakika yake ni kuwa imejengwa juu ya akili, pindi inapofaradhisha (juu ya) Muislamu kuamini kuwepo Mwenyezi Mungu na Utume wa Muhammad na Al-Qur'an Al-Kariim kwa njia ya ki-akili. Na humfaradhishia kuamini vitu asivyoviona (*ghayb*) lakini vikitokana na kitu kilichothubutu kuwepo kwake kupitia akili

kama Al-Qur'an Al-Kariim na hadithi zilizo pokelewa na wapokezi wengi (*mutawatir*). Kwa hivyo fikra kiongozi ya Kiislamu imejengwa juu ya akili. Huu ni upande wa ki-akili.

Ama kwa upande wa kimaumbile, fikra kiongozi ya Kiislamu inaafikiana na maumbile kwa sababu huamini kuwepo dini na uwajibu wake kuwepo maishani. Na hupeleka maisha kwa mujibu wa maamrisho ya Mwenyezi Mungu na makatazo yake. Hisia ya kuabudu ni maumbile kwa sababu ni ghariza miongoni mwa ghariza, nayo ina athari maalumu ambayo ni kutukuza inayotofautiana na athari za ghariza nyengine. Hiyo ni athari ya kimaumbile ya ghariza maalumu. Kwa hivyo imani kwa dini, na uwajibu wa kupeleka mambo ya mwanadamu maishani kwa mujibu wa maamrisho ya Mwenyezi Mungu na makatazo Yake ni jambo linalotokana na ghariza. Basi huwafikiana na maumbile kwa hivyo mwanamdau huitikia.

Tofauti na fikra mbili kiongozi za ukomunisti na ubepari zinazo tofautiana na maumbile, kwa sababu fikra kiongozi ya kikomunisti hukanusha kamwe kuwepo dini na hupiga vita kuitambua, hivyo hugongana na maumbile. Na fikra kiongozi ya kibepari haitambui dini wala haikanushi, wala haifanyi kutambua kwake au kukanushwa kwake ni jambo la uchunguzi. Lakini husema ni wajibu kutenganisha dini na maisha, na hutaka maisha yapelekwe kimanufaa peke yake bila ya dini kuwa na usemi wowote. Na hili hugongana na maumbile na ni mbali nayo. Kwa hivyo imekuwa fikra kiongozi ya kibepari imegongana na maumbile ya mwanadamu.

Na kufikia hapa twakuta kuwa fikra kiongozi ya Kiislamu ni pekee inayofaa kwa kuafikiana kwake na maumbile ya mwanadamu na kuafikiana kwake na akili, na kisichokuwa fikra kiongozi ya Kiislamu ni batili. Kwa hivyo imekuwa fikra kiongozi ya Kiislamu pekee ndio sahihi na ndio pekee yenye kufaulu.

Limebakia suala moja nalo ni: Je, Waislamu walitekeleza Uislamu? au walikuwa wamebeba aqida yake na kutekeleza nidhamu na hukmu nyengine? Jawabu kwa haya ni kuwa Waislamu waliutekeleza Uislamu pekee katika zama zote tangu alipofika Mtume (saw) Madina mpaka 1336 Hijri yaani 1918 miladiyya ilipoanguka serikali ya mwisho ya Kiislamu chini ya mikono ya mabepari. Na ulikuwa utekelezaji wake ni utekelezaji kamili mpaka ukafaulu utekelezaji huo kwa kiwango kikubwa cha kufaulu.

Ama kuhusu kuwa Waislamu walitekeleza Uislamu kivitendo, hakika kile kinachotabikisha nidhamu ni serikali na wenye kutabikisha katika serikali ni watu wawili. Mmoja wao ni kadhi anayeamua kesi za uhasama baina ya watu, na wa pili ni mtawala anayetawala watu. Ama kadhi, imenukuliwa kwa njia ya upokezi wa wengi (*tawatur*) kuwa ma-kadhi wanaoamua uhasama baina ya watu tangu wakati wa Mtume (saw) mpaka mwisho wa Khilafah katika Istanbul walikuwa wakiziamua kwa mujibu wa ahkamu za Sheria tukufu katika mambo yote maishani. Sawa sawa yawe ni baina ya Waislamu peke yao au baina ya Waislamu na watu wengine. Na ilikuwa mahakama inayoamua husuma zote katika haki, malipo, hali za kibinafsi na yasiyokuwa hayo ni mahakama moja inayohukumu kwa Sheria ya Kiislamu peke yake. Wala haikupokelewa kutoka kwa mtu yeyote kuwa (hata) kesi moja iliamuliwa kwa tafauti na ahkamu za Sheria za Kiislamu, au kuwa mahakama yoyote katika biladi ilihukumu kwa tofauti na Uislamu kabla ya kugawanywa mahakama kuwa za kisheria na za kinidhamu kwa taathira ya ubepari. Dalili iliyo karibu ni jalada za mahakama za kisheria zilizo hifadhiwa katika miji ya zamani kama Al-Quds, Baghdad, Damascus (Syria), Misr na Istanbul na miji mengine ambayo ni dalili ya yakini kuwa Sheria ya Kiislamu ndio pekee ilio tekelezwa na ma-Kadhi. Mpaka wasiokuwa Waislamu miongoni mwa wakristo na mayahudi waliisoma fiqhi ya Kiislamu na kuitungia vitabu, mfano Saliim Al-Baz aliye

sherehesha makala ya “Al-Majalla” (gazeti rasmi) na wengineo waliotunga katika fiqhi ya Kiislamu katika zama za mwisho. Ama kilichoingia katika kanuni, zilizoingia kufuatia fatwa za maulamaa kuwa kanuni hizo hazikhalifu hukmu za Kiislamu. Na hivi ndivyo zilivyo ingizwa kanuni za adhabu za ki-Uthmani katika mwaka 1275 Hijri sawa na 1857 Miladi, na zikaingizwa kanuni katika haki na biashara mwaka 1276 Hijri sawa na 1858 Miladi kisha katika mwaka 1288 Hijri sawa na 1870 Miladi. Mahakama zikagawanywa vigawanyo viwili, mahakama za ki-Sheria na mahakama za kawaida na kukatolewa agizo la kupangiliwa hivyo. Mwaka wa 1295 Hijri sawa na 1877 Miladi ilitolewa amri ya kubuniwa kwa mahakama ya kikanuni. Na zikawekwa kanuni za ki-msingi za mahakama ya haki na malipo mwaka 1296 Hijri. Na pindi walipokosa maulamaa kisababu kitakacho halalisha kuingizwa sheria za kiraia (civil law) katika serikali kuliwekwa jarida la Shari'ah (*al-Majallah*) kupangilia maingiliano (*mu'amalat*) mwaka 1286 Hijri sawa na 1868 Miladi.

Kanuni hizi ziliwekwa kama hukmu zilizo ruhusiwa na Uislamu na wala hazikuwekwa katika hali ya utendaji ila baada ya kuchukuliwa fatwa za kuziruhusu, na baada ya kuidhinishwa na Sheikh al-Islam kama ilivyobainika katika maandishi yaliyotoka kuzitangaza. Na kwa hakika ulikuwa ubepari tangu mwaka 1918 walipoziteka biladi za Kiislamu, walikuwa wakiamua husuma za kesi za raia kwa kutumia zisizokuwa Sheria za Kiislamu. Lakini biladi ambazo hazikuvamiwa na majeshi ya ukoloni lakini zipo chini ya nguvu zake ziliendelea kuhukumu kwa kutumia Uislamu, mfano Hijazi, Najd na Yemen na miji ya Afghanistan—hata kama  viongozi katika biladi hizi hawatekelezi Uislamu kwa sasa. Pamoja na hilo, twaona kwamba Uislamu ulitekeleza kimahakama wala hawakutekeleza tofauti na hayo katika zama zote za serikali ya Kiislamu.

Utekelezwaji wa Uislamu na kiongozi, hilo huwakilishwa ndani ya Ahkamu za kiShari'ah kuhusiana na mambo matano: mujtama, uchumi, elimu, siasa za kigeni na utawala. Hukumu za kiShari'ah kuhusiana na mambo hayo zilitekelezwa na serikali ya Kiislamu. Ama nidhamu ya kijamii inayopanga mahusiano baina ya mwanamke na mwanamume na yanayotokana na mahusiano haya, yaani hali ya ki-binafsi, hakika haijawachwa kutekelezwa mpaka leo pamoja na kuwepo ubepari na kuwepo hukmu za kikafiri; wala hakuna jengine lililo tabikishwa mpaka leo. Ama nidhamu za kiuchumi hudhihirika katika pande mbili. Upande wa kwanza ni jinsi serikali inavyochukuwa mali kutoka kwa watu ili kutatua matatizo ya watu, na pili ni vipi inavyozitumia. Ama jinsi inavyozichukua, ilikuwa ikichukua zaka za mali, ardhi, wanyama na nyenginezo kwa sifa yake kama ibada na kuzigawanya baina ya vile vikundi vinane tu vilivyotajwa katika Qur'an, wala hazikutumiwa kupeleka mambo ya serikali. Na huchukua mali ya kupeleka mambo ya kiserikali na Ummah kama ilivyoeleza Sheria, wala haikuchukuwa nidhamu yoyote ya kodi bali ilitabikisha Uislamu tu. Ilichukua kharaji katika ardhi, ikachukua jizya kutoka kwa wasiokuwa Waislamu, na ilichukua kodi ya forodha kwa uangalizi wake wa biashara za nje na ndani. Wala haikuwa ikipata mali ila kwa njia ya Sheria ya Kiislamu. Ama kugawanya mali, ilikuwa ikitekeleza hukmu za kumsimamia aliyeshindwa kujisimamia na kumuangalia safihi (anayeshindwa kusimamia mali yake vizuri) na mbadhirifu (mwenye israfu) na kumuwekea msimamizi. Na ilikuwa ikijenga majumba katika kila mji na katika njia ya Hijja ili kuwalisha mafakiri, maskini na wapita njia. Na mpake leo ziko athari zake katika miji mikuu katika biladi za Waislamu. Basi kwa jumla kilichoendelea ni kutumiwa mali na serikali kwa mujibu wa Sheria, wala katu haikupelekwa kinyume chake. Kilichoshuhudiwa katika upungufu kwa upande huu ilikuwa ni utepetevu na utekelezaji wa kimakosa wala sio kutokuwepo kwa utekelezaji wa Shari'ah.

Amma elimu, hakika siasa yake ilikuwa imejengwa juu ya msingi wa Kiislamu. Yalikuwa mafundisho ya Kiislamu ndio msingi wa manhaj ya elimu na ulifanywa ulinzi mkubwa kutochukuliwa *thaqafa* ngeni ikiwa ina gongana na Uislamu. Ama upungufu katika

kujenga vyuo vya elimu, ulitokea mwishoni mwa serikali ya ki-Uthmani kwa usawa katika kila biladi za Kiislamu, kwa sababu ya kuzorota ki-fikra kulikofikia kilele chake wakati huo. Ama zama zilizobakia, ilikuwa ni mashuhuri katika ulimwengu mzima kuwa biladi za Kiislamu zilikuwa pekee ndio kituo cha kuelekea cha ma-ulamaa na wanafunzi. Na vituo vikuu vya Cordoba, Baghdad, Damascus, Alexandria na Cairo vilikuwa na athari kubwa katika kuelekeza elimu katika ulimwengu.

Ama siasa za kigeni, hakika yake ilijengwa juu ya msingi wa Uislamu. Serikali ya Kiislamu ilikuwa ikijenga mahusiano yake pamoja na serikali nyengine juu ya msingi wa Uislamu, na serikali zote zilikuwa zikiiangalia kwa sifa yake kama serikali ya Kiislamu. Na yalikuwa mahusiano yake yote ya kigeni yamejengwa juu ya Uislamu na maslahi ya Waislamu kama Waislamu. Ama siasa ya kigeni ya serikali ya Kiislamu kuwa ni siasa ya Kiislamu, hili lilikuwa ni jambo mashuhuri kiulimwengu mpaka halihitaji dalili yoyote.

Ama katika upande wa nidhamu ya utawala, uhakika wa muundo wa serikali katika Uislamu umejengwa juu ya nguzo nane nazo ni: Khalifah naye ndiye kiongozi wa serikali, wasaidizi (*muawinun*) wake katika utawala, wasaidizi watendaji, ma-wali, ma-Kadhi, Amir al-Jihad, Idara za serikali na Majlis Al-Umma. Muundo huu ulikuwepo na Waislamu hawakupitiwa na wakati wowote bila Khalifah ila baada ya makafiri mabepari walipoiondoa Khilafah kwa kutumia mkono wa Kamal Ataturk mwaka 1342 Hijri mwaka 1924 Miladi. Ama kabla ya hapo Waislamu daima walikuwa na Khalifah, akiondoka mmoja huja baada yake mwengine hata katika nyakati za uzorotefu zaidi. Na pindi anapokuwepo Khalifah huweko serikali ya Kiislamu, kwa sababu serikali ya Kiislamu ndio Khalifah. Ama wasaidizi vivyo hivyo walikuwepo katika zama zote na walikuwa ni watekelezaji tu wala sio mawaziri hata kama wameitwa jina la mawaziri katika zama za ukoo wa Abasiyya. Lakini wao ni wasaidizi wala hawakuwa na sifa za mawaziri kama walioko sasa katika nidhamu ya utawala ya kidemokrasia, bali walikuwa ni wasaidizi na kiungo cha utekelezaji pekee, na uwezo wote ulikuwa ni wa Khalifah. Ama ma-Wali na ma-Kadhi wa idara za ki-serikali, kuwepo kwake ni jambo thabiti. Na kafiri pindi alipozikoloni biladi zetu yalikuwa mambo haya yakiendelea, na walikuwepo ma-wali, ma-Kadhi na idara za ki-serikali, kitu kisicho hitaji dalili. Ama amiri wa jihadi, alikuwa akipeleka mambo ya jeshi kwa mtazamo wa kuwa jeshi ni la Kiislamu na ulimwengu wote ulifahamu kuwa jeshi la Kiislamu halishindwi. Ama Majlis al-Umma, hakika baada ya ma-Khalifah Rashidun kuweko kwake hakukutiliwa umuhimu, na sababu yake ni kuwa shura sio nguzo miongoni mwa nguzo za utawala hata kama ni katika muundo wa serikali. Shura ni haki miongoni mwa haki za raia juu ya mtawala. Asipoitekeleza atakuwa amefanya upungufu lakini utawala utabakia ni utawala wa Kiislamu. Hiyo ni kwa sababu shura ni kuchukuwa rai na sio kuhukumu, tofauti na kikao cha wawakilishi cha kidemokrasia. Na kutokana na haya hubainika kuwa nidhamu ya utawala iliyokuwa ikitekelezwa ni Uislamu.

Na hapa huja mas-ala juu ya kubaiishwa Khalifah. Ni katika jambo liliokatikiwa kuwa haikuwa Khilafah ni nidhamu ya kurithiwa, yaani haikuwa kurithi ni hukmu iliyoruhusiwa katika serikali katika kuchukuwa utawala, yaani kuchukuwa uongozi wa serikali kama ilivyo wajibishwa katika nidhamu ya kifalme. Hakika kilicho ruhusiwa katika kuchukuwa utawala ni bay’ah, na ilikuwa ikichukuliwa kutoka kwa Waislamu katika zama fulani na kutoka kwa watu wenye usemi (*Ahl al-Hall wa al-‘Aqd*) wakati mwengine, na kutokana na Sheikh ul-Islam katika mwishoni mwa zama za uzorotefu. Kilichotendeka katika zama zote za serikali ya Kiislamu ni kuwa hatawazwi Khalifah ila baada ya kupewa bay’ah, wala hakutawazwa kwa urathi pasina bay’a katu; haikupokewa hata kisa kimoja kwamba ametawazwa Khalifah kwa urathi pasina bay’ah. Lakini kuchukuwa bay’ah ilikuwa ikitabikishwa vibaya, basi alikuwa Khalifah akiichukuwa kutoka kwa watu katika uhai

wake kwa ajili ya mtoto wake au ndugu yake au binamu yake au mtu yeyote katika ukoo wake, kisha bay'ah mpya ilipewa kwa mtu huyu baada ya kufa Khalifah. Huu ni utabikishaji mbaya wa bay'ah wala sio urathi au mrathi aliyechaguliwa (*wilayat al-'ahd*). Kama ilivyo katika kura za wabunge katika nidhamu ya kidemokrasia, hutokea utabikishaji mbaya lakini bado huitwa kura na wala hauitwi uteuzi hata akishinda kura hizo mtu aliyependwa na serikali. Kwa hayo yote, tunaona kuwa nidhamu ya Kiislamu imetekelezwa kivitendo na wala hakuna chengine kilichotekelezwa katika zama zote za serikali ya Kiislamu.

Ama kuhusu kufaulu kwa uongozi huu kivitendo, kufaulu kwake kulikuwa khasa katika mambo mawili yafuatayo:

Ama la kwanza, hakika uongozi wa kifikra wa Kiislamu ulihamisha taifa (*sha'ab*) la waarabu kutoka katika hali duni ya kifikra iliochanganyikiwa katika giza la vita vya ukabila, vya ukoo na giza la ujinga kwenda katika zama ya mwamko wa kifikra unao meremeta kwa nuru ya Uislamu ambayo nuru ya jua lake haikuangaza juu ya waarabu tu bali ili jumuisha ulimwengu mzima. Waislamu walitapakaa ulimwengu mzima na kuubeba Uislamu kwa ulimwengu wote, na wakatawala biladi ya Fursi, Iraq, Sham na Kaskazini mwa Afrika. Lilikuwa kila taifa miongoni mwa mataifa haya ni tofauti na jengine, na lugha yake tofauti na nyengine. Lilikuwa kabila la kifursi katika biladi Fursi ni tofauti na kabila la kirumi katika Sham, na tofauti na kabila la Kupti katika Misri, na tofauti na ma-Barbera katika kaskazini mwa Afrika. Na zilikuwa ada zao, mila zao na dini zao ni tofauti. Na pindi walipokuwa katika kivuli cha utawala wa Uislamu haikuchukuwa muda ila wakaufahamu Uislamu na wote wakasilimu na wote wakawa umma mmoja nao ni Umma wa Kiislamu. Kwa hivyo ilikuwa kufaulu kwa uongozi wa kifikra wa Kiislamu katika kuwaunganisha watu na mataifa ni kufaulu kusikokuwa na kifani, pamoja na kuwa mbinu za usafiri zilikuwa ni kwa kutumia ngamia na mbinu ya kuueneza ni kupitia mdomo na kalamu.

Ama ukombozi, ulikuwa ni kutumia nguvu kuondoa nguvu na kuvunja kizuizi cha nguvu mpaka wawachwe watu na kinacho waongoza kwacho akili au kuwaongoza kwayo maumbile. Kwa hilo waliingia watu katika dini ya Mwenyezi Mungu kwa makundi. Ama ukombozi wa kijeuri hutenganisha baina ya mkombozi na aliyekombolewa, na baina ya mshindi na mshindwa. Ukoloni wa Kimagharibi katika Mashariki kwa miongo kadhaa bila ya kupata ushindi, jambo lililo mbali, na lau kama si athari ya thaqafa yenye kupoteza ungelikuwa ushafutwa, na lau kama si ukandamizaji wa viongozi vibaraka ungekuwa ushaondoka ukoloni. Na ingelikuwa kurudi kwa Uislamu kama mfumo na nidhamu zake ni haraka kuliko kupepesa jicho. Tunarudia na tunasema, ilikuwa kufaulu kwa uongozi wa kifikra wa Kiislamu katika kuunganisha watu ni kufaulu kusiko kuwa na kifani, na wakabakia watu hao mpaka leo ni Waislamu pamoja na mikasa iliyoletwa na ubepari na uchafu wake na vitimbi vyake katika kufisidi aqida na kuzitia sumu fikra. Na utabaki mpaka kitakapo simama Qiyama kuwa ni Umma mmoja wa Kiislamu. Wala haijatokea kwamba taifa lolote miongoni mwa mataifa lilioamini Uislamu kuritadi kutoka Uislamu.

Ama Waislamu wa Andalus (Spain), walimalizwa na mahakama za kuhoji (inquisition courts), na majiko ya moto. Na Waislamu wa Bokhara (biladi katika Uzbekistan) na Al-Qoqaz (Caucasus) na Turkistan (eneo la Asia ya kati lililokusanya nchi kadhaa), walifikwa na mkasa uliowafikia waliowatangulia. Uislamu wa watu hawa na kuunganishwa kwao kama Umma mmoja, na pupa yao kubwa kwa aqida yake, hutoa sura ya kiwango kilichofikia kufaulu kwa fikra kiongozi hiyo na serikali ya Kiislamu katika kutekeleza nidhamu ya Kiislamu.

Ama jambo la pili linaloonyesha kufaulu kwa uongozi huu, ni kuwa Umma wa Kiislamu ulikuwa ni umma ulio mbele ulimwenguni katika hadhara, madaniyya, thaqafa na sayansi. Na ikawa serikali ya Kiislamu ndio serikali kuu katika ulimwengu iliyo na nguvu zaidi kwa muda wa karne kumi na mbili kutoka karne ya saba miladi mpaka kati kati ya karne ya kumi na nane miladi, na ilikuwa pekee ndio uwa la waridi duniani na jua linalochomoza katika ummati zote kwa muda wote huo. Jambo linalothibitisha kufaulu kwa uongozi huu, na kufaulu kwa Uislamu katika kutekeleza nidhamu yake na aqida yake juu ya watu. Na pindi ilipowacha serikali ya Kiislamu na Umma wa Kiislamu kubeba fikra kiongozi, pindi ilipowacha kulingania Uislamu na ikawa na upungufu katika kuufahamu Uislamu na kuutabikisha ulirudi nyuma kati ya ummati nyengine.

Na kwa haya twasema kuwa fikra kiongozi ya Kiislamu ndio pekee inayofaa na ndio pekee inayopaswa kubebwa kwa ulimwengu. Pindi itakaposimama serikali ya Kiislamu inayobeba uongozi huu (wa kifikra) itakuwa kufaulu uongozi huu leo kama ulivyoweza kufaulu jana.

Tumesema kuwa Uislamu unaafikiana na maumbile ya mwanadamu kwa yale yaliyotokana kwayo katika nidhamu. Kwa haya hahisabiwi mwanadamu kuwa chombo cha sanaa anayeishi bila hitilafu na anatekeleza nidhamu bila tofauti kwa vipimo makini vya kihandisi, bali huhisabiwa mwanadamu kama kiumbe cha mujtama anayetekeleza nidhamu kama kiumbe cha mujtama kinacho tofautiana kinguvu na kisifa. Ni katika hali ya kimaumbile kwa upande mmoja kukurubisha baina ya watu bila kuwafanya sawa pamoja na kudhamini utulivu kwa wote. Na ni katika hali ya kimaumbile kwa upande mwengine, na haya maudhui ndio yatakayo chambuliwa sasa, kwamba baadhi ya watu binafsi kwa hisabu hiyo huenda kombo na kukhalifu nidhamu inayo tabikishwa (tekelezwa). Na watu binafsi wasiitikie nidhamu hiyo, na watu binafsi waipe nyongo nidhamu hiyo. Kwa hivyo hakuna njia ya kujiepusha na kuwepo mafasiki na waovu katika mujtama, na kuwepo makafiri na wanafiki, na kuweko wanaoritadi na wasio muamini mungu, lakini huchukuliwa mujtama kwa ujumla kwa jinsi ilivyo fikra, hisia, nidhamu na watu. Huchukuliwa kuwa ni mujtama wa Kiislamu unao tabikisha (tekeleza) Uislamu pindi unapodhihirika kwake Uislamu katika vitu hivi.

Dalili juu ya hayo ni kuwa haimkini kwa mtu yeyote kuweza kutabikisha nidhamu ya Kiislamu kama alivyoitabikisha Muhammad (saw), Mtume wa Mwenyezi Mungu. Pamoja na hilo walipatikana katika zama zake makafiri na wanafiki, na wakapatikana mafasiki na waovu, na wakapatikana walioritadi na wasio muamini mungu. Lakini hakuna awezaye ila kusema kwa yakini kuwa: Uislamu ulikuwa ukitabikishwa kikamilifu, na mujtama ulikuwa wa Kiislamu. Lakini utabikishaji huu ni juu ya mwanadamu ambaye ni kiumbe cha kimujtama na sio chombo cha sanaa.

Na ulikuwa Uislamu ndio pekee uliotabikishwa juu ya Umma wa Kiislamu kwa ukamilifu wake, waarabu na wasiokuwa waarabu, tangu alipomakinika (saw) Madina mpaka waliponyakua mabepari biladi ya Kiislamu wakaibadilisha nidhamu ya Kiislamu kuwa nidhamu ya kibepari.

Kwa hivyo Uislamu umetabikishwa kivitendo tangu mwaka wa kwanza wa hijra mpaka mwaka 1336 Hijri inaowafikiana na 1918 Miladi, wala haukutabikisha Umma wa Kiislamu zama zote hizo nidhamu yoyote isiyokuwa ya Kiislamu.

Hata kama Waislamu wamefasiri kwa lugha ya kiarabu falsafa, sayansi na thaqafa ya kigeni tofauti tofauti lakini hawakufasiri utungaji sheria au kanuni au nidhamu yoyote kutoka umma wowote, sio kwa kuitabikisha wala kuisoma. Ila kwamba Uislamu kwa sifa

yake kama nidhamu ilikuwa watu wakiitabikisha vizuri au wakiitabikisha vibaya ikifuata nguvu ya serikali au udhaifu wake na ufunuzi wa fahamu yake na kutoweka ufahamu huu, na kufuata nguvu au ulegevu wa kubeba fikra kiongozi. Kwa hivyo utabikishaji wa kimakosa uliotokea katika zama fulani ulifanya mujtama wa Kiislamu kuzorota hali inayopatikana katika kila nidhamu kwa sababu utabikishaji wake hutegemea wanadamu. Lakini utabikishaji mbaya haumaanishi kuwa Uislamu haukutabikishwa bali hakika ni kuwa Uislamu ulitabikishwa na wala hakuna chengine kilicho tabikishwa miongoni mwa mifumo na nidhamu. Kwa sababu, la muhimu katika utabikishaji ni kanuni na nidhamu ambazo serikali inaamuru zitekelezwe, na wala haikuchukuwa serikali ya Kiislamu chochote katika hayo kutoka kokote tofauti na Uislamu. Kilichotokea tu ni utabikishaji wa kimakosa wa baadhi ya nidhamu zake kutoka kwa baadhi ya watawala. Kitu ambacho chapasa kuwa wazi ni kuwa ni wajibu pindi tunaporejelea kutabikishwa kwa Uislamu kitarekhe ni lazima tufahamu mambo mawili.

Ama la kwanza, tusichukue tarekhe kutoka kwa maadui wa Uislamu walio na chuki nao, na tuichukue baada ya kuihakikisha kimakini kutoka kwa Waislamu wenyewe ili tusichukuwe sura iliyogeuzwa. Na jambo la pili ni kuwa haijuzu kutumia qiyasi ya kijumla kwa mujtama mzima kwa sababu ya tarekhe ya watu binafsi, na wala katika tarekhe ya sehemu katika mujtama. Kwa mfano ni makosa kuchukua zama za Umawiyya kutoka tarekhe ya Yazid wala kuchukuwa tarekhe ya zama za Abasiyya kutoka kwa baadhi ya matukio ya ma-Khalifah wake. Hivyo hivyo haijuzu kuhukumu juu ya mujtama wa zama ya Abasiyya kutokana na kusoma vitabu vya nyimbo vilivyotungwa juu ya habari za wapuuzi, washairi na watunzi au kutoka kusoma kitabu cha usufi na mfano wake kisha tuhukumu kuwa zama hizo ni zama za ufasiki na uovu au zama za kuipa nyongo dunia na kujitenga. Bali yatupasa kuuchukuwa mujtama kwa ukamilifu wake. Wala haikuandikwa tarekhe ya mujtama wa Kiislamu katika zama zozote, na kilichoandikwa ni habari za watawala na baadhi ya watendaji, na walioandika hayo wengi si watu wa kutegemewa. Hao ima ni wapakaji matope au wapambaji, wala hayakubaliwi waliyoyaandika, bila kuyachuja.

Pindi tunapousoma mujtama wa Kiislamu kwa msingi huu, yaani kuusoma kwa kila upande na kwa uchunguzi wa kimakini, tutaukuta kuwa ni mujtama bora kwa sababu ulikuwa hivi katika karne ya kwanza na ya pili na ya tatu kisha karne zilizobakia mpaka katikati mwa karne ya kumi na mbili hijriya. Na tutaukuta kuwa Uislamu umetabakishwa katika zama zote hata mpaka mwishoni mwa serikali ya Uthmaniyya kwa sifa yake kama serikali ya Kiislamu. Na pia ni lazima tufahamu kuwa haijuzu kuchukuliwa tarekhe kama chimbuko la nidhamu na fiqhi, bali nidhamu huchukuliwa kutoka machimbuko yake ya kifiqhi na sio tarekhe, kwa sababu tarekhe sio chimbuko lake. Pindi tunapotaka kufahamu ukomunisti hatuuchukuwi kutoka tarekhe ya Urusi bali tutauchukuwa kutoka vitabu vya mfumo wa kikomunisti vyenyewe. Na pindi tunapotaka kujua maarifa ya fiqhi ya kiingereza, hatuichukuwi kutoka tarekhe ya Uingereza bali tutaichukuwa kutoka fiqhi ya kiingereza. Na hivi ndivyo hupimwa nidhamu au kanuni yoyote.

Uislamu ni mfumo ulio na aqida na nidhamu. Pindi tunapotaka kuujua na kuuchukuwa, haitujuzu katu kuchukuwa tarekhe kama chimbuko lake, sio katika kuujua wala katika upande wa kuchukuwa ahkamu zake.

Ama katika chimbuko la kuujuwa, nalo ni vitabu vya fiqhi za Kiislamu. Ama katika upande wa chimbuko la kuchukuwa ahkamu zake, nazo ni dalili zake fafanuzi. Kwa hivyo si sahihi kuchukuwa tarekhe kama chimbuko la nidhamu ya Kiislamu, sio katika kuufahamu wala kuistinbat. Basi si sawa kufanywa tarekhe ya Umar bin al-Khattab au Umar bin Abdulaziz au Harun Ar-Rashid au wengineyo kuwa ni chimbuko la hukmu za

kiShari'ah, sio katika matukio ya kitarekhe yaliyopokelewa kutoka kwao na sio katika vitabu vilivyo tungwa juu ya tarekhe zao. Pindi inapofuatwa rai ya Umar katika tukio, hufuatwa kwa sifa yake kama hukmu ya Shari'ah iliyochukuliwa na Umar na akaitabakisha, kama inavyofuatwa hukmu iliyochukuliwa na Abu Hanifa na Shafii na Ja'afar na mfano wao, wala haifuatwi kwa sifa yake kama tukio la kitarekhe. Kwa hivyo tarekhe haina athari yoyote katika kuchukuliwa nidhamu wala kujulikana kwake, na kujulikana kama nidhamu imetabikishwa au la, pia haichukuliwi kutoka tarekhe bali huchukuliwa kutoka fiqhi kwa sababu zama zote katika zama kulikuwepo na matatizo yake, na yalikuwa matatizo haya yakitatuliwa na nidhamu. Ili kujuwa ni nidhamu gani iliyokuwa ikitatua matatizo, haturejelei matukio ya kitarekhe kwa sababu tarekhe hutunukulia habari tu. Bali inatupasa turudi katika nidhamu iliyokuwa ikitabikishwa, nayo ni fiqhi ya Kiislamu. Kwa kuirudia tutakuta kuwa Waislamu hawakuchukua nidhamu kutoka kwa wengine na wala Waislamu hawakujichagulia nidhamu kutokana na nafsi zao, bali tutakuta zote ni ahkamu za kiShari'ah zilizochukuliwa kutokana na dalili za kiShari'ah. Na Waislamu walikuwa na hamu kubwa katika kuisafisha fiqhi kutokana na misemo dhaifu-yaani zilizochukuliwa kidhaifu-mpaka wakakataza kutenda (kwa mujibu wa) kauli dhaifu hata kama imetokana na mujtahid mutlaq.

Kwa hivyo haipatikani hata dalili moja ya kiShari'ah isiyotokana na fiqhi ya Kiislamu katika ulimwengu wote wa Kiislamu, bali kilichoko ni fiqhi ya Kiislamu pekee. Na kuwepo dalili za kifiqhi pekee katika Umma bila kuwepo dalili nyengine ni dalili ya kuwa Umma haukutumia katika Shari'ah yake dalili tofauti na hizi.

Ikiwa yajuzu kuangalia tarekhe, huangaliwa jinsi ilivyo tabikishwa. Humkinika kutaja tarekhe matukio ya kisiasa na utaona ndani yake jinsi ilivyo tabikishwa. Isipokuwa hiyo pia haijuzu kuichukuwa ila baada ya kuihakikisha kwa makini kutoka kwa Waislamu. Tarekhe (historia) ina machimbuko matatu. La kwanza ni vitabu vya tarekhe, na la pili ni athari na la tatu ni riwaya. Ama vitabu haijuzu kuchukuliwa katu kama chimbuko, hilo ni kwa sababu zama zote zimeathiriwa na dhurufu za kisiasa, na zilikuwa zikijazwa urongo ima kumuunga mkono yule aliyeandikwa katika uhai wake au imeandikwa dhidi ya yule aliyeandikwa katika wakati wa mwengine. Dalili ya karibu ni juu ya tarekhe ya familia ya Alawiyya katika Misri. Kabla ya mwaka 1952 ilikuwa na sura ya kun'gara, na baada ya mwaka 1952 ilibadilika tarekhe hiyo kuwa sura mbaya kinyume na ile iliyokuwa kabla. Na mfano wa hilo ni tarekhe ya matukio ya kisiasa katika zama zetu na kabla yake. Kwa hivyo haijuzu kuchukuwa vitabu vya tarekhe kuwa ni chimbuko la tarekhe, hata kama ni vitabu vya maisha binafsi walivyoviandika wenyewe.

Ama athari za kale, uhakika wake ni kuwa pindi inaposomwa kwa usafi wake hutoa uhakika wa tarekhe juu ya kitu hata kama haileti mfuatano wa tarekhe, lakini hujulisha kwa kutokea baadhi ya matukio. Na atakae fuatilia athari za kale za Waislamu katika biladi zao sawa sawa ziwe katika majengo yao au vifaa vyao au kitu chochote kinacho chukuliwa kama athari ya kale ya kitarekhe, hujulisha kwa dalili ya yakini kuwa hakuna kitu kilichokuwepo katika ulimwengu wote wa Kiislamu ila Uislamu na nidhamu ya Kiislamu na hukmu za Kiislamu. Na yalikuwa maisha ya Waislamu, uhai wao na miondoko yao yote si mengine ila ni ya Kiislamu.

Ama chimbuko la tatu nalo ni upokezi (*riwaya*), nalo ni miongoni mwa machimbuko sahihi ambayo hutegemewa ikiwa upokezi ni sahihi na ikifuatwa katika upokezi njia inayotumiwa katika upokezi wa hadithi. Na kwa mbinu hii huandikwa tarekhe. Kwa hivyo utakuta Waislamu pindi walipoanza kuandika vitabu walifuata njia ya upokezi. Kwa haya tutakuta vitabu vya tarekhe ya kale kama tarekhe ya At-Tabari, sira ya ibn Hisham na mifano yake vimetungwa juu ya mbinu hii. Na juu ya haya haijuzu kwa Waislamu

kuwafundisha watoto wao tarekhe kutokana na vitabu vilivyotungwa ambavyo machimbuko yao ni vitabu vyenzake. Hivyo hivyo haijuzu kulinganisha utabikishaji wa nidhamu ya Kiislamu kutoka tarekhe kama hii. Kwa hilo hubainika kuwa Uislamu ndio pekee uliotabikishwa juu ya Umma wa Kiislamu na wala hakuna jengine lililotabikishwa katika zama zote.

Isipokuwa tangu vilipokwisha vita vikuu vya kwanza vya ulimwengu na kushinda muungano wa kimagharibi, na akatangaza Lord Allenby—kiongozi wa kampeni—pindi alipoiteka Bait Al-Maqdis: ‘Leo vimekwisha vita vya msalaba’, kutoka wakati huo mpaka leo makafiri wakoloni wametabikisha juu yetu nidhamu ya kibepari katika mambo yote maishani ili ushindi waliopata juu yetu ubakie milele. Kwa hivyo hakuna budi ila kuibadilisha nidhamu hii fisidifu iliyooza ambayo kupitia kwake wameweza wakoloni kumakinika katika biladi zetu, na hakuna budi ila kuin’goa kutoka mizizi yake kikamilifu kijumla na kivipande mpaka tuweze kurudisha maisha ya Kiislamu.

Ni katika fikra duni kuweka nidhamu aina yoyote badala ya nidhamu hii, na miongoni mwa fikra finyu ni kudhani kuwa Umma unapotabikisha nidhamu peke yake bila aqida yake itaiokoa, bali hakuna budi mwanzo kwa Umma kukubali aqida kisha kutabikisha nidhamu inayotokamana na aqida hiyo. Wakati huo huwa utabikishaji wa nidhamu na kukubali aqida huwa yenye kuokoa. Hii huhusu Umma uliosimama juu ya mfumo na ambao serikali yake imesimama juu ya msingi huu. Amma kuhusu watu na umma nyenginezo, si dharura kuamini mfumo unao tabikishwa juu yake bali ni juu ya Umma unaoukubali mfumo na kuubeba kuutabikisha juu ya watu na uumma wowote hata kama hawaja uamini mfumo kwa sababu litawaendeleza pia na litawavutia kuuamini. Kuuamini mfumo sio sharti juu ya yule anayetabikishwa juu yake mfumo bali kuamini mfumo ni sharti ya kimsingi kwa yule anayetabikisha.

Miongoni mwa hatari ni sisi (Waislamu) kuchukua uzalendo na nidhamu ya kikomunisti kwa sababu haichukuliwi ikitenganishwa na fikra yake ya kimada kwa sababu haitozaa natija yeyote na athari yoyote. Na wala haichukuliwi pamoja na fikra yake ya kimada kwa sababu ni fikra ya kombo inayo gongana na umbile la mwanadamu na hulazimisha Umma wa Kiislamu kuwacha aqida ya Kiislamu. Wala haijuzu sisi kuchukuwa ujamaa na kuhifadhi upande wa kiroho wa Kiislamu kwa sababu tutakuwa hatukuchukua Uislamu wala ujamaa kwasababu ya mgongano wao na upungufu katika kilichochukuliwa. Wala haijuzu kuchukua nidhamu ya Kiislamu na kuwacha aqeeda yake iliyozaa nidhamu yake kwa sababu tutakuwa tumechukua nidhamu iliyokufa isiyokuwa na roho ndani yake. Bali hakuna budi ila tuchukuwe Uislamu kikamilifu kwa aqida yake na nidhamu zake, na tubebe uongozi wake wa kifikra pindi tunapobeba ulinganizi wake.

Njia ya mwamko wetu ni njia moja, nayo ni kurudisha maisha ya Kiislamu na hakuna njia ya kurudisha maisha ya Kiislamu ila kupitia serikali ya Kiislamu. Na hakuna njia ya kufikia hilo ila tukichukuwa Uislamu kwa ukamilifu—tuuchukue kama aqida inayotatua tatizo kubwa na inayolekeza mtazamo maishani, na nidhamu iliyozaliwa na aqida hii. Msingi wake ni kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna ya Mtume, na utajiri wa thaqafa yake ni thaqafa ya Kiislamu na kilichomo ndani yake miongoni mwa fiqhi, hadithi, tafsiri, lugha na vyenginevyo. Na wala hakuna njia ya kufikia hilo ila katika kuibeba fikra kiongozi ya Kiislamu ubebaji kamili kwa ulinganizi wa Uislamu. Na kurudisha Uislamu kikamilifu kila mahali mpaka utakapo hama ubebaji wa fikra kiongozi kwa Umma kwa ujumla wake na kwa serikali ya Kiislamu, kisha tubebe fikra kiongozi kwa ulimwengu.

Hii ndio njia ya kipekee ya mwamko—kubeba fikra kiongozi ya Kiislamu kwa Waislamu ili kurudisha maisha ya Kiislamu, kisha kuubeba kwa watu wote kupitia njia ya serikali ya Kiislamu.

### 4. NAMNA YA KUBEBA ULINGANIZI WA KIISLAMU.

Hawakurudi nyuma Waislamu katika kuongoza ulimwengu kwa sababu ya kushikamana na dini yao. Bali kulianza kurudi kwao nyuma siku walipoacha mshikamano huu na wakaudharau, na wakaruhusu hadhara ngeni kuingia katika miji yao na ufahamu wa kimagharibi ukaingia akilini mwao. Siku walipo wachana na uongozi wa kifikra wa Kiislamu pindi walipolemaa katika ulinganizi wake na kutabikisha kimakosa hukmu zake. Basi hapana budi ila warejeshe maisha ya Kiislamu ili wapate fursa ya kuwa na mwamko. Na hayatarudi maisha haya ya Kiislamu ila watakapo beba ulinganizi wa Kiislamu kwa kuubeba uongozi wa kifikra wa Kiislamu na kwa ulinganizi huo wabuni serikali ya Kiislamu itakayobeba uongozi wa kifikra kwa kubeba ulinganizi (*da'wa*) wa Kiislamu.

Yapasa iwe wazi kwetu kuwa kubeba uongozi wa kifikra kwa kubeba ulinganizi wa Kiislamu ni kwa sababu ya kuwainua Waislamu, kwa sababu Uislamu ndio pekee utakao tengeneza ulimwengu. Na kwa sababu mwamko wa kikweli haupatikani ila kupitia kwake sawa sawa iwe kwa Waislamu au kwa wengineyo. Na juu ya msingi huu yapasa kubebwa ulinganizi wa Kiislamu.

Yapasa kuwa na uangalifu katika kubeba ulinganizi huu kama uongozi wa kifikra kwa ulimwengu unaozaa kutokamana nayo nidhamu. Na juu ya uongozi huu wa kifikra hujengwa fikra zote, na kutokana na fikra hizi hutokamana ufahamu wote unao athiri mtazamo maishani bila kubagua (chochote).

Unabebwa ulinganizi wa Kiislamu leo kama ulivyo bebwa zamani, na utakwenda mwenendo wa kuigizwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) katika ukamilifu wake na vipande vyake bila ya kukengeuka hata kwa kadiri ya unywele katika njia (*twariqa*) *hiyo*, na bila kujali ikhtilafu za zama. Hii ni kwa sababu kilicho tofautika ni mbinu (*waseela*) na sura lakini asili na maana hayo hayatofautiki wala hayawezi kabisa kutofautika kadiri zinapopishana zama na kutofautika watu na biladi.

Kwa hivyo kubeba ulinganizi wa Kiislamu hulazimisha uwazi, ushujaa, nguvu na fikra, na kupinga kila kinacho khalifu fikra na twarika na kuikabili ili kudhihirisha ubatili wake bila kujali natija na hali itakayo tokea.

Kubeba ulinganizi wa Kiislamu hulazimisha kuwa ubwana wote uwe ni kwa mfumo wa Kiislamu bila kujali kama huafikiana na jumla ya watu au huwakhalifu, au hufuatana na ada zao au hugongana nazo au watu watakubaliana nao au watakataa na kuupinga. Mbebaji ulinganizi hata wapumbaza watu au kuwapaka mafuta, wala hatojipendekeza kwa walio na uongozi wala hatowasifu. Wala hatoshughulika na ada za watu na mila zao, na wala hajali kama watu watamkubali au kumpinga bali ana shikamana na mfumo peke yake na ana utangaza mfumo peke yake bila kuingiza katika mipango yake chochote kisicho kuwa mfumo. Na wala hawaambiwi wenye mifumo mengine, 'Shikeni mifumo yenu' bali hulinganiwa bila kulazimishwa kwa mfumo ili wauamini. Hii ni kwa sababu ulinganizi hulazimisha kusiwe na chengine kisichokua mfumo na uwe ubwana ni kwa mfumo pekee.

**{ هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَى وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ }**

"*Yeye ndiye aliyemtuma Mtume wake na uongofu na dini ya haki ili idhihirike juu ya dini zote hata kama washirika wanachukizwa*" [TMQ 9:33].

Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) alikuja ulimwenguni na ujumbe wake akipingana na akiwa muwazi, mwenye kuamini yale anayo yalingania na akipingana na dunia nzima, akitangaza vita dhidi ya mwekundu na mweusi katika watu, bila kujali ada na mila au dini au aqida au watawala au wanao tawaliwa. Wala hakuangalia kitu chochote ila ujumbe wa Uislamu. Alianza na makureshi kwa kutaja miungu yao na kuwaaibisha, na akapambana nao katika itikadi zao na kuzisafihi, ilhali yeye ni mpweke aliyetengwa pasina uweza wala msaidizi wala silaha isipokuwa imani thabiti kwa Uislamu anaoulingania. Wala hakushughulika na ada na mila za waarabu wala dini zao na itikadi zao wala hakuwapamba juu yake wala hakuzichunga kwa chochote.

Hivyo hivyo huwa mbebaji ulinganizi wa Kiislamu ni mwenye kupambana wazi wazi na kila kitu—hupambana na ada na mitindo na fikra kombo na fahamu za kimakosa. Hupambana na rai ya aghalabu ya watu (*rai aam)* ikiwa ni ya ki-makosa hata wakipinga kwa yeye kupambana nayo, hupambana na aqida na dini hata akikumbwa na ushupavu wa waumini wake na uadui wa waliokita kwa upotevu wake (aqida na dini hizo).

Ubebaji ulinganizi wa Uislamu hulazimisha pupa katika kutekeleza hukmu za Kiislamu utekelezaji uliokamilika na pasina kwenda kinyume juu ya kitu chochote namna kitakavyo kuwa kidogo. Mbebaji ulinganizi hakubali kuzuia, makubaliano, utepetevu au kuakhirisha bali huchukua mambo kikamilifu na hufanya haraka kufikia malengo na wala wala hakubaliaji muingiliaji kati kuja kuficha haki. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) alikataa matakwa ya ujumbe wa Thaqif kuwabakishia bila kuvunja sanamu wao *laata* kwa miaka mitatu na awasamehe kuswali kama masharti ya kusilimu kwao. Wala hakukubali kuwacha sanamu *laata* miaka miwili au miezi kama walivyo omba bali alikataa kata kata. Na kulikuwa kukataa kwake thabiti bila kurudi nyuma na kuwa na huruma kwa sababu mwanadamu ni ima muumini au si muumini na kwa kuwa malipo ni ima pepo au moto. Lakini yeye (saw) aliwakubalia wasivunje wao sanamu la *laata* na akawawakilishia Abu Sufyan na Mughira bin Shu'ba kulivunja. Ndio hakukubali ila aqida iliyo kamilika na utekelezaji unao ambatana nayo. Ama mbinu na sura aliyakubali hayo kwa sababu hayo hayahusiki na hakika ya aqida. Kwa hivyo hakuna budi kwa ulinganizi wa Uislamu kuwa na pupa na utendaji ulio kamilika bila kupuuza fikra au twarika wala haidhuru kutumia mbinu inayohitajika.

Ni wajibu kwa mbebaji ulinganizi wa Kiislamu kuwa kila kitendo miongoni mwa vitendo vyake kuwa kwa lengo maalumu na yampasa mbebaji ulinganizi daima kulenga lengo hilo na daima kufanya bidii kulifikia na hapumziki na huhangaika juu chini ili kulihakikisha lengo. Kwa hivyo utamkuta kuwa haridhiki kwa fikra pekee bila vitendo huona hilo kuwa ni falsafa inayowazwa, wala haridhiki kwa fikra na vitendo bila lengo huona hili kuwa ni harakati za parafujo zitakazo malizika kwa kuganda (*jumud*) na kukata tamaa bali hudumu katika kuunganisha fikra na kitendo. Na katika kujaalia fikra na kitendo pamoja kwa ajili ya lengo litakalo hakikishwa kivitendo na kudhihirishwa kutokea kwake. Mtume (saw) alibeba uongozi wa kifikra Makka mpaka alipoona mujtama wa Makka hautohakikisha kuufanya Uislamu kama nidhamu ya mujtama ya kutendwa, alitayarisha mujtama wa Madina kisha akabuni serikali, akatabikisha (akatekeleza) Uislamu na kubeba ujumbe wake. Na akatayarisha Umma kuubeba baada yake na kwenda katika njia aliyowachorea. Kwa hivyo hakuna budi kuwa ubebaji da'wa ya Uislamu katika hali ya kukosekana Khalifah wa Waislamu wote kuwa ulinganizi wa Uislamu na kurejesha maisha ya Kiislamu kwa kufanya kazi kusimamisha serikali ya Kiislamu itakayo tabikisha Uislamu na kubeba ujumbe wake kwa ulimwengu. Utaondoka ulinganizi wa kurejesha maisha ya Kiislamu katika Umma ili serikali ibebe da'wa kwa ulimwengu, na kutoka da'wa ya kimahali katika ulimwengu wa Kiislamu mpaka ulinganizi wa kiulimwengu.

Ulinganizi kwa Uislamu hauna budi ila kudhihirika ndani yake aqida sahihi na kutilia nguvu mafungamano kwa Mwenyezi Mungu na kuwabainishia watu tatuo la matatizo yao mpaka upatikane katika ulinganizi huu uhai katika kila pembe ya maisha. Mtume (saw) alikuwa akiwasomea watu Makka:

{ تَبَّتْ يَدَا أَبِي لَهَبٍ وَتَبَّ }

"*Imeangamia mikono ya Abu Lahab na ameangamia mwenyewe*" [TMQ 111:1]

Na akiwasomea wakati huo huo:

{ إِنَّهُ لَقَوْلُ رَسُولٍ كَرِيمٍ - وَمَا هُوَ بِقَوْلِ شَاعِرٍ قَلِيلاً مَا تُؤْمِنُونَ }

"*Kwa hakika hii ni kauli iliyoletwa na Mjumbe mwenye heshima. Wala si kauli ya mshairi. Ni machache mnayoamini*" [TMQ 69:40-41].

Na akawasomea Makka:

{ وَيْلٌ لِلْمُطَفِّفِينَ- الَّذِينَ إِذَا اكْتَالُوا عَلَى النَّاسِ يَسْتَوْفُونَ - وَإِذَا كَالُوهُمْ أَوْ وَزَنُوهُمْ يُخْسِرُونَ }

"*Maangimizo yatawa thibitikia wapunjao wenziwao.Ambao wanapo jipimia kwa watu hupokea kipimo kamili.Lakini wanapo wapimia kwa vibaba au mizani hupunguza*" [TMQ 83:1-3]

Na akawasomea:

{ إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَهُمْ جَنَّاتٌ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الأَنْهَارُ ذَلِكَ الْفَوْزُ الْكَبِير }

"*Hakika wale walioamini na kutenda vitendo vyema bila shaka watapata mabustani yenye mito ipitayo mbele yake.Huku ndio kufuzu kukubwa*" [TMQ 85:11].

Na akawasomea Madina:

{ وَأَقِيمُوا الصَّلاَةَ وَآتُوا الزَّكَاةَ }

"*Simamisheni swala na toeni zaka*"[TMQ 2:110].

Pia aliwasomea:

{ انفِرُوا خِفَافًا وَثِقَالاً وَجَاهِدُوا بِأَمْوَالِكُمْ وَأَنفُسِكُمْ فِي سَبِيلِ اللهِ }

"*Nendeni (vitani) mukiwa wepesi au wazito na piganeni na mali zenu na nafsi zenu katika njia ya Allah*" [TMQ 9:41].

Na akiwasomea:

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِذَا تَدَايَنْتُمْ بِدَيْنٍ إِلَى أَجَلٍ مُسَمًّى فَاكْتُبُوهُ }

"*Enyi mlioamini, mnapo kopesha deni kwa muda uliyotajwa liandikeni*" [TMQ 2:282].

Na akawasomea:

{ لاَ يَسْتَوِي أَصْحَابُ النَّارِ وَأَصْحَابُ الْجَنَّةِ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ هُمْ الْفَائِزُونَ }

*"Hawawi sawa watu wa motoni na watu wa peponi Watu wa peponi ndio wenye kufuzu*" [TMQ 59:20].

Kwa hivyo hakuna budi kwa ulinganizi wa Kiislamu kuwabebea watu nidhamu ambazo zitakazo tatua matatizo yao maishani kwa sababu siri ya kufaulu ulinganizi wa Kiislamu ni kuwa uhai wake katika kutatua matatizo ya mwanadamu kama mwanadamu na kuleta ndani yake mwanadamu mapinduzi ya kijumla.

Wala haiwezekani kwa wabebaji da'wa hii kutekeleza majukumu na kusimamia kazi ila itakapo pandwa katika nafsi zao msukumo kwa ukamilifu. Na wawe daima wakitafuta uhakika na kurudia daima yote wanayo yajua mpaka wasafishe yote yanayo ambatana nayo yalio mageni nayo, na waweke mbali na wao kila (kigeni) ambacho wakikurubiana

nacho kuna uwezekano kushikana na yeye. Mpaka ziwe fikra walizo zibeba ni wazi na safi. Usafi wa fikra na uwazi wake ndio dhamana ya kipekee ya kufaulu na kuendelea kufaulu.

Kisha ni juu ya wabebaji da'wa kutekeleza wajibu wao kama wajibu walio wajibishwa nao na Mwenyezi Mungu, na wauitikie ilhali wafurahi na wakiwa na bishara ya radhi za Mwenyezi Mungu. Na wasitaraji malipo kutoka vitendo vyao wala shukrani kutoka kwa watu wala wasijue ila kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu.

## 5. HADHARA YA KIISLAMU

Kuna tofauti baina ya hadhara na madaniyya. Hadhara ni mkusanyiko wa fahamu juu ya maisha, na madaniyya ni umbo la kimada la vitu vinavyoshikika ambavyo hutumiwa katika mambo ya maisha. Hadhara huwa ni maalum kwa mujibu wa mtazamo maishani na huwa madaniyya ni maalum na jumla. Umbo la kimadaniyya liliozaliwa na hadhara kama masanamu ni hadhara maalum, na umbo la kimadiniyya liliozaliwa na sayansi na maendeleo yake, na usanii na kuendelea kwake ni madaniyya jumla wala haihusiki na umma wowote miongoni mwa umma bali huwa ni ya kiulimwengu kama sanaa na sayansi.

Tofauti hii baina ya hadhara na madaniyya ni lazima daima izingatiwe. Pia ni lazima izingatiwe tofauti baina ya umbo la kimadaniyya linalotokana na hadhara na baina ya umbo la kimadiniyya linalotokana na sayansi na sanaa. Hilo huzingatiwa wakati wa kuchukuwa madaniyya tofauti katika umbo lake, na kuitofautisha baina yake na baina ya hadhara. Ama madaniyya ya kimagharibi inayotokana na sayansi na sanaa, hakuna kinachozuia kuchukuliwa kwake. Ama madaniyya ya kimagharibi inayotokamana na hadhara ya kimagharibi, haijuzu kuchukuliwa kwa hali yoyote kwa sababu haijuzu kuchukuwa hadhara ya kimagharibi kwa sababu ya mgongano wake na hadhara ya Kiislamu katika msingi uliosimama juu yake na mtazamo juu ya maisha duniani na katika maana ya kufikia mafanikio na furaha (*sa'ada*) kwa mwanadamu.

Ama hadhara ya kimagharibi, imesimama juu ya msingi wa kutenganisha dini na maisha, na kukanusha kuwa dini ina athari maishani. Natija ya hilo ni fikra ya kutenganisha dini na serikali kwa sababu huwa ni kawaida kwa yule anaye tenganisha dini na maisha na kukanusha kuwepo dini maishani. Na juu ya msingi huu husimamishwa maisha na kusimama nidhamu ya kimaisha. Ama mtazamo wa maisha, hilo ni manufaa kwa sababu hicho ndicho kipimo cha vitendo. Kwa hivyo imekuwa manufaa ndiyo iliyosimama juu yake nidhamu na kusimama juu yake hadhara. Ndipo kutoka haya manufaa huwa ufahamu unao dhihirika wazi katika nidhamu kwa sababu huyaona maisha kuwa ni manufaa. Kwa hivyo huwa kufikia furaha kwao (*sa'ada*) ni kumpa mwanadamu kiasi kikubwa cha starehe za kimwili na kuzidisha sababu zake kwake. Kwa haya imekuwa hadhara ya kimagharibi ni hadhara ya kimanufaa wazi wazi na haipi uzito wowote kwa kitu chochote kisichokuwa manufaa wala haitambui ila manufaa na hukifanya ndicho kipimo cha vitendo. Ama upande wa kiroho, huu ni wa kibinafsi wala hauhusu jamii, na hufungika katika kanisa na watu wa kanisa. Kwa hivyo haipatikani katika hadhara ya kimagharibi thamani ya kiakhlaqi au uroho au utu; kinachopatikana ni thamani ya kimada na manufaa pekee. Juu ya msingi huu imefanya vitendo vya kiutu kutekelezwa na vyama vilivyotengwa na serikali kama shirika la msalaba mwekundu na mishinari, na imetengwa na maisha kila thamani ila thamani ya mada nayo ni faida. Imekuwa hadhara ya ki-magharibi ndio mkusanyiko huu wa ufahamu juu ya maisha.

Ama hadhara ya Kiislamu, uhakika wake umesimama juu ya msingo ulio kinyume na msingi wa hadhara ya kimagharibi, mtazamo wake maishani sio mtazamo wa hadhara ya kimagharibi juu yake, na maana yake ya furaha hukhtalifiana na maana yake katika hadhara ya kimagharibi ikhtilafu ya kijumla. Hadhara ya Kiislamu imesimama juu ya msingi wa imani kwa Mwenyezi Mungu, na kuwa yeye ndiye aliyejaalia ulimwengu, mwanadamu na uhai nidhamu inayotembea kwa mujibu wake, na kuwa yeye ndiye aliyemtumia bwana Muhammad (saw) na dini ya Uislamu. Maana yake ni kuwa hadhara ya Kiislamu husimama juu ya msingi wa aqida ya Kiislamu nayo ni imani kwa Mwenyezi Mungu, malaika wake, vitabu vyake, mitume wake, Siku ya Mwisho na *al-qadhaa wa al-qadar* kheri yake na shari yake hutoka kwa Mwenyezi Mungu. Imekuwa aqida ndio msingi wa hadhara nayo imesimama juu ya msingi wa kiroho.

Amma mtazamo wa maisha katika hadhara ya Kiislamu umekitwa katika falsafa ya Uislamu ambayo imechimbuka kutoka aqida ya Kiislamu, na ambayo husimama juu yake maisha na vitendo vya mwanadamu maishani. Falsafa hii ambayo huunganisha mada na roho, yaani hufanya vitendo vipelekwe kwa mujibu wa maamrisho na makatazo ya Mwenyezi Mungu, ndio msingi wa mtazamo maishani. Vitendo vya mwanadamu ni mada na kutambua kwa mwanadamu fungamano lake na Mwenyezi Mungu pindi anapotenda vitendo—kwa jinsi kuwa kitendo ni halali au haramu—ni roho. Hupatikana kwa hilo kuunganika mada na roho. Basi juu ya hayo huwa kinacho peleka vitendo vya Mwislamu ni maamrisho ya Mwenyezi Mungu na makatazo yake. Na lengo la kupeleka vitendo kwa mujibu wa maamrisho na makatazo ya Mwenyezi Mungu ni radhi za Mwenyezi Mungu na sio manufaa kata kata. Ama shabaha ya kutenda nafsi ya kitendo, nayo ni thamani anayotarajia kuipata pindi anapotenda vitendo. Thamani hii hukhtalifiana kwa vitendo tofauti tofauti. Huenda ikawa thamani ya kimada kwa anayefanya biashara kwa shabaha ya kupata faida kwa sababu biashara yake ni kitendo cha kimada na hupeleka biashara hii akitambua fungamano lake na Mwenyezi Mungu kwa mujibu wa maamrisho na makatazo yake akitafuta radhi za Mwenyezi Mungu. Na shabaha anayoitarajia kupata katika kutenda kitendo hicho ni faida nayo ni thamani ya kimada.

Na huenda ikawa thamani ya kiroho kama swala, zaka, saumu na hijja. Na huenda ikawa thamani ya kiakhlaqi kama kusema kweli, uaminifu na kutekeleza ahadi. Na huenda ikawa thamani ya kiutu kama kuokoa aliyezama na kumsaidia aliye na shida.Thamani hizi hutafutwa na mwanadamu pindi anapotenda kitendo ili azipate lakini sicho kinacho peleka vitendo na sio mfano wa juu (lengo kuu) unaolengwa bali ni thamani ya kitendo na hutofautiana kwa kutofautika aina yake.

Amma furaha, hiyo ni kufikia radhi za Mwenyezi Mungu na sio kushibisha njaa za mwanadamu kwa sababu kushibisha njaa zote za mwanadamu, kutoka njaa za mahitaji ya kiviungo na njaa za kighariza, ni jambo la lazima kuhifadhi dhati ya mwanadamu lakini si lazima kuwa kupatikana kwake kuwa na furaha. Huu ndio mtazamo wa maisha, na huu ndio msingi ambao husimama juu yake mtazamo huu, na ndio msingi wa hadhara ya Kiislamu. Na kwa hakika hugongana mgongano wa kijumla na hadhara ya kimagharibi. Hivyo hivyo umbo la kimadaniyya linalotokana nayo hugongana na umbo la kimadaniyya linalotokana na hadhara ya kimagharibi. Mfano: Picha ni umbo la kimadaniyya na hadhara ya kimagharibi huchukulia picha ya mwanamke aliye utupu inayodhihirisha fitna zake zote kuwa ni umbo la kimadaniyya linaloafikiana na ufahamu wake maishani juu ya mwanamke. Kwa hivyo mmagharibi huitambua kama kipande cha sanaa anachojifakhiri nacho kama umbo la kimadaniyya na kama kipande cha sanaa kitakapo timiza shuruti za usanii. Lakini umbo hili hugongana na hadhara ya Kiislamu na hukhtalifiana na ufahamu wake juu ya mwanamke ambaye ana heshima ambayo ni

wajibu kuhifadhiwa. Kwa hivyo hukataza picha hiyo kwa sababu huibua ghariza ya kuendeleza kizazi na hilo hupelekea kueneza mchafuko katika akhlaqi. Na mfano wa hilo pia ni pale pindi anapotaka Muislamu kujenga nyumba nayo ni umbo la kimadaniyya, yeye huchunga katika nyumba hiyo asikashifike mwanamke aliyevaa nguo khafifu kwa aliye nje ya nyumba, basi hujenga pembezoni mwake ukuta. Kinyume na mmagharibi, yeye hajali hayo kwa sababu ya hadhara yake. Kwa hivyo vyote vinavyotokana na umbo la ki-madaniyya vinavyotokana na hadhara ya ki-magharibi kama masanamu na mfano wake. Na pia mavazi ikiwa ni khasa kwa makafiri kwa kuwa kwao makafiri haijuzu kwa Waislamu kuyavaa kwa sababu hubeba mtazamo maalumu. Na ikiwa si hivyo kwa kuwa haitambulishi kama makafiri bali wanayachukuwa kwa haja au mapambo basi wakati huo huwa ni umbo la kimadaniyya jumla na yajuzu kuyatumia.

Amma umbo la kimadaniyya linalotokana na natija ya sayansi au sanaa kama vyombo vya maabara na vifaa vya matibabu na sanaa na vyombo vinavyo shabihiana navyo vyote ni maumbo ya kimadaniyya ya kiulimwengu haikatazwi kuchukua chochote kati yao kwa sababu havitokani na hadhara maalumu wala havina fungamano nayo.

Mtazamo wa haraka kwa hadhara ya kimagharibi ambayo leo imetawala ulimwengu unatuonyesha kwamba hadhara ya kimagharibi haiwezi kumdhaminia mwanadamu utulivu bali imekuwa kinyume cha hilo. Imesababisha tabu ambayo ulimwengu waumia kwa miba yake na kuteketea kwa moto wake. Na hadhara ambayo imefanya msingi wake ni kutenganisha dini na maisha kinyume na maumbile ya mwanadamu na wala haipimi upande wa kiroho uzito wowote katika maisha kwa ujumla na huyatizama maisha kuwa ni ya manufaa pekee na hufanya fungamano baina ya mwanadamu na mwanadamu mwengine maishani ni la kimanufaa; hadhara hii haileti ila tabu na hofu ya daima. Madamu manufaa ni msingi basi kuzozania ni jambo la kawaida na ugomvi juu yake ni jambo la kawaida na kutegemea nguvu katika kusimamisha mafungamano ya watu ni jambo la kawaida, kwa hivyo huwa ubepari ni jambo la kawaida kwa watu wa hadhara hii. Na huwa akhlaqi zinalegalega kwa sababu manufaa pekee ndio msingi maishani. Na kwa haya ni jambo la kawaida kutenganisha akhlaqi njema na maisha kama ilivyotengwa thamani ya kiroho. Na husimama maisha juu ya msingi wa kuzozana, ugomvi, uadui na ukoloni. Na hiyo ndiyo hali ya ulimwengu leo. Kuwepo pia mzozo wa kiroho katika mioyo ya binadanu, na hofu ya kudumu na shari iliyoenea, hayo ni dalili wazi ya mazao ya hadhara hii ya kimagharibi kwani ndiyo inayo tawala ulimwengu. Ndio sababu iliyo sababisha natija hii ya hatari na kuwahatarisha wanadamu.

Na tukitizama hadhara ya Kiislamu iliyotawala ulimwengu tangu karne ya saba miladiyya mpaka mwisho wa karne ya kumi na nane Miladi, imetuonyesha kuwa haikuwa na sera ya kikoloni. Na ukoloni si katika maumbile yake kwa sababu haikutofautisha baina ya Waislamu na wengineo ili dhamini uadilifu kwa watu wote walio nyenyekea chini yake muda wote wa utawala wake. Kwa sababu hadhara yake imesimama juu ya msingi wa kiroho ambao huhakikisha thamani zake za kimada, kiroho, akhlaqi na utu. Na imeweka uzito wake maishani juu ya aqida. Na hutizama maisha kuwa ni yenye kupelekwa kwa mujibu wa maamrisho ya Mwenyezi Mungu na makatazo yake, na ikafanya maana ya furaha (*sa'ada*) ni radhi za Mwenyezi Mungu. Na wakati itakapo tawala hadhara ya Kiislamu kama ilivyo tawala siku za nyuma basi yatosha kutatua mizozo yote ulimwenguni na itadhamini maendeleo ya wanadamu wote.

## 6. NIDHAMU YA KIISLAMU

Uislamu ndio dini ambayo aliyoishusha Mwenyezi Mungu kwa bwana Muhammad (saw) ili kupanga mahusiano ya mwanadamu na muumba wake, na nafsi yake na wengineo miongoni mwa wanadamu. Na mahusiano ya mwanadamu na muumba wake

hujumuisha aqida  na ibadati, na mahusiano yake na nafsi yake hujumuisha akhlaqi, vilaji, vinywaji na mavazi, na mahusiano yake na wengineo miongoni mwa wanadamu hujumuisha muamalati na nidhamu za kuadhibu wahalifu. Uislamu ni mfumo wa mambo yote maishani na sio dini ya kiroho pekee wala haina ukasisi na hakika yake hupiga vita kuwepo tabaka la kidini la kibaguzi. Hakuna katika Uislamu watu wanoitwa watu wa dini na watu wanaoitwa wa dunia. Bali wote wanaoukubali Uislamu huitwa Waislamu na wote ni sawa mbele ya dini. Hakuna katika Uislamu watu wa kiroho na watu wa kileo. Na upande wa kiroho katika Uislamu ni kuwa vitu vimeumbwa na muumba na vinapelekwa kwa amri ya muumba huyu. Kwa sababu mtazamo wa kindani juu ya ulimwengu, mwanadamu na uhai na yaliyo yazunguka na yanayo ambatana nayo na kuzitumia hizo kama dalili humuonesha mwanadamu upungufu, kushindwa na kuhitajia kunako shuhudiwa katika vitu hivi vyote kuna onyesha kwa dalili iliyo wazi kuwa vimeumba na muumba na kupelekwa kwa amri yake. Na kuwa mwanadamu anapoenda katika maisha hapana budi kwake yeye kuwa na nidhamu ya kumpangia ghariza zake na mahitaji yake ya kiviungo. Wala haimkini nidhamu hii kutoka kwa mwanadamu kwa sababu ya kushindwa kwake na kukosa katika utambuzi wake (hana utambuzi wa yote). Na kwa kuwa ufahamu wake kwa ajili ya uwekaji huu wa nidhamu huathiriwa na tofauti, ikhtilafu na mgongano mambo yanayozaa nidhamu ya mgongano inayo msababishia mwanadamu tabu. Kwa hivyo ni lazima nidhamu itoke kwa Mwenyezi Mungu, na kwa haya ni lazima kwa mwanadamu kupeleka mambo yake kwa mujibu wa nidhamu inayotoka kwa Mwenyezi Mungu. Lakini kupeleka huku mambo kwa nidhamu hii ikiwa kumejengwa juu ya sababu ya manufaa ya nidhamu hii si kwa sababu iliyojengwa kwa kuwa inatoka kutoka kwa Mwenyezi Mungu, basi haiwi ndani yake upande wa kiroho. Bali hapana budi kwa mwanadamu kupanga vitendo vyake maishani kwa mujibu wa maamrisho na makatazo ya Mwenyezi Mungu, kwa sababu ya kudiriki kwake mafungamano yake na Mwenyezi Mungu ili ipatikane roho katika vitendo, yaani hapana budi mwanadamu kufahamu fungamano lake na Mwenyezi Mungu, na kwa sababu ya kufahamu kwake fungamano hili na Mwenyezi Mungu hupeleka vitendo vyake kwa mujibu wa maamrisho na makatazo ya Mwenyezi Mungu ili ipatikane roho katika kutenda vitendo. Kwa sababu roho ni mwanadamu kudiriki fungamano lake na Mwenyezi Mungu. Na maana ya kuiunganisha (roho) na mada ni kuwepo kudiriki fungamano na Mwenyezi Mungu pindi kunapo tendwa kitendo; basi hupeleka vitendo kwa mujibu wa maamrisho ya Mwenyezi Mungu na makatazo yake kuliko jengwa juu ya kudiriki fungamano hili na Mwenyezi Mungu. Kitendo ni mada, na kudiriki fungamano na Mwenyezi Mungu pindi kinapo tendwa ni roho. Huwa kupeleka kitendo kwa mujibu wa maamrisho ya Mwenyezi Mungu na makatazo yake kuliko jengwa juu ya kudiriki fungamano hili ndio kuunganisha mada na roho. Kufikia hapa haiwi upelekaji wa asiyekuwa Muislamu vitendo vyake kwa mujibu wa hukmu za kiShari'ah zinazotokana na Qur’ani na Sunna ni upelekaji wa kiroho wala haipatikani ndani yake maana ya kuunganisha mada na roho kwa sababu yeye hajaamini Uislamu basi hadiriki fungamano na Allah. Bali amezichukua hukmu za ki-Shari'ah kama nidhamu zilizo mvutia akazitumia kupanga vitendo vyake. Kinyume na Mwislamu ambaye hutenda vitendo vyake kwa mujibu wa maamrisho ya Mwenyezi Mungu na makatazo yake akijengea juu ya kudiriki kwake kwa fungamano lake na Mwenyezi Mungu, na ikawa lengo katika kupeleka vitendo vyake kwa mujibu ya maamrisho ya Mwenyezi Mungu na makatazo yake ni radhi za Mwenyezi Mungu sio kunufaika na nidhamu pekee. Kwa sababu ya hilo hakuna budi ila kuwepo upande wa kiroho katika vitu na hakuna budi kuwepo roho pindi kunapo tendwa vitendo. Ni lazima iwe wazi daima kwa watu wote kuwa upande wa kiroho humaanisha kuwa vitu ni viumbe vilivyoumbwa na muumba yaani ni fungamano la kiumbe na muumba, na roho ni kudiriki fungamano hilo yaani kudiriki kwa mwanadamu kwa fungamano lake na Mwenyezi Mungu. Huu ndio upande

wa kiroho na hiyo ndio roho. Huu ndio ufahamu pekee ulio sahihi na kinyume chake bila shaka ni ufahamu wa makosa.

Baadhi ya dini ziliona kuwa katika ulimwengu kuna vitu vya kuhisika na vya kufichika (vya *ghaib*), na mwanadamu ana usafi wa roho na matamanio ya kimwili na kuwa uhai una upande wa kimada na upande wa kiroho. Na kinacho hisika hugongona na kinacho fichika, na usafi wa roho hauungani na matamanio ya kimwili, na kuwa mada iko kando na roho. Kwa hivyo vyote hivyo kwao wao ni pande mbili tofauti kwa sababu ya mgongano baina yao ni jambo la msingi katika maumbile yao wala havimkiniki kuunganishwa. Na kuzidi uzito kwa kimoja katika mizani ni kupungua uzito kwa chengine. Kwa hivyo ni lazima kwa kila mwenye kutaka Akhera kuzidisha katika upande wa kiroho. Kwa haya, umesimama katika ukristo utawala wa aina mbili: Utawala wa kiroho na utawala wa kidunia (‘Mpe kaisari cha kaisari na mpe mungu cha mungu’). Wakawa watu wa utawala wa kiroho ni watu wa dini na ukasisi, na wakawa wakijaribu kutia mikononi mwao utawala wa kidunia ili watawale juu yake kwa utawala wa kiroho. Kwa haya kulizuka mvutano baina ya utawala wa kidunia na utawala wa kiroho, na mwishowe ikawa watu wa dini wao wameshika utawala wa kiroho wala hawaingilii utawala wa kidunia. Ikatenganishwa dini na maisha kwa sababu ni ya kiroho (hiyo dini), na kutenganishwa baina ya dini na maisha ndio aqida ya mfumo wa kibepari na ndio msingi wa hadhara ya kimagharibi na ndio uongozi wa kifikra unao bebwa na mabepari wamagharibi kwa ulimwengu na kulinganiwa kwayo, na huufanya msingi wa thaqafa yake na hutikiswa kwa msingi huo aqida ya Waislamu juu ya Uislamu kwa sababu huupima Uislamu kwa ukristo kwa njia ya kipimo cha kijumla. Kila anaebeba ulinganizi huu—‘kutenganishwa dini na maisha’—au kutenganisha dini na serikali au na siasa, ni mfuasi na ni mwenye kuelekea katika mwelekeo wa uongozi wa kifikra wa kigeni, na ni kibaraka—awe na nia nzuri au mbaya—ni miongoni mwa vibaraka wa mabepari. Naye ama ni mjinga wa Uislamu au ana adui nao.

Ama Uislamu, huona kuwa vitu vinavyo dirikiwa na hisia ni vitu vya kimada na upande wake wa kirohi ni kuwa ni viumbe vilivyoumbwa na muumba, na roho ni kule kudiriki mwanadamu kwa fungamano lake na Mwenyezi Mungu. Kwa haya haupatikana upande wa kiroho kando na upande wa kimada, na wala haupatikani katika mwanadamu (usafi) wa kiroho na matamanio ya kimwili bali mwanadamu ana mahitaji ya kiviungo na ghariza ambazo hana budi ila kuzishibisha. Na miongoni mwa ghariza ni ghariza ya kuabudu ambayo ni kule kumhitajia muumba anayeendesha aliyesalimika na udhaifu wa kimaumbile yanayopatikana kwa mwanadamu, na kushibisha ghariza hizi hakuitwi upande wa kiroho wala upande wa kimada bali huwa ni kushibisha ghariza pekee. Isipokuwa mahitaji haya ya kiviungo na ghariza zinaposhibishwa kwa nidhamu inayotoka kwa Mwenyezi Mungu iliyojengwa juu ya kudiriki fungamano kwa Mwenyezi Mungu huwa kumepelekwa na roho, na ikiwa yameshibishwa bila nidhamu au kwa nidhamu inayo tokamana na mwengine asiyekuwa Mwenyezi Mungu huwa ni kushiba kimada kavu kavu hali inayomtia mwanadamu tabuni. Ghariza ya kuendeleza kizazi inayo shibishwa bila nidhamu au kwa nidhamu inayotoka kwa mwengine asiyekuwa Mwenyezi Mungu hilo humsababisha mwanadamu kuwa tabuni na ikiwa imeshibishwa kwa nidhamu ya ndoa inayotoka kwa Mwenyezi Mungu kuambatana na hukmu za Kiislamu hupatikana ndoa inayoleta utulivu. Na ghariza ya kuabudu ikishibishwa bila nidhamu au kwa nidhamu inayotoka kwa mwengine asiyekuwa Mwenyezi Mungu kwa kuabudu masanamu au kumuabudu mwanadamu hilo huwa ni ushirikina na ukafiri, na ikishibishwa kwa hukmu za Kiislamu hilo huwa ni ibada. Kwa hivyo ni lazima kuchungwa upande wa kiroho katika vitu na kupeleka mambo yote kwa mujibu wa maamrisho ya Mwenyezi Mungu na makatazo yake, kwa sababu ya kudiriki mwanadamu fungamano lake na Mwenyezi Mungu. Yaani kuyapeleka (mambo) kwa roho. Kwa hivyo havipatikani

katika kitendo kimoja vitu viwili bali kinacho patikana ni kitu kimoja nacho ni kitendo. Na ama kusifiwa kwake kuwa ni mada tu au ni chenye kupelekwa na roho, hilo halitokani na kitu chenyewe bali hutokana na jinsi kinavyo pelekwa kwa hukmu za Kiislamu au kutopelekwa nazo. Muislamu kumuua adui wake katika vita huchukuliwa ni jihadi na hupewa thawabu juu yake kwa sababu ametenda kwa mujibu ya hukmu za Kiislamu. Na Muislamu kuua nafsi iliyohifadhiwa (Mwislamu au si Mwislamu) bila haki huchukuliwa ni kosa linalo adhibiwa juu yake kwa sababu ni kitendo kinacho khtalifiana na maamrisho ya Mwenyezi Mungu na makatazo yake. Na vitendo vyote viwili ni kitu kimoja nayo ni mauaji yanayotokana na mwanadamu. Kuua huwa ni ibada ikiwa kumetendwa kwa mujibu wa roho na huwa ni kosa kusipotendwa kwa mujibu wa roho. Na kuunganisha mada na roho si jambo linalomkinika tu bali ni jambo ambalo ni wajibu wala haijuzu kutenganishwa mada na roho. Maana yake kitendo chochote hupelekwa kwa mujibu wa maamrisho ya Mwenyezi Mungu na makatazo yake kutokana na kudiriki fungamano na Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo ni lazima kuondoa kila kinacho wakilisha upande wa kiroho kunako tenganishwa na upande wa kimada. Hakuna cha watu wa dini katika Uislamu wala hakuna katika Uislamu utawala wa kidini kwa maana ya kikasisi. Na wala hakuna utawala wa kidunia uliotenganishwa na dini bali Uislamu ni dini na serikali hutokana nayo (hiyo dini), nazo ni hukmu za kiShari'ah kama sala, nayo (serikali) ni twarika ya kutekeleza hukmu za Kiislamu na kubeba da’wa. Ni lazima kuondolewa kila kinacho leta hisia ya kuhusisha dini na maana ya kiroho na kuitenganisha na utawala na siasa, basi huondolewa mashirika yanayo simamia upande wa kiroho. Huondolewa idara ya miskiti na itakuwa idara yake hufuata idara ya elimu, na huondolewa mahakama ya kiShari'ah na mahakama za kiraia na kuweka nidhamu ya mahakamu moja kwa mujibu wa Uislamu. Na utawala wa Kiislamu ni utawala mmoja.

Uislamu ni aqida na nidhamu. Amma aqida hiyo ni imani kwa Mwenyezi Mungu, malaika wake, vitabu vyake, mitume wake, Siku ya Mwisho na *al-qadhaa wa al-qadar* kheri yake na shari yake kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Uislamu umejenga aqida yake juu ya akili kwa yale yanayodirikiwa na akili kama kumuamini Mwenyezi Mungu, utume wa Muhammad (saw) na Al-Qur’an Al-Kariim. Na ikaijenga juu ya mambo ya kufichika (*ghayb*) yaani yale yasiyo wezekana kudirikiwa na akili kama Siku ya Qiyama, malaika, pepo na moto kwa kusalimu amri kwa sharti ya kuwa chimbuko lake limethubutu kiakili nayo ni Al-Qur’an Al-Kariim na hadith *mutawatir*. Na Uislamu umefanya akili ndio kituo (*manta*) cha taklifu ya kiShari'ah.

Ama nidhamu nazo ni hukumu za kiShari'ah zinazopanga mambo ya mwanadamu. Nidhamu ya Kiislamu imejumuisha mambo haya yote lakini imezijumuisha kwa maana za kijumla na kuwacha ufafanuzi wake utolewe kutokana na maana jumla pindi kunapotokea utabikishaji. Imekuja Al-Qur’an Al-Kariim na hadithi sharifu ilhali imebeba hatua pana yaani maana jumla kutatua matatizo ya mwanadamu kwa jinsi yake kama mwanadamu, na ikawaachia mujtahidina watoe kutoka hizi maana jumla hukmu za kivipande kwa matatizo yanayotokea katika zama na mahali tofauti tofauti.

Uislamu una njia moja ya kutatua matatizo nayo ni kwa kumlingania mujtahid asome tatizo lililo tokea mpaka alifahamu kisha asome dalili za kiShari'ah zinazo ambatana na tatizo hilo kisha atoe suluhisho la tatizo hilo kutokana na *nusuu,* yaani atowe hukmu ya kiSheri'ah kwa suala hilo kutokana na dalili za kiShari'ah wala (mujtahid) hafuati njia nyengine katu. Na pindi anaposoma tatizo hilo, hulisoma kama tatizo la kibinadamu na si vyengine wala halichukulii tatizo kama ni tatizo la kiuchumi au la kiitjimai au la kiutawala au chochote chengine bali hulichukulia kama suala linalohitaji hukmu ya kiShari'ah mpaka aijue hukumu ya Mwenyezi Mungu juu yake.

## 7. HUKMU YA KISHERIA

Ni khutba ya mueka Shari'ah (*Ash-Shari'*) inayohusiana na vitendo vya waja, nayo ima imethubutu kwa kukatikiwa (*qat'iyy ath-thubut*) kama Al-Qur'an Al-Kariim na hadith *mutawatir* au imethubutu kidhana (*dhaniyy ath-thubut*) kama hadithi zisizokuwa za *tawatur*. Ikiwa imethubutu kwa kukatikiwa huangaliwa; ikiwa na maana ya kukatikiwa (*qat'iyy ad-dalalah*) basi hukmu inayobeba ni ya kukata kama rakaa katika swala zote za faradhi kwa swababu zimepokewa kupitia hadithi *mutawatir*. Na kama uharamu wa riba, kukata mkono wa mwizi na kumpiga viboko mzinifu ambazo ni hukmu zilizokatikiwa. Kupatia sawa (*swawaab)* katika hayo kumelazimishwa na hakuna ndani yake ila rai moja tu ya kukatikiwa.

Ikiwa khutuba ya *Ash-Shari'* ni *qat'iyy ath-thubut* na *dhaniyy ad-dalalah*, basi hukmu inayoibeba huwa ni ya ki-dhana kwa mfano aya ya jizya ambayo ni *qat'iyy ath-thubut* lakini *dhaniyy ad-dalalah* katika ufafanuzi. Ma-Hanafi wanashurutisha kwamba iitwe jizya na kwamba idhihirishwe udhalilifu kwa mwenye kuitoa pindi inapotolewa. Ma-Shafi'i hawashurutishi iitwe jizya bali ni sahihi ichukuliwe kwa jina la zaka ya ziada (*mudhwaa'afa*) wala si dharura kudhihirishwa udhalilifu bali hutosha unyenyekevu kwa hukmu za Kiislamu.

Ama ikiwa khutba ya *Ash-Shari'* ni *dhaniyy ath-thubut* kama hadithi isiyokuwa *mutawatir* basi hukmu inayoibeba ni ya ki-dhana sawa sawa iwe maana yake *qat'iyy ad-dalalah* kama saumu ya siku sita katika Shawali ambayo imethibiti kupitia Sunna au ni *dhaniyy ad-dalalah* kama kukataza kukodisha ardhi ambayo imethbiti kupitia Sunna.

Khutuba ya *Ash-Shari'* hufahamika kutokana nayo hukmu ya ki-sheria kupitia ijtihadi iliyo sahihi kwa hivyo huwa ijtihadi ya mujtahidina ndiyo inayodhihirisha hukmu ya kiShari'ah. Kwa hivyo hukmu ya Mwenyezi Mungu iliyo juu ya shingo ya mujtahid ni ile inayomfikisha ijtihadi yake na kumkinaisha zaidi madhania yake.

*Mukallaf* pindi anapotimiza uwezo kiukamilifu wa kufanya ijtihadi katika mas-ala miongoni mwa mas'ala au katika mas-ala yote, akifanya ijtihadi ndani yake ili ijtihadi yake imfikishe kwa hukmu ndani yake basi wote (wanavyuoni) wameafikiana kuwa haijuzu kwake kufanya *taqleed* kwa mwengine miongoni mwa mujtahidina kinyume na rai aliyo lazimishwa na madhania yake, wala haijuzu kwake kuiwacha rai yake isipokua tu katika hali nne:-

**Ya kwanza:** Inapo mbainikia yeye kua dalili ambayo ameitegemea katika ijtihadi yake ni dhaifu, na dalili ya mujtahid mwengine ni yenye nguvu zaidi kuliko dalili yake. Hivyo basi katika hali hiyo ni wajibu juu yake kuiwacha papo hapo hukmu ambayo ameifikia kupitia ijtihadi yake na kuchukua hukmu iliyo na dalili yenye nguvu zaidi

**Ya pili:** Inapo mbainikia yeye kua mujtahid mwengine ni muweza zaidi kuliko yeye juu ya kufungamanisha (*rabt*) au ni muelewa zaidi wa waqiah na ni mwenye kuzifahamu zaidi dalili au ni muelewa zaidi wa dalili za *assam'iyyah* (Quran na Sunna), hapo basi inafaa (*yajuuz)* kwake katika hali hiyo kuiwacha hukmu ambayo ameifikia kupitia ijtihadi yake, na kumfuata mujtahid huyu ambaye amemuamini kwa ijtihadi yake kuliko kuiamini nafsi yake kwa ijtihadi yake.

**Ya tatu:** Kukiwa kuna rai inayokusudiwa kuunganisha neno la Waislamu kwa ajili ya maslahi ya Waislamu, hapo basi katika hali hiyo inafaa (*yajuuz)* kwa mujtahid huyo kuwacha kile kilichofikiwa kwa ijtihadi yake na kuchukua hukmu ambayo inakusudiwa

kuwaunganisha waislamu juu yake na hili lilipatikanwa kwa Athman (ra) wakati wa kubaishwa kwake.

**Ya nne:** Pindi Khalifah anapotabanni hukmu ya kisharia inayo gongana na hukmu ambayo ameifikia kupitia ijtihadi yake, katika hali hiyo ni wajibu juu yake kuwacha kuitendea kazi kile alichokifikia kwa ijtihadi yake na kuifanyia kazi hukmu ambayo aliyoitabanni Khalifah, kwa sababu *ijmaa* ya maswahaba wamekubaliana juu ya ("amri ya Khalifah huondosha ikhtilafu") na kua amri yake ni yenye kutekelezwa na Waislamu wote.

Amma ikiwa hajafanya ijtihadi yule aliye na uwezo wa ijtihadi basi yajuzu kwake kufanya *taqleed* kwa mwengine miongoni mwa mujtahidina, kwa sababu *ijmaa* ya maswahaba imeafikiana ya kuwa yajuzu kwa mujtahid kumfuata mwengine miongo mwa mujtahidina.

Amma yule ambaye hana uwezo wa ijtihadi naye ni *muqallid*, nao ni aina mbili *muttabi'* na *'ammi*. *Mutabi'* ni yule ambaye amekusanya baadhi ya taaluma zinazotegemewa katika ijtihadi, basi yeye humfuata mujtahid baada ya kujua dalili yake. Wakati huo huwa hukmu ya Mwenyezi Mungu juu ya *muttabi'* ni kauli ya mujtahid aliyoifuata. Amma *'ammi* yeye si mwenye kukusanya baadhi ya taaluma zinazotegemewa katika ijtihadi lakini yeye humfuata mujtahid bila kujua dalili aliyoitegemea. Huyu *'ammi* hulazimika kufuata kauli ya mujtahidina na kuzichukuwa hukmu walizozivua, na huwa hukmu ya kiShari'ah kwake ni ile iliyovuliwa na mujtahid anayemfuata. Kwa haya hukmu ya kiShari'ah ni ile iliyovuliwa na mujtahid aliyetimiza shuruti za ijtihadi na huwa kwa haki yake ndiyo hukmu ya Mwenyezi Mungu na haijuzu kata kata kuikhalifu na kufuata nyengine, na hivyo hivyo ni lazima kwa *muqallid* anayefuata hukmu ya Mwenyezi Mungu haijuzu kwake yeye kuikhalifu.

*Muqallid* anapofuata baadhi ya mujtahidina katika hukmu juu ya tukio miongoni mwa matukio na akatenda kwa kauli yake juu yake, basi hana ruhusa kata kata kurudi nyuma juu ya hukmu hiyo baada hapo na kufuata nyengine. Ama kumfuata mujtahid mwengine asiyekuwa huyo katika hukmu nyengine, hiyo yajuzu kwake kwa sababu ya *ijmaa* ya maswahaba iliyotokea juu ya ruhusa ya kuchukua fatwa kutoka kila mjuzi juu ya mas'ala. Ama akiwa *muqallid* amejifunga na *madhhabu* moja kama mfano madhab ya Shafi' na akasema mimi nafuata *madhhabu* yake na akajifunga nayo, kuna ufafanuzi juu ya hilo. Nao ni: Hakika kila mas'ala kutoka *madhhabu* anayoyafuata yaliyo fungamana kitendo chake na mas-ala hayo basi kata kata si sawa yeye kumfuata mwengine katika mas-ala hayo, na mas-ala ambayo kitendo chake hakija fungamana na mas-ala hayo hapo hana kizuizi cha kumfuata mwengine katika mas-ala hayo.

## 8. AINA ZA HUKMU ZA KISHARI'AH

Hukmu za Shari'ah ni faradhi, haramu, mandub, makruh na mubah. Na hukmu ya kiShari'ah huwa ima ni khutuba inayoomba kutenda kitendo au ni khutuba ya kuomba kuwacha (kutenda). Ikiwa khutuba ya kuomba kutenda kitendo basi ikiambatana na maombi ya lazima ya kutenda kitendo, huwa ni faradhi na wajibu yote mawili yana maana moja. Ikiwa yameambatana na maombi yasiyokuwa na kutendwa kwa lazima, huwa ni mandub. Na yakiambatana na khutuba ya kuwacha (kutenda) basi ikiwa yameambatana na maombi ya ulazima ya kuwacha huwa ni haramu na *mahdhur* yote mawili kwa maana moja. Na yakiambatana na maombi yasiyokuwa ya lazima ya kuwacha basi huwa ni makruh. Na kwa hayo faradhi na wajibu ni yale ambayo husifiwa nayo mtendaji na hukemewa asiyeyatenda au ni yale anayestahiki adhabu mwenye kuwacha kuyatenda. Haramu huwa yale anayokemewa mtendaji na kusifiwa asiyeyatenda au hustahili adhabu anaeyatenda. Na mandub ni yale husifiwa mtendaji na

hakemewi asiyeyatenda au hupata thawabu mtendaji na haadhibiwi asiyeyatenda. Na makruh ni yale anayesifiwa asiyeyatenda au kuepukana nayo ni bora kuliko kuyatenda. Na mubah ni yale yaliyodokezwa na dalili zilizo sikika (*sam'iyyah*) kutoka khutuba ya *Ash-Shari'* kwa kukhiyarishwa baina ya kutenda na kutotenda.

## 9. SUNNA

Sunna katika lugha ni njia. Ama katika Shari'ah huachiliwa kutumiwa juu ya yale ya *nafila* yaliyonukuliwa kutoka kwa Mtume (saw) kama rakaa za sunna huitwa sunna yaani kinyume na faradhi. Wala sio maana yake kuitwa sunna kuwa inatoka kwa Mtume (saw) na faradhi ni kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Bali sunna na faradhi hutoka kwa Mwenyezi Mungu, na Mtume ni mbalighishaji yaliyotoka kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa sababu yeye hazungumzi kwa matamanio ya nafsi yake isipokuwa ni wahyi anao teremshiwa. Basi hata kama ni sunna iliyo nukuliwa kutoka kwa Mtume (saw) lakini imenukuliwa *nafila* basi huitwa sunna kama inavyo nukuliwa faradhi kama faradhi na huitwa faradhi. Rakaa mbili za alfajiri ni faradhi zilizo nukuliwa kutoka kwaa Mtume (saw) kwa njia ya *tawatur* huwa ni faradhi. Na rakaa mbili za alfajiri za Sunna kadhalika zimenukuliwa kwa Mtume (saw) kwa njia ya *tawatur* ni *nafila*. Zote mbili zatoka kwa Mwenyezi Mungu na hazitoki kutoka kwa Mtume kibinafsi. Amri ni faradhi na *nafila* katika ibada, na faradhi na mandub kwengineko. *Nafila* ndio hiyo mandub imeitwa *nafila* na ikaitwa sunna.

Na hivyo hivyo huitwa sunna kila kinchotokana na Mtume katika dalili za kiShari'ah zisizokuwa Qur'ani. Na huingia katika hayo maneno ya Mtume, vitendo vyake na kukiri kwake - kunyamaza kwake.

## 10. KUIGIZA VITENDO VYA MTUME (SAW)

Vitendo vinavyotokana na Mtume (saw) hugawanyika vigawanyo viwili. Katika hivyo ni vitendo vya kimaumbile (*jibiliyya)* na nyenginezo ni zile zisizokuwa hayo. Amma vitendo vya kimaumbile kama kusimama, kukaa, kula, kunywa na mfano wake, hakuna ubishi kuwa hivyo ni *mubah* kwake yeye na kwa Ummah wake. Kwa hivyo haziingii katika *mandub*.

Ama vitendo visivyo kuwa vya kimaumbile navyo ima huwa vimethibiti kuwa ni makhsusi yake bila kushirikiana katika hivyo na yeyote au si katika vilivyo makhsusi kwake yeye. Ikiwa miongoni mwa yale yaliyothibiti kuwa ni katika makhsusi yake (saw), nayo ni kama kukhusishwa kwake kuruhusiwa kuunganisha katika funga (*wiswaal*) yaani kuunganisha mchana na usiku katika swaumu, na kama kuzidisha katika ndoa zaidi ya wake wanne na yasiyokuwa hayo katika khususiya zake, basi haijuzu kwetu kushirikiana naye katika hayo. Imethibiti kwa *ijmaa* kuwa ni katika khususiya zake kwa hivyo haijuzu kumuigiza katika hayo.

Ama kinachojulikana kama kitendo chake cha kutubainishia sisi, hicho ni dalili bila ikhtilafu. Nacho ni ima kupitia maneno yake wazi kama msemo wake (saw): "**Swalini kama munavyo niona nikiswali**" na "**Chukueni kutoka kwangu mimi vitendo vyenu vya Haji (*manasiki*)**", hiyo ni dalili ya kuwa kitendo chake ni kwa ajili ya kutubainisha sisi ili tumuigize. Na ima kupitia dalili za dhurufu (*qarain al-ahwal*) nacho ni kama kukata kwake mkono wa mwizi kwenye kitengele kutubainishia msemo wa Aliyetukuka:

**{ فَاقْطَعُوا أَيْدِيَهُمَا }**

"*Wakateni mikono yao*" [TMQ 5:38]

Na ufafanuzi (*bayan*) huu katika kitendo chake kupitia msemo au dalili za hali (*qarain al-ahwal*) hufuata kinachobainishwa katika kuwa *wajib* au *mandub* au *mubah* kwa mujibu inavyodokeza dalili.

Ama vitendo ambavo havikuambatanishwa na kinachodokeza kuwa hivyo vitendo ni kwa ajili kubainisha si kwa kukataa (*nafyu)* au kuthibitisha (*ithbaat)*, huwa ima hudhihirika ndani yake shabaha ya kujikurubisha (kwa Mwenyezi Mungu) na ima haidhihiriki. Ikidhihirika ndani yake shabaha ya kujikurubisha basi huingia katika *mandub*; mja hupata thawabu akilitenda wala haadhibiwi kwa kuliwacha mfano wa sunna ya *Adh-Dhuha*. Ikiwa haikudhihirika ndani yake shabaha ya kujikurubisha, huingia katika *mubah*.

## 11. KUTABANNI HUKMU ZA KISHARI'AH

Walikuwa Waislamu katika zama za maswahaba wakizichukua hukmu za kiShari'ah wenyewe binafsi kutoka Kitabu na Sunna. Na walikuwa ma-Kadhi pindi wanapoamua husuma baina ya watu huvua (*istinbat*) hukmu ya Shari'ah wao wenyewe katika kila tukio wanalo kumbana nalo. Na walikuwa watawala kutoka Amir al-Muumineen mpaka mawali na wengineo wakivua wenyewe hukmu za kiShari'ah ili kutatua kila tatizo katika matatizo wanayo kumbana nayo wakati wa utawala wao. Abu Musa Al-Ash'ari (ra) na Shurayh (ra) wote wawili walikuwa ni ma-Kadhi na walikuwa wakivua hukmu na wakihukumu kwa ijtihadi zao. Na alikuwa Muadh bin Jabal (ra) ni wali katika zama za Mtume, na alikuwa akivua hukmu na akihukumu katika wilaya yake kwa ijtihadi yake. Na walikuwa Abubakar (ra) na Umar (ra) katika Khilafah zao wakivua hukmu wenyewe na kila mmoja wao alihukumu juu ya watu kwa kile alichokivua mwenyewe. Na walikuwa Muawiya (ra) na Amru bin al-Aas (ra) ni ma-wali, na walikuwa kila mmoja wao akivua hukmu mwenyewe na kuhukumu watu katika wilaya zao. Pamoja na ijtihadi hii kwa mawali na maKadhi, alikuwa Khalifah akitabanni hukmu khasa maalum ya kiShari'ah na kuamuru watu kuifanyia kazi. Na walikuwa watu wakijifunga nazo kwa kuzifanyia kazi na kuwacha rai zao na ijtihadi zao kwa sababu hukmu ya kiShari'ah ni 'Amri ya Imamu inatekelezwa kwa dhahiri na kwa siri.' Na katika hayo Abubakar (ra) alitabanni kutoa talaka tatu (wakati moja) ni moja, na kugawanya mali kwa Waislamu kwa usawa bila kuangalia aliyetangulia mwanzo kusilimu au kwa lolote jengine, na wakamfuata Waislamu juu ya hayo na wakazifanyia kazi ma-kadhi na ma-wali. Alipokuja Umar (ra) akatabanni rai katika mambo hayo mawili tofauti na rai ya Abubakar (ra). Akalazimisha talaka tatu zichukuliwe kuwa tatu na akagawanya mali kwa mujibu ya kutangulia (kusilimu) na kwa mwenye haja kwa kufadhilisha si kwa usawa; Waislamu wakamfuata juu ya hayo na wakahukumu kwayo ma-kadhi na ma-wali. Kisha akatabani Umar ardhi zinazotekwa ngawira (*ghanima*) katika vita ni ngawira za Bait al-Mal na zibakie katika mikono ya wenyewe wala zisigawanywe kwa wapiganaji wala Waislamu, na Waislamu wakamfuata juu ya hilo na ma-wali na ma-kadhi wakahukumu kwa mujibu yake. Ilikuwa *ijmaa* (*Ijma As-Swahabah*) iliyokatikiwa kuwa ni juu ya Imamu kutabanni hukmu maalumu na kuamuru kutendewa kazi juu yake, na ni juu ya Waislamu kumtii hata kama itakhtalifiana na ijtihadi zao. Na qaida za kiShari'ah zilizo mashuhuri ni: '*Sultani ana haki ya kutabanni kwa kadiri ya kutatua matatizo*' na: '*Amri ya Imamu humaliza mizozo*' na: '*Amri ya Imamu hutekelezwa kwa dhahiri na kwa siri*.'Kwa hivyo walikuwa ma-Khalifah baada hapo wakitabanni hukmu maalumu. Alitabanni Harun Ar-Rashid kitabu '*Al-Kharaj*' katika upande wa kiuchumi na kulazimisha watu kufanyia kazi kwa mujibu wa hukmu zilizo ndani yake.

## 12. KATIBA NA KANUNI

Neno 'kanuni' ni istilahi ya kigeni na maana yake kwao ni amri itokayo kwa Sultani ili watu wajipeleke kwa mujibu wake. Na imejulikana kanuni kuwa ni 'mkusanyiko wa *qaida* (*qawaid*) anazo walazimisha Sultani watu kuzifuata katika mahusiano yao.' Na imeitwa kanuni msingi ya kila serikali tamko la 'katiba', na ile kanuni inayo tokana na ile nidhamu iliyotajwa na katiba imeitwa tamko la 'kanuni.' Imejulikana katiba kuwa 'kanuni inayo

fafanua umbo la serikali na nidhamu ya utawala yake, na hubainisha mipaka na kazi ya kila mamlaka ndani yake' au 'kanuni inayopanga nidhamu ya utawala jumla nayo ni serikali na huweka mipaka ya mahusiano yake na watu na hubainisha haki za serikali na majukumu yake kwao na haki za watu na majukumu yao kwake.' Katiba zina machimbuko tofauti, miongoni mwake ni zile zilizo chimbuka kwa sura za kikanuni na zipo zilizochimbuka kutokana na mila na desturi kama katiba ya Uingereza na zipo zilizowekwa na kamati iliyobuniwa na bunge la kitaifa liliokuwa na uwezo katika umma wakati huo, basi ikaweka katiba na ikabainisha jinsi ya kuirekebisha kisha kamati hio ikajiuzulu na kusimama mahala pake utawala uliowekwa na katiba kama ilivyotokea Ufaransa na Amerika. Katiba na kanuni zina machimbuko zilimo chukuliwa humo, nayo ni vigawanyo viwili: la kwanza linalokusudiwa ni chimbuko ilimo chimbuka kutoka humo katiba na kanuni moja kwa moja kama mila, dini, rai za wanavyuoni wa fiqhi, hukmu za mahakama, misingi ya uadilifu na usawa. Haya huitwa machimbuko ya kisheria mfano katiba za baadhi za serikali za kimagharibi kama Uingereza na Amerika. La pili lililo kusudiwa ni kilichozaliwa nacho (*almushtaqqu 'anhu)* au ambacho kilicho nukuliwa kutoka kwake katiba au kanuni, mfano Katiba ya Ufaransa na katiba za baadhi ya nchi katika ulimwengu wa Kiislamu kama Uturuki, Misri, Iraq, Syria. Hili huitwa chimbuko la kihistoria.

Huu ni mukhtasari wa istilahi inayo bebwa na maneno mawili ya katiba na kanuni, nayo katika mukhtasari wake humaanisha kuwa serikali huchukua kutoka machimbuko tofauti tofauti sawa sawa yawe ni machimbuko ya kisheria au chimbuko la kihistoria hukmu maalumu ambazo huzitabanni na kuamrisha zifanyiwe kazi, na huwa hukmu hizi baada kutabanniwa na serikali huwa ni katiba ikiwa ni katika hukmu jumla na huwa ni kanuni ikiwa ni katika hukmu khasa.

Swali linalomkabili Muislamu leo ni: Je, yajuzu kutumia istilahi hii au haijuzu? Na jawabu ya hilo ni kuwa matamko ya kigeni ambayo hubeba maana ya kiistilahi maalum ikiwa istilahi yake hukhalifu istilahi ya Waislamu basi haijuzu kuitumia mfano tamko la 'uadilifu wa kijamii' linao maanisha nidhamu maalum ambayo kwa ufupi ni kudhamini elimu, matibabu kwa mafukara na kudhamini haki za wenye vibaruwa na wafanyi kazi. Istilahi hii hukhalifu istilahi ya Waislamu kwa sababu uadilifu kwa Waislamu ni kinyume na dhuluma. Ama kudhamini elimu na matibabu hayo ni kwa watu wote, matajiri na mafukara, na kudhamini haki ya muhitaji na aliye dhaifu ni haki kwa watu wote wanaobeba uraia wa serikali ya Kiislamu sawa sawa ni wafanyi kazi au la, au wawe ni vibaruwa au wakulima au wasiokuwa hao. Ama ikiwa tamko humaanisha istilahi inayopatikana maana yake kwa Waislamu basi yajuzu kuitumia mfano tamko la kodi ambalo humaanisha mali ambayo huchukuliwa kutoka kwa watu ili kuendesha serikali. Waislamu hupata mali inayo chukuliwa na serikali ili kuendesha serikali kwa hivyo ni sahihi kwetu kutumia tamko la kodi. Na hivyo hivyo tamko la katiba na kanuni ambayo humaanisha kutabbani serikali hukmu maalum ikawatangazia watu na kuwalazimisha kuzitendea kazi na ikawahukumu kwa mujibu wake hizo hukmu. Maana hii hupatikana kwa Waislamu kwa hivyo hakuna kinachotuzuia kujuzu kutumia maneno mawili ya katiba na kanuni, na inakusudiwa kwazo ni hukmu anazozitabanni Khalifah katika hukmu za kiShari'ah. Isipokuwa kuna tofauti baina ya katiba ya Kiislamu na kanuni za Kiislamu, na katiba nyenginezo. Machimbuko ya katiba na kanuni nyenginezo ni ada, hukumu za mahakama na kadhalika na zilizaliwa na kamati ya taasisi za kutunga katiba na bunge lililo chaguliwa na watu kutunga kanuni kwa sababu kwao watu ndio asili ya utawala, na ubwana (*as-siyadah*) ni kwa watu. Ama katiba ya Kiislamu na kanuni za Kiislamu, chimbuko lake ni Kitabu na Sunna si chengine, na huzaliwa kwa ijtihadi za mujtahidina anazo zitabanni Khalifah katika hizo ni hukmu maalumu anazo ziamuru na kulazimisha watu kuzitendea kazi, kwa sababu ubwana ni wa Shari'ah. Na ijtihadi za

kuvua hukmu za kiShari'ah ni haki ya Waislamu wote na *fardhi kifaya* juu yao, na ni haki ya Khalifah peke yake kutabanni hukmu za kiShari'ah.

Huu ni upande wa kujuzu utumiaji wa maneno mawili ya katiba na kanuni. Ama upande wa kuwepo dharura ya kutabanni hukmu: Lile ambalo Waislamu wamekuwa wakifuata tangu siku za Abubakar (ra) mpaka Khalifah wa mwisho Muislamu, ni dharura ya kutabanni hukmu maalumu na kuamrishwa Waislamu kuzitendea kazi. Lakini kutabanni huko ilikuwa kwa hukmu khasa wala hakukuwa kutabanni kijumla kwa kila hukmu inayo hukumu kwayo serikali. Serikali haikutabanni kijumla ila katika baadhi ya zama; walitabanni *Al-Ayyubiyyuun* madhhabu ya *Ash-Shafi* na serikali ya Uthmaniyya ilitabanni madhhabu ya *Hanafi.*

Suali la kuulizwa ni: Je, ni katika maslahi ya Waislamu kuweka katiba jumla na kanuni jumla kwao au la? Jawabu la hilo ni kuwepo katiba jumla na kanuni jumla kwa hukmu zote haisaidii katika uvumbuzi na ijtihadi. Kwa hivyo Waislamu karne za mwanzo, karne za maswahaba na *tabiin* na *tabii tabiin* walijiepusha na kutabanni hukmu zote kutoka kwa Khalifah bali walitosheka na kutabanni hukmu katika ahkamu maalumu zisizokuwa na budi kuzitabanni kwa ajili ya kuhifadhi umoja wa hukmu (utawala) na Shari'ah na idara. Kwa hivyo ni bora ili kuwepo uvumbuzi na ijtihadi kukosekana katiba jumla ya serikali juu ya hukmu zote. Bali kuwa na katiba inayo jumuisha hukmu jumla zinazoweka umbo la serikali na kudhamini kuhifadhiwa umoja wake na kuwaachia mawali na ma-kadhi kufanya ijtihadi na istinbati. Isipokuwa haya hutokea ikiwa ijtihadi imesahalishwa na ikiwa watu ni mujtahidina kama ilivyokuwa hali katika zama za maswahaba na *tabiin* na *tabii tabiin*. Ama ikiwa watu wote ni muqallidina wala hawapatikani kati yao mujtahidina ila kwa uhaba, basi huwa ni jambo la lazima kwa serikali kutabanni hukmu ambazo itahukumu watu kwazo sawa sawa iwe ni Khalifah, ma-wali au ma-kadhi kwa sababu ni vigumu kuhukumu na yale aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu kwa upande wa mawali na ma-kadhi kwa kukosekana ijtihadi zao isipokuwa kuwepo taqleed tofauti tofauti zinazo gongana, na tabanni hupatikana baada ya kuchunguza na kufahamu tukio na kuijuwa dalili. Juu ya hayo, kuwachwa ma-wali na ma-kadhi kuhukumu kwa wanayo yafahamu itafikia kukhtalifiana kwa hukmu na kugongana kwao katika serikali moja bali katika biladi moja, bali huenda kufikia kuhukumu kuwa tofauti na yale yaliyoteremshwa na Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo huwa ni lazima kwa serikali ya Kiislamu, katika hali ya ujinga katika kufahamu Uislamu kama ilivyo hali leo, kutabanni hukmu maalumu na kuwa tabani hii ni jumla kwa hukmu zote mpaka serikali idhibiti mambo na kupeleka mambo yote ya Waislamu kwa mujibu wa hukmu za Mwenyezi Mungu. Ni juu ya serikali, pindi inapotabanni hukmu na kuweka katiba na kanuni, ni wajibu ijifunge na hukmu za kiShari'ah peke yake wala isichukuwe chochote chengine bali isitafiti chochote chengine. Isichukuwe zisizokuwa hukmu za kiShari'ah kwa chochote, bila kuangalia kama yaafikiana na Uislamu au hukhalifiana nayo. Haichukui kwa mfano utaifishaji (*taameem*) bali huweka hukmu ya umilikaji *amma*. Kwa hivyo ni wajibu kujifunga na hukmu za kiShari'ah katika kila kinacho ambatana na fikra na njia (*twariqa*). Ama kanuni na nidhamu zisizo ambatana na fikra na njia, na ambazo hazidhihirishi mtazamo maalum kama kanuni za kiidara na kuziratibisha idara na yanayo fanana na hayo, huhisabiwa miongoni mwa vyombo na mbinu (*al-wasiila wal-usluub)*. Nayo ni kama elimu, viwanda na teknolojia; huzichukua serikali na kuzitumia katika kupanga mambo yake kama alivyofanya Umar ibn al-Khattab (ra) pindi alipoweka sajili (*diwan*) za jeshi; yeye alizichukua kutoka Fursi. Na vitu hivi vya kiidara na kiufundi sio katika katiba wala sio katika kanuni za kiShari'ah wala haviwekwi katika katiba. Kwa hivyo ni wajibu kwa serikali ya Kiislamu kuwa katiba yake ni ahkamu za kiShari'ah; hii humaanisha kuwa katiba yake ni ya Kiislamu na kanuni zake kuwa za Kiislamu. Pindi inapotabanni hukmu ni wajibu kwake kutabanni juu ya msingi wa nguvu ya dalili ya

kiShari'ah pamoja na ufahamu sahihi kwa tatizo inalolikabili. Kwa hivyo ni lazima kwake kuchunguza tatizo, mwanzo kwa kufahamu kwa sababu kufahamu tatizo ni jambo la dharura sana kisha kufahamu hukmu ya kiShari'ah inayo ambatana na tatizo hilo kisha kuchunguza dalili ya hukmu ya kiShari'ah kisha kutabanni hukmu hiyo juu ya msingi wa nguvu ya dalili. Ni kwa kuchukuliwa hukmu hizi za kiShari'ah ima kutoka rai ya mujtahid baada ya kuichunguza dalili na kuwa na utulivu na nguvu yake, ima kutoka Kitabu, Sunna, *ijmaa* au *qiyaas* lakini kwa ijtihadi ya kiShari'ah hata kama ni ijtihadi ya kivipande nayo ni ijtihadi ya ki-mas'ala. Ikitaka kutabanni rai ya kukataza bima juu ya vitu kwa mfano, ni juu yake kwanza kuchunguza ni nini bima juu ya vitu na kuijua kisha kuchunguza njia za kumiliki kisha kutabikisha hukmu ya Mwenyezi Mungu katika umilikaji juu ya bima na kutabanni hukmu ya kiShari'ah juu ya hilo. Kwa haya, hapana budi ila kuwepo kwa ajili ya katiba na kwa ajili ya kila kanuni utangulizi katika kubainisha kwa uwazi madhhabu iliyofuatwa katika kuchukua kila kifungu chake na dalili iliyotegemewa juu yake au kubainisha dalili ambayo imevuliwa kutoka kwake kifungu hicho ikiwa kuvuliwa kwake kumepitia ijtihadi sahihi, ili Waislamu wajue hukmu ambayo serikali imetabanni katika katiba na kanuni nazo ni hukmu za kiShari'ah zilizovuliwa kwa ijtihadi iliyo sahihi. Hii ni kwa sababu Waislamu hawalazimiki kuitii serikali katika yale inayo hukumu ila ikiwa ni hukmu ya kiShari'ah iliyo tabaniwa na serikali. Na juu ya msingi huu hutabanni serikali hukmu za kiShari'ah ili ziwe ni katiba na kanuni ili izihukumie nazo watu wanaobeba uraia wake.

Kwa njia ya mfano, tunaweka mbele ya Waislamu mfano wa katiba ya serikali ya Kiislamu katika ulimwengu wa Kiislamu mpaka waisome Waislamu ilhali wao wanafanya kazi kusimamisha serikali ya Kiislamu inayobeba ulinganizi wa Kiislamu kwa ulimwengu. Hapana budi itambuliwe kuwa katiba hii si makhsusi kwa eneo fulani bali ni ya serikali ya Kiislamu katika ulimwengu wa Kiislamu; wala haikusudiwi serikali maalum au biladi maalum.

## 13. AKHLAQI KATIKA UISLAMU

Umejulikana Uislamu kuwa ni dini ambayo aliyoiteremsha Mwenyezi Mungu kwa bwana wetu Muhammad (saw) ili kupanga mahusiano ya mwanadamu na muumba wake, na nafsi yake, na wengine kati ya wanadamu. Mahusiano ya mwanadamu na muumba wake hujumuisha itikadi na ibadati, na mahusiano ya mwanadamu na nafsi yake hujumuisha akhlaqi, vilaji na mavazi, na mahusiano yake na wengineo kati ya wanadamu hujumuisha maingiliano (*mu'amalat*) na nidhamu ya kuadhibu wakhalifu.

Uislamu hutatua matatizo yote ya mwanadamu na humuangalia mwanadamu kikamilifu asiyegawanyika. Kwa hivyo hutatua matatizo yake kwa njia moja, na imebuniwa nidhamu yake juu ya msingi wa kiroho nayo ni aqeeda, na ikawa upande wa kiroho ndio msingi wa hadhara yake, na ndio msingi wa serikali na ndio msingi wa Shari'ah yake.

Pamoja na kuwa Shari'ah ya Kiislamu imepambanua nidhamu zake kwa upambanuzi wa kinaganaga kama nidhamu za kiibadati na maingiliano na nidhamu ya kuadhibu wahalifu, pamoja na yote hayo haikuiwekea akhlaqi nidhamu fafanuzi bali ikazifanya ahkamu za kiakhlaqi kama maamrisho na makatazo kutoka kwa Mwenyezi Mungu bila kuangalia kuzipambanua kuwa akhlaqi zapasa kupewa upande maalumu wa uangalizi unao tofautiana na mwengine. Bali akhlaqi katika upande wa ufafanuzi wa ahkamu ni chache kuliko nyengine wala haikuwekewa katika fiqhi mlango maalumu. Vitabu vya kifiqhi vinavyokusanya ahkamu za kiShari'ah hazina mlango maalumu unayoitwa 'mlango wa akhlaqi.' Wala mafuqahaa na mujtahidina hawakushughulika na uchunguzi au uvuaji (*istinbat)* katika mambo ya ahkamu za kiakhlaqi.

Akhlaqi haziathiri katika kujenga mujtama kabisa, kwa sababu mujtama hujengwa juu ya nidhamu ya kimaisha na huathirika (mujtamaa) kwa hisia na fikra. Ama akhlaqi haiathiri katika kujenga mujtama si katika kuunyanyua au kuudidimiza kwake; bali chenye kuathiri ni hadhara ya kijumla inayotokana na nidhamu juu ya maisha, na chenye kupeleka mujtama si akhlaqi bali ni nidhamu zinazo tabikishwa ndani yake na fikra na hisia zinazobebwa na watu. Akhlaqi zenyewe hutokana na fikra na hisia, na ni natija ya nidhamu inayo tabikishwa.

Kwa hayo haijuzu kubeba ulinganizi wa akhlaqi kwa mujtama kwa sababu akhlaqi ni natija ya maamrisho ya Mwenyezi Mungu nayo hutoka kutoka ulinganizi wa aqida na kwa kutabikishwa Uislamu kikamilifu. Na kwa sababu ulinganizi wa akhlaqi huugeuza ufahamu wa Kiislamu juu ya maisha na huwaweka watu mbali na ufahamu wa kihakika juu ya mujtama na nguzo zake, na huwapa matumaini ya kirongo juu ya uwema wa kibinafsi unaowapeleka kughafilika na njia za kihakika kuendeleza maisha.

Na kwa haya huwa ni hatari kuufanya ulinganizi wa Kiislamu kuwa ni ulinganizi wa akhlaqi kwa sababu hutoa picha ya kirongo kuwa ulinganizi wa Kiislamu ni ulinganizi wa kiakhlaqi, kufuta sura ya kifikra ya Kiislamu, kuwa ni kizuizi kinachozuia watu kuufahamu Uislamu na kuwatowa kutoka katika twarika ya kipekee inayofikisha katika kutabikishwa kwake nayo ni kusimamishwa serikali ya Kiislamu. Shari'ah ya Kiislamu pindi inapotatua mahusiano ya mwanadamu na nafsi yake kwa hukmu za kiShari'ah zinazo ambatana na sifa za kiakhlaqi, haikuwekea hilo nidhamu kama ibadati na maingiliano bali imechunga ndani yake kupatikana thamani maalumu aliyoiamrisha Mwenyezi Mungu kama ukweli, uaminifu, kutokuwa na udanganyifu (*ghush*), uhasidi; hizo hupatikana kutokana na kitu kimoja nacho ni amri kutoka kwa Mwenyezi Mungu tuwe na thamani ya kiakhlaqi kama ukarimu na uwema (*fadhail*). Uaminifu ni akhlaqi aliyoiamrisha Mwenyezi Mungu na ni wajibu kuchunga thamani yake ya kiakhlaqi pindi unapotendwa (huo uaminifu); kwa hivyo hupatikana kwayo thamani ya kiakhlaqi na huitwa akhlaqi. Ama kupatikana sifa hizi kama natija ya vitendo kama stara ya kujizuia na yasiyotakikana (*iffa)* inayotokana na swala au kupatikana kwake kutoka uwajibu wa kuichunga pindi inapotendwa katika maingiliano kama ukweli katika biashara, haipatikani ndani yake thamani ya kiakhlaqi kwa sababu halikuwa ni lengo la kutendwa kitendo bali lilikuwa ni sifa iliyopatikana kama natija ya vitendo, na kutoka uwajibu wa kuchunga, sifa za kiakhlaqi kwa muumini pindi anapomuabudu Mwenyezi Mungu na pindi anapotenda maingiliano. Muumini huhakikisha shabaha ya kwanza thamani ya kiroho, katika swala na huhakikisha shabaha ya pili thamani ya kimada katika biashara na kusifika wakati huo huo kwa sifa za kiakhlaqi.

Sheria imebainisha sifa ambazo kusifika nazo ni kuwa na akhlaqi njema na zipi ambazo kusifika nazo ni kuwa na akhlaqi mbaya; ikahimiza akhlaqi njema na kukataza akhlaqi mbaya. Ikahimiza ukweli, uaminifu, uchangamfu wa sura, haya, kutendea wema wazazi, kuunganisha kizazi, kusaidia katika shida, na kumpendelea mwenziwe lile alipendalo mwenyewe. Na ikazifanya zote hizo na mithali yake kushajiisha kufuata maamrisho ya Mwenyezi Mungu. Na ikakataza yaliyo kinyume nayo kama urongo, khiyana, uhasidi, uovu na mithali yake, na ikazihisabu hizi na mithali yake kama makatazo aliyoyakataza Mwenyezi Mungu hayo.

Akhlaqi ni sehemu ya Shari'ah hii na sehemu miongoni mwa maamrisho ya Mwenyezi Mungu na makatazo yake, na hakuna budi kwa Muislamu ila kuzihakikisha katika nafsi yake ili zitimie amali zake katika Uislamu na kukamilika kutenda kwake maamrisho ya Mwenyezi Mungu. Isipokuwa kuzifikia mujtama mzima ni kwa njia ya kuwekwa hisia za Kiislamu na fikra za Kiislamu, na kwa kupatikana kwake katika mujtama ndio lazima

kupatikana kwake kwa watu binafsi. Ni wazi kuwa kuzifikia haziwi kwa ulinganizi kwa akhlaqi bali kwa njia iliyoashiriwa ni kuwekwa hisia na fikra. Isipokuwa ni lazima mwanzo kuandaliwe kikundi kwa Uislamu kikamilifu, watakuwa watu binafsi ni sehemu katika jamii sio kama watu binafsi kando, ili wabebe ulinganizi wa Kiislamu kwa jumla kwa mujtama ili waunde hisia za Kiislamu na fikra za Kiislamu ili watu waingie katika Uislamu makundi kwa makundi moja kwa moja kufuata kuingia kwao katika Uislamu makundi kwa makundi. Ni lazima ifahamike kwa uwazi kuwa huu msemo wetu hufanya akhlaqi kuwa ni jambo la lazima lililo lazimishwa kilazima na maamrisho ya Mwenyezi Mungu na kutabikishwa Uislamu, na huhakikisha dharura ya Muislamu kusifika kwa akhlaqi njema.

Amekwisha bainisha Mwenyezi Mungu katika Sura nyingi katika Al-Qur'an Al-Kariim sifa ambazo ni lazima kwa mwanadamu kusifika nazo, na ni lazima aziendee mbio. Sifa hizo ni itikadi, ibadati, maingiliano na akhlaqi na hakuna budi kuwa hizi sifa nne zijumuike. Asema Mwenyezi Mungu katika Sura Luqman:

**{وَلَقَدْ آتَيْنَا لُقْمَانَ الْحِكْمَةَ أَنْ اشْكُرْ للهِ وَمَنْ يَشْكُرْ فَإِنَّمَا يَشْكُرُ لِنَفْسِهِ وَمَنْ كَفَرَ فَإِنَّ اللهَ غَنِيٌّ حَمِيدٌ - وَإِذْ قَالَ لُقْمَانُ لابنه وَهُوَ يَعِظُهُ يَابُنَيَّ لاَ تُشْرِكْ بِاللهِ إِنَّ الشِّرْكَ لَظُلْمٌ عَظِيمٌ - وَوَصَّيْنَا الإِنسَانَ بِوَالِدَيْهِ حَمَلَتْهُ أُمُّهُ وَهْنًا عَلَى وَهْنٍ وَفِصَالُهُ فِي عَامَيْنِ أَنْ اشْكُرْ لِي وَلِوَالِدَيْكَ إِلَيَّ الْمَصِيرُ - وَإِنْ جَاهَدَاكَ عَلى أَنْ تُشْرِكَ بِي مَا لَيْسَ لَكَ بِهِ عِلْمٌ فَلاَ تُطِعْهُمَا - وَصَاحِبْهُمَا فِي الدُّنْيَا مَعْرُوفًا وَاتَّبِعْ سَبِيلَ مَنْ أَنَابَ إِلَيَّ ثُمَّ إِلَيَّ مَرْجِعُكُمْ فَأُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ - يَابُنَيَّ إِنَّهَا إِنْ تَكُنْ مِثْقَالَ حَبَّةٍ مِنْ خَرْدَلٍ فَتَكُنْ فِي صَخْرَةٍ أَوْ فِي السَّمَاوَاتِ أَوْ فِي الأَرْضِ يَأْتِ بِهَا اللهُ إِنَّ اللهَ لَطِيفٌ خَبِيرٌ - يَابُنَيَّ أَقِمْ الصَّلاَةَ وَأْمُرْ بِالْمَعْرُوفِ وَانْهَ عَنْ الْمُنكَرِ وَاصْبِرْ عَلَى مَا أَصَابَكَ إِنَّ ذَلِكَ مِنْ عَزْمِ الأُمُورِ- وَلاَ تُصَعِّرْ خَدَّكَ لِلنَّاسِ وَلاَ تَمْشِ فِي الأَرْضِ مَرَحًا إِنَّ اللهَ لاَ يُحِبُّ كُلَّ مُخْتَالٍ فَخُورٍ- وَاقْصِدْ فِي مَشْيِكَ وَاغْضُضْ مِنْ صَوْتِكَ إِنَّ أَنكَرَ الأَصْوَاتِ لَصَوْتُ الْحَمِيرِ }**

"*Na (wakumbushe) Luqman alipomwambia mwanawe hali ya kuwa anampa nasaha: Ewe mwanangu! Usimshirikishe Mwenyezi Mungu maana kumshirikisha ndiyo dhulma kubwa. Na tumemuusia mwanadamu (kuwafanyia ihsani) wazazi wake. Mama yake amechukuwa mimba yake kwa udhaifu juu ya udhaifu, na kumwachisha kunyonya katika miaka miwili ya kwamba anishukuru Mimi na wazazi wako. Meregeo yenu ni kwangu.--Na wakikushurutisha kunishirikisha Mimi na yale ambayo huna elimu nayo, usiwatwii lakini kaa nao kwa wema hapa duniani, na shika njia ya wale wanao elekea kwangu kisha. Maregeo yenu ni kwangu kisha nitakuambieni mliyokuwa mkiyatenda.--Ewe mwanangu! Kwa hakika jambo lolote ijapokuwa na uzito wa chembe ya khardali kikawa ndani ya jabali au mbinguni au katika ardhi, Mwenyezi Mungu atalileta bila shaka. Mwenyezi Mungu ni mjuzi wa mambo yaliyofichika na mjuzi wa mambo yaliyo dhahir.-Ewe mwanangu! Simamisha swala na amrisha mema na kanya maovu, na usubiri juu ya yale yatakayo kusibu. Hakika hayo ni katika mambo yanayo stahiki kuazimiwa.-Wala usiwatizame watu kwa upande mmoja wa uso (kwa ujeuri) wala usitembee katika nchi kwa maringo. Hakika Mwenyezi Mungu hampendi kila ajivunae mwenye kujifakhiri.-Na ushike mwendo wa kati na kati na uteremshe sauti yake. Bila shaka sauti ya punda ni mbaya kuliko sauti zote.*"[TMQ Luqman: 13-19]

Na asema Mwenyezi Mungu katika Surat Al-Furqan:

**{ وَعِبَادُ الرَّحْمَنِ الَّذِينَ يَمْشُونَ عَلَى الأَرْضِ هَوْنًا وَإِذَا خَاطَبَهُمْ الْجَاهِلُونَ قَالُوا سَلاَمًا - وَالَّذِينَ يَبِيتُونَ لِرَبِّهِمْ سُجَّدًا وَقِيَامًا - وَالَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا اصْرِفْ عَنَّا عَذَابَ جَهَنَّمَ إِنَّ عَذَابَهَا كَانَ غَرَامَ - إِنَّهَا سَاءَتْ مُسْتَقَرًّا وَمُقَامًا - وَالَّذِينَ إِذَا أَنفَقُوا لَمْ يُسْرِفُوا وَلَمْ يَقْتُرُوا وَكَانَ بَيْنَ ذَلِكَ قَوَامًا - وَالَّذِينَ لاَ يَدْعُونَ مَعَ اللهِ إِلَهًا آخَرَ وَلاَ يَقْتُلُونَ النَّفْسَ الَّتِي حَرَّمَ اللهُ إِلاَّ بِالْحَقِّ وَلاَ يَزْنُونَ وَمَنْ يَفْعَلْ ذَلِكَ يَلْقَ أَثَامَ - يُضَاعَفْ لَهُ الْعَذَابُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَيَخْلُدْ فِيهِ مُهَانًا - إِلاَّ مَنْ تَابَ وَآمَنَ وَعَمِلَ عَمَلاً صَالِحًا فَأُوْلَئِكَ يُبَدِّلُ اللهُ سَيِّئَاتِهِمْ حَسَنَاتٍ وَكَانَ اللهُ غَفُورًا رَحِيمًا - وَمَنْ تَابَ وَعَمِلَ صَالِحًا فَإِنَّهُ يَتُوبُ إِلَى اللهِ مَتَابًا - وَالَّذِينَ لاَ يَشْهَدُونَ الزُّورَ وَإِذَا مَرُّوا بِاللَّغْوِ مَرُّوا كِرَامًا - وَالَّذِينَ إِذَا ذُكِّرُوا بِآيَاتِ رَبِّهِمْ لَمْ يَخِرُّوا عَلَيْهَا صُمًّا وَعُمْيَانًا - وَالَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا هَبْ لَنَا مِنْ أَزْوَاجِنَا وَذُرِّيَّاتِنَا قُرَّةَ أَعْيُنٍ وَاجْعَلْنَا لِلْمُتَّقِينَ إِمَامًا - أُوْلَئِكَ يُجْزَوْنَ الْغُرْفَةَ بِمَا صَبَرُوا وَيُلَقَّوْنَ فِيهَا تَحِيَّةً وَسَلاَمًا - خَالِدِينَ فِيهَا حَسُنَتْ مُسْتَقَرًّا وَمُقَامًا }**

"*Na waja wa Ar-Rahman ni wale wanaokwenda ulimwenguni kwa unyenyekevu. Na wajinga wakisema nawo huwajibu: Salama--Na wale wanaopitisha baadhi ya saa za usiku kwa ajili ya Mola wao kwa kusujudu na kusimama.--Na wala wanaosema: Mola wetu tuondolee adhabu ya jahannamu. Bila shaka adhabu yake ni yenye kuodolea.--*

*Hakika hiyo ni kituo kibaya na mahali (pabaya kabisa) pa kukaa.--Na wale ambao wanapotumia hawatumii kwa fujo (kwa haramu)  wala hawafanyi ubahili (kwa wajibu) bali wanasimama baina hayo.--Na wale wasiomuomba mungu pamoja na Mwenyezi Mungu wala hawauwi nafsi aliyoiharamisha Mwenyezi Mungu ila kwa haki wala hawazini na atakayefanya hayo atapata madhara.--Na atazidishiwa adhabu Siku ya Qiyama na atakaa humo kwa kufedheheka milele--. Ila yule atakayetubia na kuamini na kutenda mema basi hawo ndio Mwenyezi Mungu atawabadilishia maovu yao kuwa mema. Na Mwenyezi Mungu ni mwingi wa kusamehe na mwingi wa kurehemu. --Na aliyetubia na kufanya wema basi kwa hakika yeye anatubu kweli kweli kwa Mwenyezi Mungu.--Na wale ambao hawashuhudii shahada za uwongo na wanapopita penye upuzi hupita kwa heshima yao.--Na wale ambao wanapo kumbushwa aya za Mola wao hawaziangukii kwa uziwi na upofu.--Na wale wanaosema: 'Mola wetu, tupe katika wake zetu na watoto wetu yaburudishayo macho yetu na tujaalie waongozi kwa wamchao Mungu.--Hawo ndio watakaolipwa ghorofa (za peponi) kwa kusubiri kwao na watakuta humo heshima na amani.---Wakae humo milele; kituo kizuri na mahali pazuri kabisa pa kukaa.*"
[TMQ Al-Furqan: 63-76]

Na asema Allah Ta'ala katika Surat Al-Isra:

**{ وَقَضَى رَبُّكَ أَلاَّ تَعْبُدُوا إِلاَّ إِيَّاهُ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا إِمَّا يَبْلُغَنَّ عِنْدَكَ الْكِبَرَ أَحَدُهُمَا أَوْ كِلاَهُمَا فَلاَ تَقُلْ لَهُمَا أُفٍّ وَلاَ تَنْهَرْهُمَا وَقُلْ لَهُمَا قَوْلاً كَرِيمًا - وَاخْفِضْ لَهُمَا جَنَاحَ الذُّلِّ مِنْ الرَّحْمَةِ وَقُلْ رَّبِّ ارْحَمْهُمَا كَمَا رَبَّيَانِي صَغِيرًا - رَبُّكُمْ أَعْلَمُ بِمَا فِي نُفُوسِكُمْ إِنْ تَكُونُوا صَالِحِينَ فَإِنَّهُ كَانَ لِلأَوَّابِينَ غَفُورًا - وَآتِ ذَا الْقُرْبَى حَقَّهُ وَالْمِسْكِينَ وَابْنَ السَّبِيلِ وَلاَ تُبَذِّرْ تَبْذِيرًا - إِنَّ الْمُبَذِّرِينَ كَانُوا إِخْوَانَ الشَّيَاطِينِ وَكَانَ الشَّيْطَانُ لِرَبِّهِ كَفُورًا - وَإِمَّا تُعْرِضَنَّ عَنْهُمُ ابْتِغَاءَ رَحْمَةٍ مِنْ رَبِّكَ تَرْجُوهَا فَقُلْ لَهُمْ قَوْلاً مَيْسُورًا - وَلاَ تَجْعَلْ يَدَكَ مَغْلُولَةً إِلَى عُنُقِكَ وَلاَ تَبْسُطْهَا كُلَّ الْبَسْطِ فَتَقْعُدَ مَلُومًا مَحْسُورًا - إِنَّ رَبَّكَ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَنْ يَشَاءُ وَيَقْدِرُ إِنَّهُ كَانَ بِعِبَادِهِ خَبِيرًا بَصِيرًا - وَلاَ تَقْتُلُوا أَوْلاَدَكُمْ خَشْيَةَ إِمْلاَقٍ نَحْنُ نَرْزُقُهُمْ وَإِيَّاكُمْ إِنَّ قَتْلَهُمْ كَانَ خِطْئًا كَبِيرًا - وَلاَ تَقْرَبُوا الزِّنَى إِنَّهُ كَانَ فَاحِشَةً وَسَاءَ سَبِيلاً - وَلاَ تَقْتُلُوا النَّفْسَ الَّتِي حَرَّمَ اللهُ إِلاَّ بِالْحَقِّ وَمَنْ قُتِلَ مَظْلُومًا فَقَدْ جَعَلْنَا لِوَلِيِّهِ سُلْطَانًا فَلاَ يُسْرِفْ فِي الْقَتْلِ إِنَّهُ كَانَ مَنصُورًا - وَلاَ تَقْرَبُوا مَالَ الْيَتِيمِ إِلاَّ بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ حَتَّى يَبْلُغَ أَشُدَّهُ وَأَوْفُوا بِالْعَهْدِ إِنَّ الْعَهْدَ كَانَ مَسْئُولا - وَأَوْفُوا الْكَيْلَ إِذَا كِلْتُمْ وَزِنُوا بِالْقِسْطَاسِ الْمُسْتَقِيمِ ذَلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيلاً - وَلاَ تَقْفُ مَا لَيْسَ لَكَ بِهِ عِلْمٌ إِنَّ السَّمْعَ وَالْبَصَرَ وَالْفُؤَادَ كُلُّ أُولَئِكَ كَانَ عَنْهُ مَسْئُولاً - وَلاَ تَمْشِ فِي الأَرْضِ مَرَحًا إِنَّكَ لَنْ تَخْرِقَ الأَرْضَ وَلَنْ تَبْلُغَ الْجِبَالَ طُولاً -كُلُّ ذَلِكَ كَانَ سَيِّئُهُ عِنْدَ رَبِّكَ مَكْرُوهًا }**

"*Na Mola wako amehukumu msimuabudu yeyote ila Yeye tu na kuwafanyia wema wazazi.Kama mmoja wao au wote wawili akifikisha uzee pamoja nawe basi usiwaambie hata 'Uff' wala usiwakemee. Na usema nao kwa msemo wa heshima kabisa.--Na uwainamishie bawa la unyenyekevu kwa huruma na useme: 'Mola wangu warehemu kama walivyonilea katika utoto.'--Mola wenu anajua sana yaliyo nyoyoni mwenu na kama mkiwa wema Yeye ni mwenye kuwaghufiria wenye kuregea kwake.--Na umpe jamaa yako haki yake na maskini na msafiri aliyeharibikiwa wala usitawanye mali yako kwa ubadhirifu.--Hakika watumiao kwa ubadhirifu ni ndugu na mashetani. Na Shetani ni mwenye kumkufuru Mola wake.--Na kama unajiepusha nao (kwa kukosa cha kuwapa) ilhali unatafuta rehema ya Mola wako (riziki) unayoitumaini basi sema nao maneno laini.--Wala usifanye mkono wako (kama) uliofungwa shingoni mwako, wala usiukunje ovyo ovyo au utakuwa ni mwenye kulaumiwa na kufilisika.-- Hakika Mola wako humkunjulia riziki amtakaye na humdhikishia (amtakaye). Hakika Yeye kwa waja wake ni mwenye kuwajua na kuwaona.--Wala msiwauwe watoto wenu kwa kuogopa umasikini. Sisi ndio tunaowaruzuku wao na nyinyi. Kwa yakini kuwaua ni khatia kubwa--Wala msikurubie zina. Hakika hiyo ni uchafu na njia mbaya.--Wala msiuwe nafsi nafsi ambayo Mwenyezi Mungu ameiharamisha isipokuwa kwa haki. Na mwenye kuuwawa kwa dhulma basi tumempa nguvu mrithi wake basi asifanye fujo katika kuuwa. Hakika yeye atasaidiwa.--Wala msikurubie mali ya yatima isipokuwa kwa njia iliyo bora mpaka afikie kubalighi. Na timizeni ahadi; kwa hakika ahadi itaulizwa (Siku ya Qiyama).--Wala usifuate usiyo na elimu nayo. Hakika masikio na macho na moyo; hivyo vyote vitaulizwa.Wala usitembee katika ardhi kwa maringo. Hakika wewe huwezi kuipasua ardhi wala huwezi kufikia urefu wa milima.--Haya yote ubaya wake ni wenye kuchukiza mbele ya Mola wako.*" [TMQ Al-Isra: 23-38]

Aya hizi katika Sura hizi tatu, kila mojawapo kamili imekusanya sifa tofauti tofauti. Hutoa picha ya Muislamu na kubainisha shakhsiya ya Kiislamu kwa dhati yake ya kipekee tofauti na nyenginezo. Na hudhihirisha ndani yake kuwa ni maamrisho na makatazo ya Mwenyezi Mungu. Miongoni mwake ni hukmu zinazo ambatana na aqida, kama ilivyo kati yake hukmu zinazo ambatana na maingiliano na hukmu zinazo ambatana na akhlaqi. Na imedhihirika kuwa hazielezi tu sifa za kiakhlaqi bali zimejumuisha aqida, ibadati, maingiliano kama zilivyo kusanya akhlaqi. Nazo ni sifa zilizo katika shaksiya ya Kiislamu. Na kuwepo tu akhlaqi hakupatikana mtu kamili wala shaksiya ya Kiislamu; na ili lihakikishike lengo ambalo kwa sababu zimewekwa hakuna budi ila iwe imejengwa juu ya msingi wa kiroho nayo ni aqida ya Kiislamu. Na iwe kusifika kwake kuwa kumejengwa juu ya aqida hii, na kwa kuwa Mwislamu hasifiki kwa ukweli kwa ajili ya ukweli bali husifika nao kwa sababu Mwenyezi Mungu ametuamrisha nao hata kama huchunga ahakikishe thamani ya kiakhlaqi pindi anaposema ukweli. Akhlaqi hasifiki nayo kwa ajili ya dhati yake bali kwa sababu Mwenyezi Mungu ametuamrisha nazo.

Kwa haya hakuna budi kwa Muislamu ila kusifika kwa sifa zake na kuzitekeleza kwa twaa na kunyenyekea kwa sababu ni katika yanayo mfikisha katika uchajimungu. Na kwa kuwa hupatikana kama natija ya ibada:

{ إِنَّ الصَّلَاةَ تَنْهَى عَنْ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ }

"*Hakika swala hukataza machafu na maovu*" [TMQ 29:45]

Na ni katika yale ambayo ni lazima kuchunga katika maingiliano: "**Dini ni maingiliano (*mu'amalat*)**." Na juu ya yote hayo ni kuwa ni maamrisho na makatazo maalumu; hilo hulimakinisha katika nafsi ya Muislamu na kulifanya ni jambo la lazima. Na kwa hayo imekuwa kuunganisha akhlaqi na yaliyobaki katika nidhamu maishani pamoja na kuwa sifa pekee hutosheleza kwa kumuandaa Muislamu maandalizi mema khasa khasa kusifika na akhlaqi ni kuitikia maamrisho ya Mwenyezi Mungu na kuepukana na makatazo yake si kwa sababu ya kuwa akhlaqi hunufaisha au kudhuru maishani. Haya ndiyo yanayofanya kusifika na akhlaqi njema ni daima na thabiti maadamu Muislamu anathibiti katika kutekeleza utabikishaji wa Uislamu, wala haizunguki inavyozunguka manufaa, kwa sababu manufaa sio katika makusudio yake bali ni lazima kujiepusha nayo kwa sababu shabaha yake ni thamani ya kiakhlaqi pekee sio thamani ya kimada au kiutu au kiroho. Bali haijuzu kutiwa thamani hizi ndani yake ili kusipatikane mgongano katika kuzitekeleza au kusifika nazo. Katika yale ambayo ni lazima kuzinduka nayo ni kuwa ni wajibu kuwekwa mbali thamani ya kimada na akhlaqi. Na kuwekwa mbali kutekeleza kwa sababu ya manufaa na faida kwa sababu hilo ni hatari kwake.

Kwa ufupi, akhlaqi sio katika nguzo za mujtama bali ni katika mambo ya kibinafsi. Kwa hivyo mujtama hautengenei kwa sababu ya akhlaqi bali hutengenea kwa sababu ya fikra za Kiislamu, hisia za Kiislamu na kwa kutabikishwa nidhamu za Kiislamu. Na pamoja ya kuwa akhlaqi ni katika mambo ya kibinafsi lakini sio peke yake, wala haijuzu kuwa peke yake bali hakuna budi ila iwe pamoja nayo aqida, ibadati, maingiliano na akhlaqi. Kwa hivyo hatambuliki yule ambaye akhlaqi zake ni njema na aqida yake sio ya Kiislamu kwa sababu yeye huwa wakati ule ni kafiri na hakuna dhambi kubwa kushinda ukafiri. Na hivyo hivyo yule ambaye akhlaqi zake ni njema lakini yeye hatekelezi ibadati au hapeleki maingiliano yake kwa mujibu wa hukmu za Kiislamu. Kufikia hapa ni lazima kuchunga katika kujenga mtu binafsi kuwepo aqida, ibadati, maingiliano na akhlaqi. Wala haijuzu kiShari'ah kuangalia akhlaqi peke yake na kuwacha sifa nyengine, bali haijuzu kuangaliwa chochote kabla ya utulivu wa aqida. Na jambo la msingi katika akhlaqi ni kuwa ni lazima ijengwe juu ya aqida ya Kiislamu, na kusifika nazo muumini kama maamrisho na makatazo ya Mwenyezi Mungu.